JARIDA MAALUM LA

# Nchi Yetu



Kutoka Wanafunzi 14 wa Elimu ya Juu Mwaka 1961 Hadi 206,302 Mwaka 2021

Uk. 24

Mfahamu Mwanamke wa Kwanza Tanzania Kusoma Taarifa ya Habari ya Kiingereza

Uk. 54

## Miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania;

Uongozi badala ya Utawala. **Uk.01**



Toleo la Disemba, 2021.

1961-2021

MIAKA 60 YA UHURU; Tanzania imara, Kazi iendelee.

Tanzania imara, kazi iendelee.

HALIUZWI

Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, akiwa na hati ya Uhuru kamili wa Tanganyika Disemba 9, 1961 katika ukumbi wa Karimjee jijini Dar es salaam




Picha na Getty Images. Imeboreshwa na Richard Maguluko Dindili.

**Bodi ya Wahariri:**

**Mwenyekiti**
Gerson Msigwa
Mkurugenzi wa Idara ya Habari
(MAELEZO) na Msemaji Mkuu wa Serikali.

**Wajumbe**
Rodney Thadeus
Zamaradi Kawawa
Jonas Kamaleki

**Msanifu**
Kelvin N. Kanje

Idara ya Habari MAELEZO
S.L.P. 25
Dodoma, Tanzania
Simu: **+255 22 292192**
Barua pepe: **maelezo@mawasiliano.go.tz**
**www.maelezo.go.tz**

Tufuatilie katika kurasa zetu
kwenye mitandao ya jamii

/ Msemaji Mkuu wa Serikali
/Maelezo News

# Neno la Utangulizi

Kwa niaba ya Idara ya Habari-MAELEZO nawakaribisha wasomaji wetu katika Jarida la Nchi Yetu. Jarida hili hukuletea mkusanyiko wa taarifa mbalimbali zinazohusu kazi zinazofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zikiwemo utekelezaji wa miradi ya maendeleo na masuala mbalimbali ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni.

Tofauti na majarida yaliyopita, jarida hili la Nchi Yetu litakuletea taarifa mahususi zinazohusu mafanikio ya Miaka 60 ya Uhuru. Tumechapisha Makala zinazoeleza hali ilivyokuwa kabla na wakati Tanzania ikipata Uhuru, hatua tulizopiga baada ya Uhuru, tulipo sasa na tuendako katika sekta mbalimbali.

Ni dhahiri maendeleo ambayo Tanzania imeyapata katika kipindi cha miaka 60 katika sekta mbalimbali ni makubwa na yaliyoleta manufaa makubwa katika ustawi wa Watanzania, hivyo kupitia jarida hili utaweza kujua kilichofanyika kwa kila sekta na mchango wake katika Taifa na ustawi wa jamii.

Ni matarajio yangu kuwa utafurahia kusoma makala zilizoandikwa katika jarida hili, naomba kuchukua nafasi hii adhimu kuwapongeza Watanzania wote kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kujenga nchi yetu kwa miaka hii 60. Kwa hakika mafanikio yaliyopatikana yamedhihirisha uzalendo, utaifa, mshikamano, umoja na upendo wa Watanzania kwa nchi yao ukichagizwa na amani na utulivu uliopo.

Naungana na Watanzania wenzangu kuishukuru Serikali kwa jitihada kubwa zilizofanyika kulinda tunu za Taifa letu ambazo zimetuwezesha kufikisha miaka 60 ya Uhuru tukiwa Taifa lenye heshima Afrika na Duniani, na Taifa lenye mwelekeo mzuri wa kupiga hatua kubwa zaidi. Ni matarajio yangu kuwa katika miaka hii 60 Watanzania tumejifunza mengi na tupo tayari kupiga hatua maradufu katika miaka 60 ijayo tukitumia fursa tulizonazo za kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni katika kukuza zaidi maendeleo ya Taifa letu na kuleta ustawi wa jamii.

Sisi Idara ya Habari-MAELEZO tupo tayari kuendelea kutekeleza wajibu wetu wa kuhakikisha Watanzania wanapata taarifa mbalimbali kuhusu Serikali yao, kutangaza nchi yetu na kuisimamia vizuri tasnia ya habari kwa kuzingatia Sheria, kanuni na taratibu huku tukihakikisha tasnia hii inazingatia weledi na maadili yanayopaswa ili iendelee kutoa mchango wake katika maendeleo ya nchi na ustawi wa jamii.

Tutaendelea kushirikiana na wadau wetu wa habari wakiwemo waandishi wa habari, wamiliki wa vyombo vya habari, taasisi mbalimbali za habari na wananchi katika kuhakikisha mazuri yote tuliyoyapata katika miaka 60 ya Uhuru tunayaendeleza na tunafanyia kazi changamoto zilizojitokeza ili Sekta ya Habari ikue zaidi na kutoa mchango unaotarajiwa. Nawatakia Watanzania wote heri katika kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru.

**Miaka 60 ya Uhuru, Tanzania Imara, Kazi Iendelee.**

Gerson Partinus Msigwa
**Mkurugenzi wa Idara ya Habari-MAELEZO**
**na Msemaji Mkuu wa Serikali**



# NDANI *ya* JARIDA



## YALIYOMO


001 **Miaka 60 ya Uhuru** *Uongozi badala ya Utawala*

004 **Miaka 60 ya uhuru** *Mafanikio Utumishi wa Umma*

007 **Tanzania Kidedea Uhifadhi Afrika** *Miaka 60 ya Uhuru*

036

**NISHATI, UVUVI, AFYA...**

009 **Tanzania Yapiga Hatua** *Sekta ya Nishati*

012 *Sekta ya Uvuvi* **Yainua Wananchi Kiuchumi**

014 *Huduma Bora za Afya Zawafikia Wananchi*

016 **Miaka 60 ya Uhuru:** *Maendeleo ya Teknolojia Sekta ya Afya Yapunguza Safari za Matibabu Nje ya Nchi*

018 **Kuimarika kwa Miundombinu Kwachochea Ukuaji wa Uchumi**

020 *Simulizi Nzito ya Kushushwa kwa Bendera ya Muingereza na Kupandishwa Bendera ya Tanganyika - Asimulia Hamza Kasongo*

022 **Miaka 60 ya Uhuru:** *Kilimo Chaongeza Lishe na Kupunguza Utapiamlo*

024 **Kutoka Wanafunzi 14 wa Elimu ya Juu Mwaka 1961 Hadi 206,302 Mwaka 2021**

**ARDHI, ULINZI, DIPLOMASIA...**

026 **Upimaji Ardhi kwa Kasi Wapunguza Makazi Holela**

030 **Miaka 60 ya Uhuru:** *Tanzania Yaongozwa na Rais wa Kwanza Mwanamke*

032 **Tanzania Yaendelea Kuwa Kinara wa Diplomasia Duniani**

**UWEKEZAJI, NISHATI...**

038 **Miaka 60:** *Uwekezaji wa Mitaji Kutoka Nje Wafikia Bilioni 1.01*

040 **Matumizi ya Koroboi Yapungua kwa Zaidi ya 80%**

041 **Historia Yaandikwa Maendeleo ya Watanzania**

042 **Tanzania ya Miaka 60,** *Ndoto ya Mwalimu Nyerere*

044 **Uhuru Ulivyoimarisha Miundombinu ya Usafiri**


046 **Miaka 60 ya Uhuru:** *Viwanda Vyaongeza Ajira 482,601 Mwaka 2020*

**TULIPOTOKA...**

052 *Tumetoka Mbali..... Mzee Msekwa*

053 **Miaka 60 ya Uhuru:** *Uzoefu wa Mzee Kassim Mpenda Kwenye Tasnia ya Habari*

054 *Mfahamu Mwanamke wa Kwanza Tanzania Kusoma Taarifa ya Habari ya Kiingereza*







NCHI YETU

Toleo Maalum la Jarida la Nchi Yetu tukiwa tunatimiza Miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara
*Picha na Getty Images*


056 **Miaka 60 ya Uhuru:** *Muungano Wetu ni Imara na Mfano wa Kuigwa*

058 **Utamaduni, Sanaa, Michezo Vyakonga Nyoyo za Watanzania** *Miaka 60 ya Uhuru*

061 **Maendeleo ya Teknolojia** *Yarahisisha Mawasiliano*

063 **Miaka 60 ya Uhuru:** *Ustawi wa Jamii Katika Elimu, Afya na Miundombinu*

065 **Sekta ya Madini** *Yachangia Tsh Bilioni 584.8 Kwenye Pato la Taifa 2021*


## MENGINEYO..


068 **Miaka 60 ya Uhuru:** *Vijana Wapatiwa Ujuzi, Wajiepusha na Dawa za Kulevya, Wajikita kwenye Uzalishaji*

071 **Natamani Kuanzisha Elimu ya Watu Wazima ya TEHAMA:** *Balozi Mongella*

077 *Tanzania Kuendeleza Jitahada za Kukuza Uchumi*

078 **Miaka 60** *na Mapinduzi ya Sekta ya Maji*





Tembelea tovuti yetu, www.maelezo.go.tz



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Mhe. Samia Suluhu Hassan



# Miaka 60 ya Uhuru: Uongozi Badala ya Utawala

Na **Balozi na Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu, Ombeni Sefue**

**Mwalimu alikuwa na kipaji kikubwa cha kuona mbali na kilimwezesha kujenga misingi imara ya Taifa huru, Taifa lenye umoja na mshikamano, linaloweza kuhimili kila aina ya changamoto kama Taifa moja.**

Tunaposherehekea miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara, mengi mazuri yamesimuliwa na kuandikwa kuhusu tulikotoka, tulipo na tunakoelekea. Takwimu nyingi zimetolewa kuashiria mema mengi yaliyotendeka na hatua kubwa zilizopigwa katika sekta mbalimbali. Yote yanavutia, na ni ya kujivunia.

Mimi nitajikita kwenye eneo nilipendalo, nalo ni uongozi. Nasema uongozi, si utawala. Sina uhakika kama Watanzania wengi, hasa vijana, wanaelewa kuwa nchi yetu imebahatika sana kuwa na viongozi, waonyesha njia, na si watawala kwa maana ya hali ilivyo kwenye baadhi ya nchi nyingine.

Kiongozi ni binadamu, kamwe hawezi kuwa malaika. Kama lengo lako ni kumtafutia kosa, utalipata tu. Ni rahisi sana kurusha madongo au kulalamikia hili na lile. Ni kawaida ya binadamu. Lakini ukweli ni kuwa kwa ujumla tumebahatika sana, na tunapaswa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Ulalamishi ndiyo kazi nyepesi kuliko zote, lakini ni kazi ambayo kamwe haijengi nchi.

Baba wa Taifa, Mwalimu Julius K Nyerere, alituasa tangu mwanzo kuwa maendeleo ni watu, si vitu. Na akasema ili tuendelee tunahitaji watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Viongozi wetu wa awamu zote wameonyesha njia, na hawakuacha kuzingatia hekima hiyo ya uongozi aliyojaliwa Mwalimu Nyerere.

Tofauti na baadhi ya nchi ambapo maradhi ya kutoheshimu katiba ilikuwepo na sasa imeanza kurudi, Tanzania hatujawahi kuwa na tatizo katika kurithishana madaraka; kupokezana vijiti katika kuwaongoza Watanzania. Hiyo nayo si kuishi viapo vya uongozi na kuheshimu katiba tu, bali ni kielelezo cha kuwajali wananchi unaowaongoza.

Ujenzi wa taifa hauna tofauti na ujenzi wa nyumba. Lazima uanze na msingi, tena msingi imara. Iwapo kila baada ya muda utafumua msingi ili uanze upya, ujenzi hauwezi kwenda mbele, na nyumba haitakuwa imara.

Aidha, ndani ya dhana ya kukabidhiana kijiti ni mwendelezo wa mbio, tena pengine kwa kasi zaidi. Hata kwenye mbio za kupokezana vijiti, si lazima kukimbia kwa staili ile ile ya mtangulizi wako; la muhimu ni kwenda mbele, japo kwa staili tofauti.
Kila awamu ilikabiliwa na changamoto na majukumu ya kihistoria kwa wakati na muktadha wake. Lakini kila awamu ilijenga juu ya kilichofanywa na awamu iliyotangulia. Tangu Uhuru hakuna awamu iliyoturudisha nyuma.
Ningeweza kuandika kitabu kuhusu jambo hili; lakini leo nitajikita katika sifa kuu, tena chache tu, za uongozi katika kila awamu hadi leo.

## BABA WA TAIFA

Nianze na Awamu ya Kwanza ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Baba wa Taifa, kwanza wa iliyokuwa Tanganyika, na baadaye kwa kushirikiana na Mzee Abeid Amani Karume, wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Baada ya Uhuru, jukumu lake kubwa, alilolifanya kwa umahiri mkubwa mno, ilikuwa kujenga Taifa. Mwalimu anaitwa Baba wa Taifa, si kwa sababu ya kuleta Uhuru, bali kwa kujenga Taifa.

Mwalimu alikuwa na kipaji kikubwa cha kuona mbali na kilimwezesha kujenga misingi imara ya Taifa huru, Taifa lenye umoja na mshikamano, linaloweza kuhimili kila aina ya changamoto kama Taifa moja.
Mwaka 1961 hapakuwa na taifa ambalo wakoloni walimwachia Mwalimu; walichomwachia ni makabila kadri ya 125 na machifu wao na lugha zao, yenye mchanganyiko wa Wakristo, Waislamu na wenye imani za kimila.

Hapakuwepo chochote kikubwa baada ya Uhuru cha kuwafanya watu hao wajihisi kuwa kweli wote ni Taifa moja linalopaswa kusimama pamoja katika kila hali. Mapambano ya kutafuta Uhuru yaliwaunganisha, lakini cha kuwaunganisha baada ya Uhuru ni nini?
Unajengaje Utaifa, wakati hakuna Taifa bali mkusanyiko tu wa makabila ndani ya mipaka isiyo na maana waliyoichora wakoloni kule Berlin mwaka 1984-85. Ni changamoto aliyopambana nayo Baba wa Taifa.
Baada tu ya Uhuru, Mwalimu alipinga yale yote yenye uwezo wa kuwagawa wananchi, kama vile ukabila, ukanda na udini; badala yake akaanzisha na kuendeleza yale yanayowaleta wananchi pamoja na kujenga hisia za Utaifa.

Kiongozi atakayeendekeza mambo hayo ya kuwagawa wananchi, kwa hakika atabomoa misingi ya Taifa letu. Watanzania tuna sababu ya kumshukuru Mungu kuwa hatujapata viongozi wa aina hiyo. Wote waliomfuata Mwalimu, kwa ujumla, wamezingatia mwiko huo.





Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Mwalimu, katika kuona mbali, alitambua kuwa ardhi inaweza kuwa chanzo kikubwa cha kugawa wananchi kati ya wenye nacho na wasiokuwa nacho. Ukiruhusu watu wamiliki kiasi chochote cha ardhi, tena kwa umiliki usio na mwisho, mbele ya safari utakuwa na watu maskini wasioweza hata kuwa na eneo la kuishi au kulima.

Mapema kabisa akawahi kuweka ardhi chini ya serikali; akaweka haki ya kutumia ardhi kwa kila raia, lakini si haki ya kuhodhi ardhi milele hata pale ambapo huitumii, jambo ambalo leo linasumbua nchi nyingi. Awamu zote zikarithi na kuendeleza jambo hilo.

Akaanzisha rasmi lugha ya Taifa, Kiswahili; akaikuza na kuiendeleza sambamba na mengine mengi yanayojenga uzalendo. Msipoongea lugha moja mnajengaje hisia za Utaifa?

Akawachanganya vijana wa Kitanzania; wakatoka Bukoba kwenda kusoma Mtwara. Wa Mtwara wakaenda kusoma Arusha na kadhalika, ili mradi vijana wakaanza kuchanganyana na kuzoeana na hivyo kufuta baadhi ya mambo yanayoleta ubaguzi wa kikabila, wakati mwingine kwa imani zisizo na msingi.

Mengine aliyoyaanzisha ili kujenga uzalendo ni kama vile Jeshi la Kujenga Taifa, mfumo wa Chama Kimoja cha Siasa; Sera ya Ujamaa na Kujitegemea, na kadhalika.
Wapo wanaofanya makosa kuangalia Azimio la Arusha kwa jicho la sera ya Ujamaa peke yake; lakini Azimio la Arusha lilikuwa zaidi sana ya Ujamaa. Liliimarisha uzalendo na hali ya watu kujiona kuwa kweli wako sawa na ni wamoja.

Hakuna shaka yoyote kwamba Mwalimu alikuwa mmoja wa viongozi mashuhuri sana katika nusu ya pili ya karne ya 20, mwenye ushawishi mkubwa sana, si hapa nyumbani na bara la Afrika tu, bali duniani kote. Mwalimu alisifika kwa kudai uhuru wa kweli wa watu; si uhuru bandia au uhuru nusu. Alikuwa mmoja wa vinara wa sera za kutofungamana na upande wowote. Lakini hakulewa madaraka wala sifa. Hakupenda mali, wala makuu. Hakuvumilia rushwa.

Badala yake Mwalimu alipenda na kujali watu, si wa nchi yake tu, bali duniani kote. Alisema tangu enzi hizo: "Binadamu wote ni ndugu, na Afrika ni moja". Huo ulikuwa msingi wa yote aliyokuja kuyafanya nchini mwetu, barani Afrika na duniani.

Pamoja na kufanikiwa kupata Uhuru wa nchi yake, Mwalimu aliiona hiyo kama hatua ya mwanzo tu inayoiweka nchi yake huru katika mstari wa mbele wa kupigania uhuru na umoja wa Bara la Afrika. Angeweza kusema kila mtu na lwake, nimeshapata Uhuru wa Tanganyika, hao wengine wapambane wenyewe.
Lakini yeye alisema anataka uhuru wetu uwe mwenge ulio juu ya Mlima Kilimanjaro, wenye uwezo wa kumulika ndani na nje ya mipaka yetu na kuleta matumaini kwetu na kwa wengine, upendo badala ya chuki, heshima badala ya dharau. Alipenda na kujali watu.

Ni kweli Mwalimu aliwekeza kwenye miundombinu ya mwanzo, lakini aliwekeza sana kwenye mambo yanayoongeza uhuru wa mtu – afya na elimu, ikiwemo elimu ya ufundi na ya kujitegemea. Alibaini maadui watatu wa Taifa jipya la Tanzania wanaostahili kupigwa vita: Ujinga, maradhi na umaskini. Kila Mtanzania alisikia kuhusu vita hivyo, akavikubali. Na hivi ni vita vya kudumu, vikaja kuendelezwa na awamu zote zilizofuata.
Jambo jingine muhimu katika uongozi wa Mwalimu, na ambalo awamu zote zimelizingatia, ilikuwa uhifadhi wa mazingira na maliasili ya taifa; aliviona kama urithi wa dunia na urithi wa vizazi vijavyo. Mapema kabisa wakati tunapata uhuru Mwalimu alitoa ahadi ambayo tangu wakati huo imekuwa msingi wa uhifadhi wa wanyamapori na mazingira yao hadi leo.

Alitoa kilichoitwa Ilani ya Arusha (Arusha Manifesto) iliyoahidi ifuatavyo: "Tunapopokea udhamini wa wanyamapori wetu, tunatamka kwa dhati kuwa tutafanya kila lililo ndani ya uwezo wetu kuhakikisha wajukuu wa watoto wetu wataweza kufurahia urithi huu wenye thamani kubwa".

Na Mwalimu alitimiza ahadi hiyo kwa vitendo, akaongeza Hifadhi za Taifa kutoka 1 aliyoirithi kutoka kwa wakoloni hadi 9 ndani ya miaka 10 tu ya mwanzo, pamoja na ongezeko kubwa la mbuga za wanyama.
Alijali vizazi vijavyo. Leo utalii ni chanzo kikubwa cha uchumi wetu.
Mwalimu pia aliwekeza sana kwenye mashirika ya umma. Alitaifisha makampuni binafsi, na akaanzisha mengi mengine. Yangefanikiwa katika malengo ya Mwalimu, Tanzania ingekuwa mbali; lakini ilibidi mengi yabinafsishwe katika awamu za uongozi zilizofuata maana mengi yalikufa au kuendeshwa kwa hasara kubwa.

## RUKHSA

Yapo mageuzi ambayo Mwalimu aliyaanzisha na yakakamilishwa na Rais Mwinyi. Mojawapo ni mageuzi ya kisiasa kutoka kwenye mfumo wa chama kimoja kwenda kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa.
Lakini kwenye uchumi hali ilikuwa mbaya, fedha za kigeni zilikuwa karibu zimeisha, madeni yalikuwa mengi na ukawepo uhaba mkubwa wa bidhaa muhimu. Rais Mwinyi akatoa ruhusa kwa wenye fedha zao kuagiza bidhaa muhimu, tatizo likaisha. Akafungua milango kwa sekta binafsi kuwekeza na kufanya biashara, uchumi ukaanza kukua. Akaanza kubinafsisha mashirika ya umma kupunguza mzigo kwa Serikali na kuongeza uzalishaji na ubora wa bidhaa na huduma.

Hata hivyo mifumo ya udhibiti na sheria zake ilikuwa haipo au haikuwa imara. Kwenye kipindi cha pili kukaongezeka vitendo vya rushwa na ukwepaji kodi. Alikuwa amefungua madirisha hewa safi iingie lakini wakaingia pia inzi na mbu na wadudu.

## UWAZI NA UKWELI

Alipopokea kijiti, Rais Mkapa akaanza na kupambana na hao inzi na mbu. Akatunga sheria na kuweka mifumo ya udhibiti. Rais Mwinyi alikuwa ametunga sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Mapato; Rais Mkapa akaitekeleza na kuhakikisha inafanya kazi ipasavyo. Akapambana na rushwa.

Ubinafsishaji wa mashirika ya umma ukaendelea kwa kasi zaidi. Akaboresha mazingira ya uwekezaji na biashara; akaanzisha mifumo ya majadiliano na sekta binafsi ya ndani na nje, pamoja na kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara. Kasi ya kukua kwa uchumi ikaongezeka.

Tukapata msamaha na unafuu wa madeni makubwa ya nje aliyoyarithi, na yaliyobaki akaanza kuyalipa.
Uhuru wa kisiasa na wa habari ukapanuka zaidi. Uwekezaji kwenye miundombinu ya elimu, afya na mawasiliano ukaongezeka.

Mipango mingi ikaanzishwa ya kukuza uchumi na kutoa fursa za kujiendeleza za wananchi, ikiwemo Dira ya Maendeleo 2025, TASAF, MKURABITA na kadhalika.

### ARI MPYA, NGUVU MPYA NA KASI MPYA

Ilipopokea kijiti, Awamu ya Nne chini ya Rais Kikwete ikaamua kuendeleza misingi na yote yaliyofanywa na awamu zilizopita kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Na hivyo ndivyo ilivyokuwa.

Uhuru wa kisiasa, uhuru wa habari na uhuru wa kuwekeza na kufanya biashara nao ukaendelea zaidi, na kasi ya kukua uchumi ikaongezeka. Safari ya Tanzania kufikia uchumi wa kati ikashika kasi.

### TINGATINGA

Serikali ya Awamu ya Tano, chini ya Hayati Rais Magufuli, ikajenga juu ya uchumi ambao sasa ulikuwa na hali nzuri zaidi na kuharakisha kufikia uchumi wa kati.

Awamu hiyo ilifanya kazi kubwa sana ya kuondoa vikwazo vya miundombinu katika kukuza uchumi. Haikuwa mzaha watu walipomwita Rais Magufuli 'tingatinga'; si kwa sababu tu huko nyuma alikuwa Waziri wa Ujenzi kwa miaka mingi bali kwa uchapa kazi wake, au kwa sababu ya staili yake ya uongozi. Yaliyofanyika katika miaka yake 5 ni makubwa mno.

Ujenzi wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji, ikiwemo barabara, reli, meli na vivuko, ndege, madaraja na kadhalika ni mambo ambayo atakumbukwa nayo. Aidha alijenga miundombinu ya huduma za afya na elimu, pamoja na vifaa vyake. Akaweka lengo la kila Mtanzania kupata umeme wa uhakika, na kuwekeza katika kupanua vyanzo na mtandao wa umeme, ikiwemo ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere.

### KAZI IENDELEE

Alipochukua madaraka katika mazingira magumu ya msiba wa Rais Magufuli, Rais Samia Suluhu Hassan, aliwahakikishia Watanzania kuwa kazi kubwa iliyoanzishwa na mtangulizi wake itaendelea. Na ndivyo anavyofanya hadi sasa. Pamoja na matatizo ya UVIKO-19, uchumi umeanza kukua kwa kasi, akiba ya fedha za kigeni imeongezeka sana, mauzo nje ya nchi yanashika kasi, ikiwemo kwenda nchi jirani.
Mafanikio haya yamejengwa juu ya kazi iliyofanywa na awamu zilizopita. Uwekezaji unaongezeka kutokana na sera nzuri, pamoja na hali nzuri ya miundombinu ya usafirishaji watu, huduma na bidhaa, ikiwemo kwenda nchi za jirani.
Diplomasia ya uchumi nayo imefungua milango ya biashara na nchi jirani, ikijengwa juu ya historia ndefu ya diplomasia ya Tanzania, tangu enzi za Mwalimu Nyerere hadi sasa.

> **Baada tu ya Uhuru, Mwalimu alipinga yale yote yenye uwezo wa kuwagawa wananchi, kama vile ukabila, ukanda na udini; badala yake akaanzisha na kuendeleza yale yanayowaleta wananchi pamoja na kujenga hisia za Utaifa.**
>
> Balozi na Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu, Ombeni Sefue

Lengo la makala hii halikuwa kuorodhesha kwa undani yaliyofanyika nchini mwetu tangu mwaka 1961. Lengo lilikuwa kuwakumbusha Watanzania, hasa vijana, kuhusu misingi ya Taifa letu iliyojengwa hatua kwa hatua tangu tupate uhuru na aina ya uongozi uliotufikisha hapa.

Nimeweka mkazo mkubwa zaidi kwenye Awamu ya Kwanza ambapo ndipo misingi mikuu ya Taifa hili ilipowekwa, misingi ambayo imeimarisha Taifa na kujenga uzalendo na kutuwezesha kuhimili misukosuko mingi, ikiwemo kifo cha Rais Magufuli.
Misingi hiyo ndiyo pia imetuwezesha kuyafanya mengine yote katika hali ya amani na utulivu. Ni misingi ya kuenziwa, na si ya kuchezewa hata kidogo.

Tangu Uhuru, hakuna mafanikio ya awamu yoyote ya uongozi ambayo hayakujengwa juu ya misingi, au maandalizi yaliyofanyika katika awamu zilizopita. Tanzania tunapokezana vijiti kwa namna inayozidi kujenga, na kamwe si kubomoa. Mwenyezi Mungu atujalie tuendelee hivyo daima.



# Miaka 60 ya Uhuru: Mafanikio Katika Utumishi wa Umma

Tanganyika ilipopata uhuru mwaka 1961, ilirithi Utumishi wa Umma ambao jukumu lake kubwa lilikuwa ni kuhudumia na kulinda masilahi ya Serikali ya kikoloni. Katika kipindi hicho, nchi ilikuwa inakabiliwa na upungufu wa watumishi wazawa wenye sifa na taaluma mbalimbali za kuwawezesha kutekeleza majukumu ya taasisi mpya zilizoanzishwa.

Nchi nzima ilikuwa na Madaktari 12 tu na Wahandisi wawili, wakati asilimia 85 ya wananchi walikuwa hawajui kusoma na kuandika. Pia hawakuwepo watumishi wazawa wa kujaza nafasi zilizoachwa wazi na maafisa wa kikoloni ambao walilazimika kuacha kazi baada ya uhuru, kuwepo kwa mifumo ya utawala na mitizamo ya watumishi ya kikoloni, na huduma nyingi za kijamii kama vile afya, makazi bora, barabara na elimu zilielekezwa katika maeneo waliyokuwa wakiishi wakoloni. Mwelekeo na mtazamo wa Utumishi huo ulisababisha changamoto kubwa tatu ambazo ni ujinga, umaskini na maradhi miongoni mwa wananchi.

Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuongezeka kwa ajira katika Utumishi wa Umma kutoka watumishi 17,565 mwaka 1961 hadi 528,290 mwezi Oktoba, 2021. Kati ya hao, watumishi wa sekta ya Afya wamefikia 72,961 sawa na asilimia 13.8 na walimu wamefikia 281,729 sawa na asilimia 53.3, kuboreshwa kwa Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) na kujengewa uwezo wa Watumishi kutoka Taasisi za Serikali 427 kutumia Mfumo huo.

Mfumo huu umeongeza wigo wa taarifa na watumiaji na hivyo basi kuboresha usimamizi wa masuala ya rasilimaliwatu katika taasisi za Umma, kuwaondoa kwenye Orodha ya Malipo ya Mishahara (Payroll) watumishi 15,578 waliobainika kughushi vyeti vya kufaulu mtihani wa Kidato cha Nne, cha Sita na Ualimu kati ya watumishi 535,770 waliohakikiwa. Pia, kuwaondoa katika Orodha ya Malipo ya Mishahara Watumishi 5,335 walioajiriwa katika Utumishi wa Umma kinyume na Sifa za Miundo ya maendeleo ya kiutumishi, hivyo kubakia na watumishi wenye sifa stahiki, kuwaondoa katika Orodha ya Malipo ya Mishahara watumishi hewa 19,708 na kuiwezesha Serikali kuokoa jumla ya Shilingi bilioni 19.84.

Serikali katika miaka 60 ya uhuru, imeanzisha na kuimarisha vyombo mbalimbali vya kusimamia menejimenti ya utumishi wa Umma na Utawala Bora ambavyo ni: Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)....

...Chuo cha Utumishi wa Umma, Taasisi ya UONGOZI, Wakala ya Ndege za Serikali, Tume ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Ajira, Watumishi Housing, na Mamlaka ya Serikali Mtandao.

Vyombo hivyo vilivyoanzishwa na kuimarishwa kusimamia menejimenti ya utumishi wa Umma na Utawala Bora, vimeweza kuleta mafanikio mbalimbali kupitia utekelezaji wa majukumu yake.. Mfumo huu umesaidia kuingiza watumishi wapya kwenye Orodha ya Malipo ya Mishahara kwa wakati na kuwawezesha kupata mishahara yao ndani ya kipindi cha mwezi mmoja.

Mafanikio mengine yaliyopatikana ni kuimarika kwa Mfumo wa Kitaasisi wa Usimamizi wa Serikali Mtandao kwa kuanzisha Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya mwaka 2019 na Kanuni zake za mwaka 2020 zinazoweka utaratibu na masharti ya kisheria kuhusu utekelezaji, usimamizi na uendeshaji wa Serikali Mtandao nchini, kurahisishwa kwa mawasiliano na upatikanaji wa huduma zitolewazo na Serikali kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika Utumishi wa Umma. Vile vile, kuanzisha Vitengo vya Usimamizi wa TEHAMA katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**"Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imepata mafanikio ya kuridhisha katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru. Mafanikio hayo ni pamoja na kuongezeka kwa nidhamu katika utumishi wa umma, kuongezeka kwa idadi ya watumishi wazawa na kupambana na vitendo vya rushwa na ufisadi.**




Arusha clock tower, 1961

# Watumishi Wazawa Waongezeka. Nidhamu Serikalini Yaimarika, Rushwa Yadhibitiwa.

**Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuongezeka kwa ajira katika Utumishi wa Umma kutoka watumishi 17,565 mwaka 1961 hadi 528,290 mwezi Oktoba, 2021.**

Kurahisisha upatikanaji wa taarifa za ajira kwa kuanzisha kanzidata ya waombaji na waliofaulu usaili ambayo hutumika kuwapangia vituo moja kwa moja wasailiwa waliofaulu usaili hivyo kupunguza gharama za usaili, kuongezewa uwezo, ujuzi na maarifa Viongozi na watumishi wa Umma kwa kuanzisha Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute) na kuimarishwa kwa Chuo cha Utumishi wa Umma, kuongezeka kwa uwezo na weledi wa watumishi wa Umma na sekta binafsi kupitia Chuo cha Utumishi wa Umma kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu, kusogeza huduma kwa umma kwa kuanzisha matawi ya Chuo cha Utumishi wa Umma Dar es Salaam, Tabora, Mtwara, Singida, Tanga, Mbeya pamoja na kuanzisha Kituo cha Mafunzo kwa njia ya Mtandao.

Kuimarika kwa mahusiano kazini kati ya Viongozi na watendaji wengine kupitia mafunzo ya Taasisi ya UONGOZI ambapo yameongeza uwezo wa kufanya kazi kwa ufanisi. Pia, mafunzo hayo yamewaongezea uwezo wa kuchambua changamoto kwa kina, kuzitafutia ufumbuzi na kuboresha usimamizi wa rasilimali za Serikali ikiwa ni pamoja na rasilimaliwatu na rasilimali fedha, kukusanywa, kuchambuliwa na kutunzwa kwa taarifa, kumbukumbu, nyaraka na machapisho mbalimbali kuhusu historia ya nchi kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Vile vile, kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa letu vilikusanywa na kuhifadhiwa kwa lengo la kuhifadhi historia ya Waasisi wa Taifa, kuhifadhi nyaraka kidijitali ili zidumu, kurahisisha upatikanaji wake, kuwa na hifadhi mbadala na kulinda nakala halisi. Aidha, hadi kufikia mwaka 2021 jumla ya Majalada 2,843 yamehifadhiwa kwenye mfumo wa kidijitali.

Kupitia TASAF, Serikali imewasilisha ruzuku kwa kaya masikini ili kuziwezesha kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu na kujenga rasilimaliwatu hususan watoto kwa kugharamia elimu na huduma za afya, ambapo kiasi cha shilingi Trilioni 1.646 kilitumika katika utekelezaji wa Kipindi cha Kwanza cha Awamu ya Tatu, kuanzishwa kwa miradi ya kutoa ajira ya muda kwa walengwa na miradi ya kuendeleza miundombinu ya huduma za jamii. Katika Awamu ya I na II, jumla ya miradi 14,051 ya kutoa huduma za jamii yenye thamani ya shilingi bilioni 502.0 ilitekelezwa kwa kutoa huduma zilizokusudiwa kwa jamii husika katika Sekta mbalimbali.





Hifadhi uya Taifa ya Ngorongoro

# Tanzania Kidedea Uhifadhi Afrika

**Na Aron Msigwa – WMU.**

Wizara ya Maliasili na Utalii imeendelea kuwa nguzo muhimu katika uhifadhi na usimamizi wa matumizi endelevu ya rasilimali za Wanyamapori, Misitu, ufugaji Nyuki, Malikale na Maendeleo ya Utalii hapa nchini. Ikumbukwe kuwa juhudi za kuhifadhi na kulinda rasilimali za maliasili zilikuwepo hata kabla ya ukoloni ambapo jamii nyingi nchini zilitenga maeneo maalumu ya misitu kwa ajili ya shughuli za ibada na matambiko.

Maeneo hayo yaliheshimika kwa jamii husika na adhabu ilitolewa kwa wale waliokuwa wanakiuka au kuharibu maeneo hayo. Aidha, baadhi ya spishi za miti zilizuiwa kukatwa na aina fulani za wanyamapori hazikuruhusiwa kuwindwa.Wakati wa utawala wa Wakoloni baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia mwaka1945 zilianzishwa Sheria za uhifadhi wa rasilimali za Maliasili na Malikale.

Sheria zilizoanzishwa ni pamoja na Sheria Kuhifadhi Majengo ya Kihistoria 1937, Sheria ya Makumbusho ya mwaka 1941, Sheria ya Usimamizi wa Misitu 1957, Sheria ya Hifadhi ya Ngorongoro mwaka 1959, Sheria ya Hifadhi za Taifa 1959 na Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori ya mwaka 1959. Katika kipindi hicho sheria nyingi zilitungwa bila kuwashirikisha wananchi hali iliyosababisha jamii kutoshiriki kikamilifu katika kutunza rasilimali zao.

Baada ya Uhuru mwaka 1961, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alitoa tamko la Arusha kuweka msisitizo juu ya umuhimu wa kuhifadhi na kulinda rasilimali za maliasili ambazo nchi yetu imebarikiwa. Alisema: "Uhai wa wanyamapori ni jambo linalotuhusu sana sote katika Afrika. Viumbe hawa wa porini, wakiwa katika mapori wanamoishi, sio muhimu tu kwa ajili ya kuajabiwa na kuvutia lakini pia ni sehemu ya maliasili yetu na pia ndio mustakabali wa maisha yetu ya baadaye. Kwa kukubali dhamana ya wanyamapori wetu tunatamka kwa dhati kwamba tutafanya kila tuwezalo kuhakikisha kwamba wajukuu wa watoto wetu wataweza kufurahia urithi huu mkubwa na wa thamani adimu."

Tamko hili lilitoa mwongozo na dira ya uendelezaji wa shughuli za uhifadhi ikiwemo kuundwa kwa Wizara ya Ardhi, Misitu na Wanyamapori mwaka 1962 ambayo ilikuwa na jukumu la kusimamia uhifadhi wa Maliasili, Malikale na uendelezaji wa Utalii. Hata hivyo katika kipindi hicho tangu mwaka 1962 hadi 2009 yalifanyika mabadiliko mbalimbali na mapitio ya sheria ili kuwezesha ushirikishwaji wa jamii katika uhifadhi wa maliasili, malikale na utalii.

Wizara iliandaa sheria mpya na kufuta sheria zilizokuwepo awali; mfano ni sheria mpya ya kuhifadhi Wanyamapori ya mwaka 1974 na Sheria ya Makumbusho ya mwaka 1965. Pia, Wizara ilizifanyia marekebisho Sheria za Mambo ya Kale 1964 na Sheria za Wanyamapori 1974 na 2002. Pia kuanzishwa kwa sheria mpya za Makumbusho ya Taifa 1980, Sheria ya Misitu Na.14 ya mwaka 2002, Sheria ya Ufugaji Nyuki Na.15 ya mwaka 2002, Sheria ya Utalii 2008 na Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 2009.

Mabadiliko haya ya Kisera na kisheria yalichochea upatikanaji wa mafanikio makubwa katika sekta na kuongeza ushirikishwaji wa wananchi na wadau mbalimbali katika kuhifadhi na kunufaika na rasilimali zilizopo. Aidha, awamu zote sita za uongozi kuanzia Awamu ya Kwanza ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hadi Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais, Mhe. Samia Suluhu Hassan, zimetoa kipaumbele kikubwa katika usimamizi na ulinzi wa maliasili kuhakikisha kwamba urithi mkubwa, adimu na wa thamani tulionao unakinufaisha kizazi cha sasa na baadaye.

Kufuatia juhudi hizi sekta hii imepata mafanikio makubwa yakiwemo ya kuongezeka kwa maeneo ya uhifadhi na utalii hususan Vituo vya Mambo ya Kale kutoka vitatu (3) mwaka 1961 hadi 133 na kituo 1 hadi saba 7 vya Makumbusho ya Taifa mwaka 2021, Mapori ya Akiba ya Wanyamapori kutoka 9 hadi 22, Hifadhi za Taifa kutoka tatu (3) hadi 22, Mapori Tengefu hayakuwepo na sasa yapo 27.

Mafanikio mengine ni kuanzishwa kwa misitu ya Hifadhi za Mazingira Asilia 20 yenye jumla ya eneo la takribani hekta 924,876.22 ambayo ni hadhi ya juu kabisa inayotambuliwa na shirika la kimataifa la uhifadhi la (International Union of Conservation for Nature (IUCN), kusimamia, kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za misitu na nyuki katika maeneo ya misitu 463 iliyohifadhiwa kisheria, Kuanzishwa kwa mashamba ya miti ya Serikali 23, kuanzishwa kwa maeneo Matatu (3) ya Ardhioevu chini ya Mkataba wa Ramsar na Kuundwa kwa Jumuiya za Uhifadhi wa Wanyamapori 38.

Pia, Wizara imefanikiwa kuboresha shughuli za uhifadhi na kutangaza utalii kwenye masoko mbalimbali ya Kimataifa ambapo vivutio vya utalii vya Tanzania vimepata umaarufu mkubwa na tuzo mbalimbali za kimataifa.

Mfano ni Hifadhi ya Taifa Serengeti kuwa hifadhi bora zaidi barani Afrika katika kipindi cha miaka 3 mfululizo kuanzia 2019, 2020 na 2021. Pia imetambuliwa na Gazeti Maarufu la Forbes la nchini Marekani kama kivutio cha pili duniani miongoni mwa vivutio bora 21 vya kutembelewa kwa mwaka 2021. Aidha, Hifadhi za Taifa Kilimanjaro, Serengeti na Tarangire zimeshinda tuzo ya ubora ya Travelers Choice (TripAdvisor) best of the best 2021.

Kwa upande mwingine Wizara imepata mafanikio kwa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) kutangazwa kuwa mshindi wa kundi la dhahabu miongoni mwa washindi 51 kutoka nchi 39 duniani wa tuzo ya huduma za viwango vya Kimataifa kwa mwaka 2020. Aidha, hifadhi 5 za Taifa ambazo ni Kilimanjaro, Serengeti, Mkomazi, Manyara na Arusha zimepata tuzo za ubora wa huduma za viwango vya Kimataifa kwa mwaka 2020 pamoja na kiwanja cha ndege cha Msembe kilicho katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kuwa kiwanja chenye mandhari nzuri zaidi Barani Afrika kwa mwaka 2020.

# Hifadhi za taifa 3 mwaka 1961 hadi 22 mwaka 2021

Aidha, rasilimali za maliasili na malikale zimekuwa na mchango mkubwa katika uendelezaji utalii, ukuaji wa uchumi, ustawi wa jamii na uhifadhi wa mazingira. Mathalan, utalii huchangia wastani wa asilimia 17.2 ya Pato la Taifa; asilimia 25 ya fedha za kigeni na huzalisha ajira takriban milioni 1.6 za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa mwaka. Kwa upande mwingine, sekta ya misitu na nyuki huchangia asilimia 3.5 ya Pato la Taifa; asilimia 5.9 ya mapato yatokanayo na biashara ya nje na ajira takriban milioni 4 kwa mwaka. Sekta hii inachangia zaidi ya asilimia 90 ya nishati ya kupikia nchini kutokana na miti.

Mafanikio mengine ambayo nchi imeyapata katika Sekta ya Maliasili na Utalii tangu mwaka 1961 ni kufanikiwa kuingiza maeneo saba (7) ya uhifadhi katika Orodha ya UNESCO ya Maeneo ya Urithi wa Dunia (UNESCO World Heritage Sites). Maeneo hayo ni Pori la Akiba Selous, Hifadhi ya Ngorongoro, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Magofu ya Kale ya Songo Mnara na Kilwa Kisiwani, Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro,Mji Mkongwe wa Zanzibar na Michoro ya Miambani ya Kondoa Irangi.

Ili kuongeza wigo wa mazao ya utalii na kuvutia watalii, Wizara imefanikiwa kuendeleza mazao mbalimbali yakiwemo utalii ikolojia; utalii wa jiolojia; utalii wa faru; utalii wa kuona wanyamapori nyakati za usiku; utalii wa farasi; utalii wa kupiga makasia; na uvuvi wa kujiburudisha. Aidha, katika kuendeleza utalii wa malikale, Wizara imeanzisha makumbusho mpya katika eneo la Urithi wa Dunia la Kilwa Kisiwani. Sambamba na hilo, Wizara imefungua fursa za shughuli za utalii katika Ukanda wa Kaskazini Magharibi kwa kuanzisha utalii wa maji katika Ziwa Victoria na Ghuba ya Speke.
Mafanikio mengine yaliyopatikana ni kuanzishwa kwa jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu ambalo halikuwepo hapo awali. Jeshi hili limekua na kazi kubwa ya kuimarisha ulinzi na kudhibiti vikundi vya uhalifu dhidi ya ujangili wa tembo, faru na wanyamapori wengine katika hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu.

Wizara kupitia taasisi zake za uhifadhi ambazo ni Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) imeendelea kuimarisha ulinzi wa rasilimali za maliasili kwa kudhibiti ujangili, biashara haramu ya nyara na uvunaji haramu wa mazao ya misitu na kufanikiwa kupunguza vitendo hivyo kwa asilimia 90.
Mafanikio mengine ni kuanzishwa kwa kanuni zinazosimamia maeneo ya uwekezaji mahili kuwezesha uwekezaji katika maeneo maalum yenye wanyamapori (Special Wildlife Investment Consession Areas - SWICA) kwa lengo la kuvutia na kurahisisha shughuli za uwekezaji katika maeneo yenye wayamapori nchini.



"Uhai wa wanyamapori ni jambo linalotuhusu sana sote katika Afrika. Viumbe hawa wa porini, wakiwa katika mapori wanamoishi, sio muhimu tu kwa ajili ya kuajabiwa na kuvutia lakini pia ni sehemu ya maliasili yetu na pia ndio mustakabali wa maisha yetu ya baadaye. Kwa kukubali dhamana ya wanyamapori wetu tunatamka kwa dhati kwamba tutafanya kila tuwezalo kuhakikisha kwamba wajukuu wa watoto wetu wataweza kufurahia urithi huu mkubwa na wa thamani adimu."

**Mwl. Julius Kambarage Nyerere**



# Tanzania Yapiga Hatua Sekta ya Nishati

**"Tanzania ndani ya miaka 60 imeanzisha miradi mbalimbali ya uzalishaji umeme ambapo hadi kufikia mwezi Oktoba 2021 jumla ya uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme iliyounganishwa katika Gridi ya Taifa imefikia MW 1,573.65 kati ya hizo MW 573.70 zinatokana na vyanzo vya maji, MW 901.32 gesi asilia na MW 10.50 tungamotaka (Biomass).**

Nishati ni injini muhimu katika nchi yoyote ile duniani kwani inachagiza ukuaji wa kiuchumi na kuboresha huduma za kijamii, hivyo kuwepo kwa maendeleo kunategemea pia uwepo wa nishati ya uhakika na inayotabirika.

Kwa kutambua hilo, tangu Tanganyika ipate uhuru wake mwaka 1961, Serikali za Awamu zote zimehakikisha kuwa Sekta ya Nishati inakua kwa kuwekeza katika miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa Umeme, Mafuta na Gesi.

Wakati tunapata uhuru jumla ya umeme uliokuwa unazalishwa nchini ulikuwa Megawati 54.Umeme huo ulitumika kwenye mashamba ya mkonge kule Tanga na kwenye Shirika la Reli Dar es Salaam, hivyo haukuuzwa kwa wateja wa majumbani. Jumla ya urefu wa njia za umeme za 33kV na 11kV ulikuwa kilomita 400. Kwa sasa 33kV na 11kV hazitumiki kama 'transmission' bali 'distribution lines'.

Ili kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na umeme wa kutosha baada ya Uhuru, lilianzishwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mwaka 1964 ambalo lilitokana na kuunganishwa kwa mashirika binafsi mawili ya Tanganyika Electric Supply Company Limited (TANESCO) na Dar es Salaam District Electric Supply Company Limited (DARESCO) chini ya sheria ya umeme ya mwaka 1931 iliyorekebishwa mwaka 1957 (Electricity Ordnance Cap 131 of 1931, na maboresho ya mwaka 1957).

Kuanzia mwaka 1968 Serikali ilianza kununua hisa za TANESCO na hadi kufikia mwaka 1975 hisa zote zilikuwa chini ya Serikali, hivyo kulifanya kuwa Shirika la Umma ambalo linamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100. Aidha, TANESCO ilianza kupanga mikakati ya kupata miradi mipya ya kuzalisha umeme na kujenga njia za kusafirisha na kusambaza umeme kwa viwanda na miji nchini kote.

Mikakati hiyo ya kuwa na miradi mipya imepelekea Tanzania kuwa na ongezeko la miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme ambapo ndani ya miaka 60 ya Uhuru imefikisha kilometa 6,110.57 za usafirishaji umeme, kati ya hizo kilometa 670 ni za msongo wa 400kV, kilometa 3,225 ni za msongo wa 220kV, kilometa 1,672.57 ni za msongo wa 132kV na kilometa 543 ni za msongo wa 66kV.
Aidha, ndani ya miaka 60, njia za usambazaji umeme zimeongezeka kufikia kilomita 47,487.88 za msongo wa 33, kilometa 12,486.11 za msongo wa 11 na kilometa 88,570.24 za msongo wa chini (400V/231V).

Katika suala la uzalishaji umeme, Tanzania ndani ya miaka 60 imeanzisha miradi mbalimbali ya uzalishaji umeme ambapo hadi kufikia mwezi Oktoba 2021 jumla ya uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme iliyounganishwa katika Gridi ya Taifa imefikia MW 1,573.65 kati ya hizo MW 573.70 zinatokana na vyanzo vya maji, MW 901.32 gesi asilia na MW 10.50 tungamotaka (Biomass). Vile vile TANESCO inamiliki mitambo ambayo haijaunganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa yenye uwezo wa kuzalisha MW 32.21 na hivyo kufanya jumla ya uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme nchini kufikia MW 1,605.86. Mitambo hii inaweza kukidhi mahitaji ya juu ya umeme ambayo yameendelea kuongezeka na kufikia MW 1,255 mwezi Oktoba 2021.

## MIRADI YA UMEME

**Miradi ya umeme iliyoanzishwa na kutekelezwa ndani ya miaka 60 imepelekea wateja wa umeme kufikia 3,440,728 hadi Septemba, 2021. Idadi ya Wateja waliounganishiwa umeme (connection level) sasa ni 37.7% ya wateja wote, wakati idadi ya wananchi waliofikiwa na huduma ya umeme (access level) ni 78.4%.**

Tanzania bado inaendelea kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme ikiwemo ya kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere – MW 2,115, Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Rusumo – MW 80, Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi I Extension – MW 185, Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Singida – Arusha – Namanga, Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma, Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Sumbawanga – Mpanda – Kigoma, Mradi wa Kujenga Kituo Kipya cha Kupoza Umeme Luguruni chenye Msongo wa kV 220/33 ambayo itaifanya Tanzania kuwa na umeme wa uhakika utakaosambazwa katika maeneo mengi zaidi.



Katika miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania bara, nchi haikubaki nyuma katika kuhakikisha kuwa wananchi katika maeneo yote vijijini na mijini wanapata huduma ya umeme na hivyo mwaka 2007 ilianzisha Wakala wa Nishati Vijijini (REA) ambao una jukumu la kuhamasisha na kuwezesha upatikanaji na matumizi ya nishati bora vijijini kwa kutoa ruzuku, mafunzo na ushauri wa kitaalamu kwa waendelezaji wa miradi.

Kutokana kuanzishwa kwa Wakala huo, imeshuhidiwa jinsi umeme ulivyoanza kusambaa kwa kasi katika vijiji mbalimbali nchini na kuanza kubadilisha hali ya uchumi ya wananchi hao kutokana na kuanzisha shughuli mbalimbali za maendeleo zinazotegemea nishati ya umeme.

Ndani ya Miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara utekelezaji wa miradi ya nishati ya umeme vijijini umewezesha vijiji vipatavyo 8,897 kupata umeme kati ya 12,345 hivyo kubakia na vijiji 3,448 visivyokuwa na huduma ya umeme.

Upelekaji umeme kwenye vijiji hivyo umepelekea kuongezeka kwa uwekezaji katika viwanda vya kuzalisha vifaa vya ujenzi wa miradi kutoka viwanda 23 mwaka 2020 hadi viwanda 56 mwaka 2021 vya nguzo, nyaya, mita mashineumba na viunganishi.

Aidha, uunganishaji umeme vijijini umewezesha Taasisi za Afya 3,396, Shule 8,569, visima vya maji 887, Nyumba za Ibada 2,917 na maeneo ya biashara takriban 13,242 kufikiwa na huduma za umeme hivyo kuboresha na kuongeza ufanisi katika utoaji huduma.

Ndani ya miaka 60 ya Uhuru, kumekuwa na udhibiti wa biashara ya mafuta lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa inafanyika kwa ufanisi na nchi inapata mapato stahiki kwa kupambana na uchakachuaji wa mafuta ambao ulikuwa ukiipa nchi hasara kwani magari mengi yalikuwa yakiharibika na hivyo nchi ilipata hasara kwa kuwa na ongezeko kubwa la mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya manunuzi ya vipuri vya magari.

Aidha, ndani ya miaka 60 tofauti na miaka ya kabla ya Uhuru, Tanzania imeanzisha mfumo wa uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja lengo likiwa ni kuongeza ufanisi kwenye uagizaji wa mafuta kwa kupunguza gharama za ucheleweshaji wa meli bandarini kutoka siku 40 hadi 3 na gharama za usafirishaji mafuta kwa wastani wa shilingi bilioni 81.90 kwa mwaka na hivyo kuleta unafuu wa bei za mafuta.

Shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi nchini zimeendelea kufanyika ndani ya miaka 60 ya Uhuru tangu kuanzishwa kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) mwaka 1969 ambapo kampuni mbalimbali zimeendelea na utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika maeneo mbalimbali nchini ikiwamo nchi kavu na baharini ambapo jumla ya kiasi cha gesi asilia futi za ujazo trilioni (TCF) 57.54 ziligunduliwa.

Kugunduliwa kwa kiasi hicho cha Gesi Asilia kumeleta manufaa mbalimbali kiuchumi ikiwemo Serikali kuokoa zaidi ya takribani Shilingi trilioni 38.16 kwa kutumia gesi asilia katika uzalishaji umeme badala ya mafuta ambayo yangeagizwa nje ya nchi ambapo asilimia 60 ya umeme wa Gridi ya Taifa unazalishwa kwa kutumia gesi asilia.

Manufaa mengine yaliyopatikana ndani ya miaka 60 kutokana na ugunduzi wa Gesi Asilia ni pamoja na Serikali kupitia TPDC kuunganisha wateja wa Gesi asilia kwenye mtandao wa miundombinu ya usambazaji yenye jumla ya kilomita 130 iliyotandazwa mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Mtwara.

Katika mtandao huo jumla ya viwanda 52, mitambo 8 ya kuzalisha umeme, taasisi 9 na nyumba 1,191 za awali zimeunganishwa kutumia gesi asilia. Aidha, vituo viwili 2 vya kujazia gesi kwenye magari vimejengwa katika mikoa ya Mtwara na Dar es Salaam, vilevile, karakana nne 4 za kuongeza mifumo ya matumizi ya nishati ya gesi kwenye magari zimejengwa Dar es Salaam (3) na Mtwara (1) ambapo hadi sasa zaidi ya magari 750 yamewekewa mfumo wa matumizi ya nishati ya Gesi asilia.

Ndani ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania bara, nchi imeanza kuchukua hatua mbalimbali ili kutekeleza miradi kielelezo katika Sekta ya Mafuta na Gesi ambayo kukamilika kwake kutazidi kupaisha uchumi, na mfano wa miradi hiyo ni Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia (LNG) ambao unalenga kuchakata na kusindika gesi asilia iliyogunduliwa katika Vitalu namba 1, 2 na 4 katika hali ya kimiminika ili iweze kutumika kwa matumizi ya ndani na kuuzwa nje ya nchi.

Miradi mingine ya vielelezo ni pamoja na Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania (EACOP), mradi wa Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia wa Mnazi Bay, unaolenga kufanya utafutaji wa Mafuta na Gesi asilia katika kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini kilichopo Bahari ya kina cha kati kusini mwa Tanzania na Mradi wa Eyasi-Wembere unaolenga kufanya utafutaji wa mafuta katika kitalu cha Eyasi – Wembere, Kaskazini Mashariki mwa Tanzania kwenye Bonde la Ufa.



Kivukoni, Dar es salaam 2019

# Sekta ya Uvuvi Yainua Wananchi Kiuchumi

Sekta ya Uvuvi ni moja ya sekta tatu zinazoajiri wananchi wengi wa kipato cha chini ikiongozwa na sekta za kilimo na mifugo. Sekta hii inachangia upatikanaji wa chakula na lishe kwa asilimia 30, ajira za moja kwa moja za wavuvi 195,435 na zaidi ya wananchi milioni 4.5 na inachangia pato la taifa kwa asilimia 1.7.





Kabla ya uhuru kati ya mwaka 1960 hadi 1961 Sekta ya Uvuvi ilikuwa chini ya Wizara ya Maliasili na Maendeleo ya Ushirika. Baada ya kupata uhuru mwaka 1961 usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi ulifanyika chini ya Sheria ya "Fisheries Ordinance and Trout Protection Ordinance CAP 368" kupitia Wizara ya Kilimo, Misitu na Wanyamapori. Mwaka 1971 Idara ya Uvuvi ilihamishiwa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mnamo mwaka 1985 Sekta ya Uvuvi ilihamishiwa Wizara ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Mwaka 1997 Wizara ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ilivunjwa ambapo Wizara ya Maliasili na Utalii ilirejeshwa na Idara ya Uvuvi ilikuwa chini yake. Februari mwaka 2008 Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi iliundwa ambapo sekta ya uvuvi ilipanua majukumu yake na kukasimiwa kwenye Idara mbili ambazo ni Idara ya Maendeleo ya Uvuvi na Idara ya Ukuzaji Viumbe Maji.

Pamoja na mabadiliko yote hayo katika Wizara, sekta ya uvuvi imekuwa ikiendelea kusimamia jukumu lake la msingi ambalo ni kuhakikisha rasilimali za uvuvi zinalindwa, zinahifadhiwa, zinaendelezwa na zinatumiwa kwa njia endelevu kwa faida ya kizazi kilichopo na vizazi vijavyo.

Tangu uhuru mpaka sasa, sekta ya uvuvi imekuwa ikifanya mapitio na mabadiliko ya sheria, kanuni na miongozo kulingana na uhitaji, mfano wa mabadiliko ya miaka ya hivi karibuni ni Sheria ya Taasisi ya Utafiti Tanzania Na. 6 ya mwaka 2016, Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu Na. 5 ya mwaka 2020 na Kanuni zake za mwaka 2020.

## UVUNAJI WA RASILIMALI ZA UVUVI KIBIASHARA

Shughuli za uvuvi katika kipindi cha mwaka 1961-1988 katika maeneo yote ya uvuvi nchini zilikuwa zikifanywa na wavuvi wadogo ambapo kiasi cha samaki kilichozalishwa kutoka kwenye maji ya asili kimeonekana kuongezeka kutoka tani 385,771.80 zenye thamani ya shilingi bilioni 7.73 mwaka 1986 hadi tani 473,593.24 zenye thamani ya shilingi trilioni 2.36 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 18.54.

## USIMAMIZI WA UBORA, USALAMA, VIWANGO VYA SAMAKI NA MAZAO YA UVUVI

Tangu kupatikana kwa uhuru, Serikali imeendeleza jitihada za kudhibiti ubora, usalama wa samaki na mazao ya uvuvi ili kulinda soko la ndani na nje ya nchi ambapo mwaka 1997 ilianzishwa Maabara ya Taifa ya Uvuvi ya Nyegezi. Kufuatia jitihada hizo mazao ya uvuvi yanayouzwa nje ya nchi yameendelea kuongezeka kutoka tani 17,269.90 na samaki wa mapambo 4,477.97 zenye thamani ya shilingi bilioni 11.93 mwaka 1995 hadi tani 40,477.97 na samaki wa mapambo 128,316 zenye thamani ya shilingi 386.37 mwaka 2020. Mauzo hayo ya mwaka 1995 yaliliingizia Taifa shilingi milioni 629.57 ikilinganishwa na shilingi bilioni 21.67 za mwaka 2020 kama mrabaha.

## KUHAMASISHA UWEKEZAJI KWENYE SEKTA YA UVUVI

Suala la uhamasishaji limekuwa likifanyika katika vipindi tofauti kwa kutumia mbinu mbalimbali katika miaka hii 60 ya uhuru. Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji katika sekta ya uvuvi kwa kuanzisha Dawati la Sekta Binafsi Wizarani kwa ajili ya kutoa elimu na kuwaunganisha wadau wa uvuvi na taasisi za kifedha ili kuwawezesha kupata mikopo yenye masharti nafuu. Mazingira hayo yamehamasisha ongezeko la viwanda mathalani mwaka 1992 kulikuwa na viwanda 4 vilivyokuwa na uwezo wa kuzalisha tani 3 kwa siku lakini mwaka 2021 vipo viwanda 15 vyenye uwezo wa kuzalisha tani 40 – 60 kwa siku.

## UJENZI WA BANDARI YA UVUVI

Mojawapo ya mafanikio makubwa ya sekta hii ndani ya miaka 60 ni ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ambapo kwa sasa Wizara inaendelea kufanya upembuzi yakinifu kupitia Mtaalam Mwelekezi ambaye ni Kampuni ya M/S Sering Ingegneria ya nchini Italia kwa gharama ya shilingi 1,421,041,703.08. Serikali tayari imechagua eneo la bandari ya Kilwa Masoko kwa ajili ya kujenga bandari ya uvuvi na tayari katika bajeti ya mwaka 2021/2022 imetenga shilingi bilioni 50 kwa ajili ya kuanza ujenzi mara baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu.

## SHIRIKA LA UVUVI TANZANIA

Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) lilianzishwa kupitia Tamko la Rais la mwaka 1974 chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma Na. 17 ya mwaka 1969. Mwaka 1996 TAFICO iliwekwa kwenye orodha ya mashirika ya umma yaliyotakiwa kubinafsishwa. Serikali inakamilisha taratibu za kulifufua shirika hilo ili liweze kufanya majukumu yake ya kusimamia sekta ya uvuvi kibiashara ambapo Serikali itanunua meli tano (5) za uvuvi wa bahari kuu ambapo meli moja itapatikana kupitia msaada wa Serikali ya Japan na meli nne (4) kupitia mradi wa IFAD.

## UENDELEZAJI WA UKUZAJI VIUMBE MAJI

Shughuli za ukuzaji viumbe maji ni ngeni hapa nchini, kutokana na mafanikio ya sekta ya hiyo yaliyopatikana baada ya uhuru, shughuli hiyo sasa imerasimishwa. Ukuzaji viumbe maji unajumuisha ufugaji wa samaki, kambamiti, chaza, kaa, majongoo bahari na kilimo cha mwani. Kuanzia mwaka 2008 Serikali iliongeza vituo vya kuendeleza ukuzaji viumbe maji kutoka kimoja cha Kingolwira - Morogoro hadi vitano vya Mwamapuli – Tabora, Ruhila – Ruvuma, Nyengedi/Mtama – Lindi na Machui – Tanga.

Idadi ya vifaranga kwenye vituo vya Serikali imeongezeka kutoka 5,000 mwaka 1992 hadi 3.191,160 mwaka 2021 wakati idadi ya vitotoleshi kwa Sekta Binafsi na Umma vyenye uwezo wa kuzalisha zaidi ya vifaranga 25,000,000 vimefikia 28, aidha kuna jumla ya viwanda 11 vya chakula cha samaki ambavyo vina uwezo wa kuzalisha tani 1,000.

Kati ya mwaka 2014/2015 na 2020/2021 idadi ya vizimba vimeongezeka katika Maziwa Makuu na malambo kutoka 50 hadi 473. Pia kuwepo kwa Mifumo ya Ukuzaji Viumbe Maji Inayorejeleza Maji imepelekea kuongezeka kwa uzalishaji ambapo idadi ya mabwawa imeongezeka kutoka 8,611 yaliyozalisha tani 1,350 mwaka 1992 hadi mabwawa 30,034 yaliyozalisha tani 22,793.2 mwaka 2020/2021.

> **Mwaka 1961-1988 shughuli za uvuvi katika maeneo yote ya uvuvi nchini zilikuwa zikifanywa na wavuvi wadogo.**




Hospitali ya Taifa ya Muhimbili-Mloganzila

# Huduma Bora za Afya Zawafikia Wananchi

Na **Beatrice Lyimo**

Watanzania wanajivunia mafanikio ya sekta ya afya ndani ya miaka 60 tangu Uhuru wa iliyokuwa Tanganyika uliopatikana Tarehe 9 Desemba, 1961 na kutangazwa kuwa Jamhuri kamili tarehe 9 Desemba, 1962 chini ya Rais wa Kwanza na Amiri Jeshi Mkuu, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Baada ya Uhuru wa Tanganyika, viongozi waliweka mazingira mazuri ya kujenga misingi mikuu ya utaifa ambayo ni utambulisho wake miongoni mwa mataifa .Misingi hiyo ni pamoja na umoja, utu, uhuru, maendeleo, usawa, haki, kujitegemea, utaifa na uzalendo, amani na maadili.

Kwa msingi huo, watu wenye afya bora ndiyo msingi wa maendeleo ya Taifa ikizingatiwa kabla ya uhuru vituo vya huduma za afya nchini vilijengwa na kuendeshwa na Serikali kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Dini na Mamlaka nyingine ambapo kila moja ya mamlaka hizo ilijenga vituo vya huduma za afya kwa madhumuni na shabaha zake yenyewe bila kujali uwiano na mipango ya Mamlaka nyingine.

Kutokana na utaratibu huo ambao haukuwa na uwiano mzuri, ulifanya baadhi ya maeneo ya nchi kuwa na Vituo vya huduma za afya huku mengine yakikosa huduma hiyo muhimu.

Baada ya uhuru, Serikali ilichukua hatua kadhaa za kurekebisha hali hiyo kwa kuanzisha mipango ya kusambaza vituo vya huduma za afya kwa usawa na uwiano wa haki kwa wananchi wote.

Ni miaka 60 sasa imetimia tangu nchi hii ipate uhuru na kumekuwa na mafanikio makubwa katika kuboresha huduma za afya kutokana na jitihada zilizofanywa na Serikali zote kuanzia Awamu ya Kwanza iliyoongozwa na Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na hata sasa Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Wakati nchi inapata Uhuru kulikuwa na idadi ya hospitali na zahanati 1,343, uwiano wa wagonjwa kwa kitanda ulikuwa 1:1000, Madaktari waliosajiliwa 403 na uwiano wa Vituo vya Afya kulingana na idadi ya watu ulikuwa ni Kituo kimoja cha Afya kinahudumia watu kati ya 40,000 hadi 50,000.

Lakini baada ya jitihada kubwa ya Serikali ya Awamu zote Sita, idadi ya hospitali na zahanati kwa pamoja ni 8,537, jumla ya Madaktari waliosajiliwa ni 71,365 na uwiano wa vituo vya afya kwa idadi ya watu ni kituo kimoja cha afya kinahudumia watu 6,751. Aidha, kuna kuna Hospitali moja ya Taifa, Hospitali sita za matibabu Kibingwa ngazi ya Kanda, Hospitali tano za ubingwa maalumu, Hospitali 28 za Kibingwa Ngazi ya Mikoa na Hospitali za Wilaya 178.

Kutokana na hatua hii kubwa iliyopigwa ya kupambana na adui mkubwa maradhi, baadhi ya wananchi kutoka maeneo mbalimbali nchini wametoa maoni yao kuhusu Sekta ya Afya kuanzia wakati wa uhuru wa Tanganyika mpaka sasa nchi inapoadhimisha miaka 60 ya uhuru.

"Nashukuru Awamu zote za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zao za kusogeza huduma za afya kwa wanaNchi, kwani kabla ya Uhuru huduma nyingi za jamii ikiwemo huduma za afya zilikuwa zikitolewa mijini. Hospitali zote kubwa zilikuwa mijini isipokuwa hospitali chache zikiwemo za Mashirika ya Dini ambazo zilikuwa vijijini," anaeleza Bi. Aisha Maulid (76), ambaye wakati huo alikuwa anaishi Manolo-Lushoto mkoani Tanga lakini kwa sasa anaishi Makole jijini Dodoma.

Bi. Aisha anafafanua kuwa "Namshukuru sana Mungu kwa kuweza kushuhudia baadhi ya mambo ambayo tangu nizaliwe sikuwahi kujua kama ningeyaona kwani kwa sasa huduma za afya zinapatikana hadi kijijini kwetu wakati zamani huduma za afya za kawaida kabisa tulikuwa tunazifuata mbali sana hadi kusababisha vifo hasa kwa wale wagonjwa waliozidiwa sana"

Kwa upande wake Bi. Lucy Temu (71) wa Kayenze Mwanza anaeleza kuwa, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika huduma za afya zenye ubora na zinazowafikia wananchi wote ili kuboresha afya zao.

"Tangu nimekuwa nimeona mabadiliko katika sekta ya afya, nakumbuka kabla ya uhuru nikiwa kijijini kwetu Kayenze Mkoani Mwanza. Nilikuwa mdogo lakini nilishuhudia wazazi wangu na watu wa pale kijijini wakihangaika sana kupata huduma za afya kwani zilikuwa mbali na maeneo tunayoishi, hivyo ilitupasa kusafiri zaidi ya saa moja kufuata huduma za afya, ilichosaidia sisi tumekuwa kwenye mazingira ya kidini ila wengi walikimbilia kwa waganga wa kienyeji ili kuweza kutibu Magonjwa yaliyowakabili.

Kwa sasa sio kama zamani kwani ukiumwa unatibiwa kwa kuwa huduma za hospitali zinapatikana kwa karibu, maduka ya madawa yaliyoruhusiwa na Serikali yanapatikana kwa wingi ikilinganishwa na zamani," anaeleza Bi. Temu na kuongeza kuwa Serikali inatambua umuhimu wa afya bora kwa wananchi wake kwani afya bora ni raslimali muhimu kwa maendeleo hivyo kwa sasa huduma za afya katika kijiji chake zimeimarika.

Kwa upande wake Bw. Athumani Ally wa kijiji cha Mloka Wilaya ya Rufiji anaeleza kuwa maendeleo yeyote katika Taifa huletwa na wananchi wenye afya njema na kusisitiza kuwa katika kipindi cha miaka 60, Tanzania imefanya mabadiliko na mafanikio katika sekta ya afya. "Nimezaliwa mwaka 1965, miaka minne baada ya uhuru lakini nimeweza kushuhudia baadhi ya mabadiliko na mafanikio katika sekta ya afya ndani ya Wilaya yetu ya Rufiji," anasisitiza Bw. Athumani.

Fausta Pius (64) ni mzaliwa wa Heru Juu Wilaya ya Kasulu, Mkoa wa Kigoma, anazungumza mafanikio ya miaka 60 ya uhuru kwenye sekta ya afya na kusema kuwa Serikali kupitia sekta hiyo imeweza kutoa elimu kwa umma juu ya kujikinga na maradhi mbalimbali yasioambukiza.

"Nimeona Serikali kupitia sekta ya afya imeweza kuelimisha wananchi kuhusu maradhi yanayoweza kuzuilika ili wananchi wenyewe waweze kutambua maradhi hayo na kutafuta mbinu za kuyatokomeza wao wenyewe," anaeleza Bi. Fausta.




SIEMENS




MAGNETOM Spectra
SIEMENS



Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dodoma

# Miaka 60 ya Uhuru: Maendeleo ya Teknolojia Sekta ya Afya Yapunguza Safari za Matibabu Nje ya Nchi

Na **Ahmed Sagaff - MAELEZO**

Afya ni neema, mtu mwenye afya njema huwa na nguvu ya kujitafutia riziki ya halali na kutimiza wajibu wa kiroho. Kwa kulifahamu hilo, mara baada ya Tanzania Bara kupata Uhuru wake mnamo 1961, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliunda Wizara inayosimamia sekta ya afya ili kupambana na adui maradhi.

Mapambano ya kujikinga na kudhibiti maradhi yameendelea chini ya viongozi wote walioiongoza Seriakali hadi kufikia leo ambapo tunasherehekea miaka 60 ya uhuru wetu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, mafanikio yaliyopatikana kwenye Sekta ya Afya ndani ya miaka 60 ya Uhuru ni makubwa sana ukilinganisha na yale yaliyokuwepo zaidi ya miaka 70 (1889-1961) ya utawala wa kikoloni.

Kabla ya Uhuru, idadi ya hospitali na zahanati kwa pamoja ilikuwa 1,343 ambapo uwiano wa vituo vya afya kwa idadi ya watu ilikuwa ni kituo cha afya kimoja kwa watu 40,000 au 50,000.

"Aina ya watumishi kwenye vituo hivyo ilikuwa mganga msaidizi mmoja, mkaguzi wa afya mmoja, wakunga kijijini wawili, wauguzi wawili, mhudumu wa afya mmoja, na watumishi wa kawaida wawili," inaeleza taarifa hiyo.

**Wataalam wa Maendeleo ya Jamii katika miaka ya 1960 hadi 1980 walikuwa chachu ya kutekeleza kampeni mbali mbali za kitaifa zinazohitaji ushiriki wa jamii ikiwemo Uhuru na Kazi; Siasa ni Kilimo; Kisomo Chenye Manufaa; Azimio la Arusha; Mtu ni Afya; Elimu kwa Wote; Chanjo ya Watoto wenye Umri Chini ya Miaka Mitano; Uhai, Ulinzi na Maendeleo ya Mtoto.**

Idadi ya vitanda vya kulazia wagonjwa ilikuwa vitanda 18,832 tu, kwa hospitali kubwa 12 zilizokuwepo wakati huo zilikuwa na vitanda 3,046 huku uwiano wa vitanda kwa idadi ya watu ni kitanda kimoja kwa watu 1000. Kati ya hospitali kubwa zilizokuwepo, saba zilikuwa zikimilikiwa na Serikali, nne za mashirika ya kidini na hospitali moja ilikuwa ya mtu binafsi.

Hadi mwaka 1961, jumla ya Madaktari waliosajiliwa na waliokuwa na leseni na kufanya kazi walikuwa 403 tu huku jitihada za kuongeza watumishi mpaka kufikia idadi hiyo zikifanyika katika kipindi cha miaka mitano ya mwisho ya utawala wa Muingereza.

"Madaktari 182 walikuwa katika vituo binafsi, 140 serikalini, na 81 waliajiriwa na mashirika ya afya ya kujitolea," taarifa hiyo inaarifu.

Kliniki za mama wajawazito zilikuwa 412, huku serikali kuu ikimiliki kliniki 71 tu. Jumla ya wajawazito 177,214 ndio waliopatiwa huduma kwenye kliniki hizo huku wakunga asilia wakihudumia idadi kubwa.

Pamoja na hayo, kulikuwa na kliniki za watoto zipatazo 454 zilizoweza kutoa huduma za kliniki kwa watoto 136,504 tu.

Aidha, watu walitumia gharama kubwa na siku nyingi kufuata huduma za afya zisizokuwa na ubora zilizokuwa zikitolewa bila malipo kutokana na changamoto za kukosekana dawa.

Miaka 60 baada ya uhuru, Tanzania imeandika historia ulimwenguni kwa kufikia malengo ya Umoja wa Mataifa katika upatikanaji wa huduma za afya kwa kuzingatia idadi ya watu na jiografia.

Sambamba na hili, umri wa kuishi wa Mtanzania umeongezeka kutoka miaka 36 mwaka 1961 hadi miaka 66 mwaka 2020.

Idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya vimeongezeka kutoka vituo 1,343 kabla ya uhuru mpaka vituo 8,537 ambapo imewezesha kupunguza uwiano kutoka kituo kimoja kuhudumia watu 40,000 mpaka 50,000 hadi kituo kimoja kwa watu 6,751. Serikali inamiliki asilimia 64 ya vituo hivyo.

Aina ya kada za afya zilizopo nchini hivi sasa zinajumuisha Madaktari bingwa, Madaktari wa kawaida, Wauguzi, Wataalamu wa Maabara, Wafamasia na Wataalamu wa Mionzi, na Watumishi wa Umma kwenye kada hii ni 71,365.

Idadi ya vitanda kwa sasa ni 90,488 ikiwa ni sawa na ongezeko la vitanda 71,656 sawa na asilimia 79.18 huku uwiano wa vitanda ukiwa ni kitanda kimoja kwa watu 19.

Hospitali za kibingwa Ngazi ya Mkoa ni 28, Ngazi ya Kanda ni sita, hospitali za ubingwa maalum tano na hospitali ya taifa ni moja. Aidha, kuna Hospitali za Wilaya 178, hospitali nyingine 151, vituo vya afya 926 na zahanati 7,242.

Huduma bobezi zinazotolewa nchini zimekuwa zikiwavutia watu wa mataifa jirani ambao huhiminika nchini kufuata matibabu ya maradhi mbalimbali.


Sera nzuri inayotaka kila kituo cha kutolea huduma za afya kiwe na kliniki za mama na watoto imeifanya Tanzania Bara kuwa na kliniki nyingi. Jambo hili limepunguza vifo vya wajawazito na watoto wachanga.

Mafanikio mengine yaliyopatikana ni kuanzishwa kwa Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF), Bohari Kuu ya Dawa (MSD), Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) na Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC).

Vilevile, uwepo wa sera nzuri umewezesha kuwepo kwa makampuni ya dawa nchini kama vile Keko Pharmaceutical Limited, Pyramid Pharma Limited, Kairuki Pharmaceuticals Industry Limited na Salama Pharmaceuticals Limited.


Aidha, Serikali inaendelea kuwekeza kwenye ubora wa huduma, kuimarisha mifumo ya TEHAMA, kusambaza bima ya afya kwa wote, kuvutia wawekezaji sekta ya afya, kupanua huduma za kibingwa, kuongeza uwekezaji kwenye tafiti na kujikita kwenye afya kinga dhidi ya magonjwa yanayoepukika.
























Barabara ya Mbeya - Lwanjiro - Chunya (km 72)

# Kuimarika kwa Miundombinu Kwachochea Ukuaji wa Uchumi

**Na Mwandishi Wetu, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi**

Tanzania Bara inapoadhimisha miaka 60 ya Uhuru kutoka kwa Wakoloni wa Kiingereza, ni muda muafaka wa kupitia na kutafakari tulipotoka, tulipo na tunapoelekea, hususan katika suala zima la miundombinu ya usafirishaji.
Kwa kipindi chote hicho, njia kuu za usafirishaji zinazotumika nchini ni barabara, reli, ndege na vyombo vya majini, ambapo usafiri kwa njia ya barabara ndio njia kuu inayotumika nchini ikikadiriwa kusafirisha zaidi ya asilimia 90 ya mizigo na abiria.
Kutokana na ukubwa wa nchi hii inayokadiriwa kuwa na kilometa za mraba 945,203, mtandao wa barabara umekuwa ukiboreshwa na kuongezeka mwaka hadi mwaka ili kukidhi mahitaji ya ongezeko la watu.

## BARABARA NA MADARAJA

Kwa sasa mtandao huo una jumla ya kilometa 180,687.77 (kilometa 36,258 zinasimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania TANROADS na kilometa 144,429.77 zinasimamiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) ikilinganishwa na kilometa 33,600 mwaka 1961.
Mtandao wa barabara unaosimamiwa na Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), ambapo ujenzi kwa kiwango cha lami umekamilika kwa kilometa 11,186 na kilometa 25,176 zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi.
Ujenzi wa barabara unaenda sambamba na kuhakikisha kuwa ukarabati wa barabara hizo unafanyika mara kwa mara, hii ikiwa ni pamoja na barabara ambazo bado hazijakamilika kwa kiwango cha lami zinakuwa katika hali nzuri.

Aidha, ujenzi wa madaraja kwenye barabara hizo unaendelea ili kuweza kuunganisha mawasiliano kutoka sehemu moja hadi nyingine na kuzifanya barabara hizo ziweze kupitika kwenye majira yote ya mwaka.

Katika miaka ya hivi karibuni imeshuhudiwa kukamilika kwa madaraja makubwa 12 hapa nchini ambapo ni daraja la Magufuli (Kilombero), Nyerere (Kigamboni -Dar es Salaam), Kavuu (Katavi), Sibiti (Singida), Lukuledi II (Lindi), Ruvu Chini (Pwani), Magara (Manyara), Momba (Rukwa), Mlalakuwa (Dar es Salaam), Mara (Mara), Kitengule (Kagera), na Ruhuhu (Ruvuma).

Taarifa kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi inaeleza kuwa ujenzi wa madaraja makubwa sita (6) ambayo ni Kigongo – Busisi (JPM), daraja Jipya la Selander (Tanzanite -Dar es Salaam), Wami (Pwani), Msingi (Singida) na Gerezani (Dar es Salaam) unaendelea na uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea kufuata nyayo za Serikali zilizotangulia katika kuboresha miundombinu ikiongozwa na Kauli Mbiu yake ya 'Kazi Iendelee'. Akihutubia Bunge la 12 tarehe 22 Aprili 2021, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan alisisitiza nia ya Serikali katika kuimarisha miundombinu ya usafiri, ambayo ni moyo wa ukuaji wa sekta za kiuchumi na kijamii.

Ili kuyaunganisha maeneo yenye mito mikubwa, maziwa na maeneo ya nchi kavu, Serikali imeendelea kuboresha vivuko katika maeneo hayo ili kurahisisha huduma za usafirishaji wa watu na mizigo.

Wakati Tanzania Bara inapata Uhuru mwaka 1961 kulikuwa na vivuko vitano visivyo vya kisasa vilivyokuwa vinavutwa kwa kamba. Miaka 60 baadaye nchi yetu imefanikiwa kuwa na vivuko 33 vya kisasa vinavyotoa huduma katika vituo 22 nchini kote pamoja na uwepo wa boti kubwa sita na ndogo tano katika maeneo ya mito.

## SEKTA YA ANGA

Serikali pia inaendelea kuimarisha usafiri wa anga ambapo ujenzi wa viwanja vya Ndege vyenye lengo la kurahisisha huduma za usafiri na usafirishaji vimeendelea kujengwa na kukarabatiwa katika mikoa mbalimbali nchini.
Viwanja hivyo ni pamoja na Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere (JNIA – TB III) ambapo jengo la kisasa la abiria limejengwa, Viwanja vya Ndege vya Mwanza, Tabora, Kigoma na Bukoba ambavyo uboreshaji wake umekamilika.

Kazi nyingine zinazoendelea kutekelezwa ni ukarabati wa Viwanja vya Ndege vya Mtwara, Iringa, Geita, Songea na Kiwanja cha Musoma ambapo ukarabati upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Aidha, Mkataba wa ujenzi wa mradi mpya wa Kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Msalato Awamu ya Kwanza (package 1) unaohusisha ujenzi wa miundombinu ya Kiwanja (Airport Infrastructure); umesainiwa tarehe 13 Septemba, 2021 kwa gharama ya zaidi ya Shilingi Bilioni 165.62 ambapo utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu (3).

Aidha, Maandalizi ya ukarabati na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Moshi, Sumbawanga, Tabora (Awamu ya 3) Kigoma (Awamu ya pili), Shinyanga, Mwanza (Jengo jipya la abiria) na Arusha yanaendelea.

Serikali pia inaendelea na mipango ya kuanza ujenzi wa viwanja vya ndege vya Lindi, Lake Manyara, Tanga na Simiyu.

Jitihada kubwa zimefanywa na Serikali ndani ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara katika kuhakikisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji inafunguliwa na kuwafikia wananchi ikiwa ni kichocheo cha maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini.

Uwekezaji katika miundombinu hii ni mkubwa, hivyo kila mmoja wetu asimame katika nafasi yake kuhakikisha kuwa miundombinu inalindwa ili idumu kwa ajili ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.



Jiji la Dar es Salaam
Picha na Osse Greca Sinare

# Simulizi Nzito ya Kushushwa kwa Bendera ya Muingereza na Kupandishwa Bendera ya Tanganyika- Asimulia Hamza Kasongo

**"Watu walikumbatiana. Nje ya Uwanja madebe na makopo yaligongwa, magari yaligonga honi na meli zilizokuwa bandarini zilipiga honi. Mizinga 21 ilipigwa....**

Jumamosi, tarehe 9 Desemba, 1961 ni siku ya kihistoria ambayo itabaki katika hisia kwenye mioyo ya watu wengi wa Karne ile na wale wa Karne hii wataitambua kama siku ya tukio muhimu katika Maisha yao. Kwangu binafsi inabaki kuwa muhimu zaidi kwa sababu nilibahatika kufanya kitendo ambacho hakitajirudia tena. Ilipotimia saa sita usiku kamili niliutangazia umma uliojaa kwenye uwanja uliojengwa mahsusi kwa sherehe za Uhuru. Halikadhalika matangazo hayo yalisikika nchi nzima katika sehemu zilizowekwa maalumu. Niliwaambia wasikilizaji wetu jinsi Bendera ya Kiingereza ilivyokuwa inashushwa na kupandishwa kwa Bendera ya Taifa Jipya la Tanganyika.

Hii ilikuwa ni kilele cha safari ndefu ilioanza miaka mingi ya kutafuta Uhuru, ambao, mwaka huu, 2021, Tanganyika, sasa Tanzania inatimiza miaka 60 ya kujitawala. Jinsi tulivyofika hapa nitawaachia wana historia ambao wataieleza safari hiyo kwa marefu na mapana na kwa usahihi kabisa. Mimi jukumu langu ni kuelezea vile ambavyo sherehe za Uhuru zilivyokwenda kwa kupitia matangazo ya redio.

Ninakumbuka kulikuwa na makundi matano yaliyoshiriki sana katika matayarisho ya sherehe ya siku ya Uhuru. Kwanza kulikua na Vikosi vya Majeshi ya Ulinzi na Usalama pamoja na vijana wa halaiki na sarakasi. Baadhi yao walikwenda kuchukua mafunzo maalumu China. Pili, Vikundi vya utamaduni ambavyo viliwakilisha karibu makabila yote makubwa ya Tanganyika. Tatu ni Serikali yenyewe na Itifaki ya wageni kuratibu mpangilio wa sherehe zote. Nne lilikuwa kundi la Luteni Alex Gwebe-Nyirenda lililotakiwa kupanda Mlima Kilimanjaro. Kundi la tano lilikuwa ni sisi watangazaji wa redio. Kama vile kundi la wanajeshi na usalama na Serikali yenyewe walivyopata wataalamu wakuwaongoza. TBC Asili pia hatukuachwa nyuma tulipata wataalamu waliopata uzoefu kutoka Ghana (Gold Coast), 1957 na Nigeria, 1960.

Nimeongeza neno asili ili kuonyesha TBC ile haikuwa Idara ya Serikali kama ilivyo sasa. Sisi tulikuwa tunaongozwa na Baraza la Magavana. Ingawa Gavana ndio alikuwa anawateua lakini Serikali ilikaa kando kutuacha tufanye kazi yetu bila ushawishi wowote.

**HIVYO NDIYO ILIVYOKUWA TAREHE 9 DESEMBA, I961 NINAVYO IKUMBUKA.**

Kwa upande wa TBC wataalam wetu kutoka BBC, London walifika karibu miezi minne kabla ili tupange mipango. Walianzisha kitengo maalumu kilichoitwa MATAYARISHO YA VIPINDI VYA UHURU. Na wakajengewa studio maalumu, STUDIO FOUR. Kutoka watangazaji wa TBC nilichaguliwa mimi peke yangu nikasaidiane nao. Jambo la kwanza walilotaka nifanye ni kuzunguka nchi nzima kuwauliza wenye makampuni na viwanda vikubwa, halikadhalika wenye mashamba makubwa kama watakuwa tayari kubaki na kuendelea kufanya kazi chini ya Serikali ya Mwalimu Nyerere . Baada ya Dar es Salaam nilikwenda Morogoro, Kilosa, Kimamba kuwauliza wahusika swali hilo hilo. Wakulima wa hapa walikuwa wanalima Mkonde.

Kisha nikasafiri kwenda Iringa na kukaa White Horse Inn. Huu ulikuwa ni mpango mkakati kwa sababu kila jioni wakulima karibu wote, wengi wao ni wa Asili ya Ugiriki, walikuwa wanakuja pale.

Zao lao kuu lilikuwa Tumbaku. Niliwapata wengi kwa pamoja. Kazi yangu ikawa rahisi. Kutoka Iringa nikaenda Arusha kwenye mashamba mchanganyiko. Hatimaye nikawasili Tanga. Kila mwaka wakulima wa kila zao, hususan Wagiriki hukutana katika Hoteli ya Lady Grid na kufanya mkutano wa mwaka. Mgeni Rasmi mara nyingi huwa Gavana. Katika Mkutano huu wa mwaka 1961, Sir Richard Turnbul, Gavana wa mwisho wa Tanganyika alihudhuria kwa madhumuni matatu. Kwanza kama ilivyo kawaida, pili kuwaaga na tatu kuwauliza na kuwaomba washirikiane na Serikali mpya. Kwa sauti moja kubwa wote wakakubali kubaki.

Zilipobaki siku kama sita kabla ya kilele, mazoezi ya Sherehe yakapamba moto. Ikabidi Mtangazaji mwenzangu Salim Seiff Nkamba na mimi twende kila siku kwenye Uwanja wa Uhuru kuona jinsi mazoezi yanavyoendelea ili siku ya siku tuwe timamu.

Tarehe 8 Desemba, 1961, Salim Seiff Nkamba, maarufu kama S.S au Mjomba pamoja na mimi na mafundi wetu wakiongozwa na Anthony Demello na Eliuter Nderimo tuliwasili Uwanja wa Uhuru kiasi cha saa mbili usiku. Tukashangaa kuona Uwanja umejaa na watu wengine wanasubiri kuingia. Baada ya viongozi kuingia shughuli zikaanza. Kwenye gwaride, Jeshi hilo hilo moja la Kiingereza, KAR {Kings African Riffles} lilijigawa mara mbili. Moja likabaki kama KAR na lingine likawa Jeshi la Taifa jipya, TANGANYIKA RIFFLES.

Baada ya kubadilishana bendera nikazungumza na Luteni Nyirenda ambaye wakati ule tayari alikuwa kwenye kilele cha Mlima Kilimanjaro. Nikamuuliza jinsi msafara wao ulivyokuwa. Kuhusu mawasiliano kutoka Uwanjani matangazo yetu yalikwenda Studio Pugu Road. Kutoka hapo yakapelekwa Posta, Carrier Room. Nao wakayapeleka Moshi Carrier Room na baada ya hapo Kikosi cha Masiliano ya Jeshi la KAR kilichotoka Nairobi kikachukuwa jukumu. Akijibu swali langu, Lt. Alex Gwebe-Nyirenda alisema nimetumwa na Waziri Mkuu Julius Kambarage Nyerere kuja kuwasha mwenge na kutangaza: **SISI WATU WA TANGANYIKA TUNAWASHA MWENGE NA KUUWEKA KWENYE KILELE CHA MLIMA KILIMANJARO, ILI UMULIKE NJE YA MIPAKA YA NCHI YETU, ILETE MATUMAINI AMBAKO WATU WAMEKATA TAMAA, UPENDO PALE KWENYE CHUKI NA HESHIMA KWENYE UDHALILISHAJI.**











Sekta ya Kilimo

# Miaka 60 ya Uhuru: Kilimo Chaongeza Lishe na Kupunguza Utapiamlo

**Kilimo ni sayansi, uwekezaji wa kutosha kwenye vituo vya utafiti wa kilimo na matumizi ya kilimo cha umwagiliaji kutakifanya kilimo kifanye mapinduzi makubwa ya kijani nchini kwani ardhi bora tunayo, uongozi bora tunao...**

Na **Dino Mgunda- MAELEZO**

Historia inaonyesha kilimo kimeanza kufanywa na binadamu miaka 105,000 iliyopita. Hii inaonesha kuwa kilimo ni moja ya shughuli kongwe nchini ukiondoa uwindaji na uokotaji matunda.

Kilimo kinafanyika kuanzia pwani ya Bahari ya Hindi mpaka kwenye mialo ya Ziwa Nyasa kwa Nyanda za Juu Kusini fukwe za Ziwa Tanganyika kwa upande wa Magharibi wa nchi na mialo ya Ziwa Nyanza kama linavyojulikana na wenyeji wa Mwanza na Simiyu huku kwenye vitabu likijulikana kama Ziwa Victoria kilimo kinafanyika hata Kilimanjaro.

Kupitia kilimo Watanzania wanajipatia chakula cha kutosha na hivyo kupunguza tatizo la utapiamlo. Kwa ujumla Tanzania imejitosheleza kwa chakula licha ya changamoto ya uhaba wa chakula iliyojitokeza mwaka 1979 baada ya vita ya Kagera.

Wakati Taifa likisheherekea miaka 60 toka limepata uhuru sekta ya kilimo nayo imekua ukianzia zile kauli mbiu za Awamu ya Kwanza kama vile kilimo cha kufa na kupona kilichowataka wakulima kujituma kwa nguvu zao zote lakini haikuishia hapo mwaka 1974 miaka 14 baada ya kupata uhuru akiwa Iringa alitoa wito wa siasa ni kilimo ulio wafanya viongozi wa kisiasa kukihubiri kilimo kwa wananchi wao.

Wapo wakulima wanazikumbuka kauli mbiu zilizoleta mapinduzi katika kilimo, Mzee Hadohado Ntwalane mkulima maarufu wa mahindi na pamba katika Kijiji cha Kifufu Wilaya ya Geita Vijijini anasema, "Naukumbuka wito wa Mwalimu baada ya ukame mkali kulikumba taifa miaka ya 70 ilikuwa mvua ya kwanza ni yakupandia, hii ilitufanya wakulima wafanikiwe kwenye shughuli zao." Kilimo kilipiga hatua kwa kiwango chake kwani katika Awamu ya Kwanza wananchi walishawishiwa kulima mazao yanayohimili ukame kama vile muhogo na mtama na hii ikafanya mazao haya kusambaa nchini kote.

> **Kila awamu kulikuwa na upigaji hatua kwenye kilimo ingawa kuanzia Awamu ya Nne mpaka sasa kumekuwa na ongezeko la wakulima wanaotafuta huduma za ugani kwenye kilimo**

Kwa upande wa Awamu ya Pili kuhusu kilimo, Rais Mwinyi aliachia wakulima kumbukumbu ya soko huria lililochagiza upatikanaji rahisi wa pembejeo za kilimo kwani kiwango cha uagizaji vitendea kazi iliongezeka kama vile majembe ya kukokotwa na ng'ombe plau na matrekta hii ilisababisha kiwango cha mazao kuongezeka na idadi ya wanaofanya kilimo biashara ikaanza kukua, kwani uhuria ulifanya iwe rahisi kuuza mazao ndani na nje ya nchi.

Awamu ya Tatu ilikuja na ubinafsishaji ambao uliongeza idadi ya viwanda binafsi ambavyo viliongeza uhitaji wa mali ghafi za kilimo mfano viwanda vya nguo viwanda vya usindikaji wa matunda na nafaka

Awamu ya Nne nayo ikaja na Kilimo Kwanza huku ikiboresha vituo vya utafiti wa kilimo kama vile uanzishwaji wa Taasisi ya Utafiti ya Kilimo (Mikocheni Agricutural Reseach Instute ) pia katika awamu hii kuliongezeka zana za kilimo hasa Matrekta yaliyokopeshwa kwa wakulima.

Kwa upande wa Awamu ya Tano nao uliongeza juhudi katika sekta ya kilimo mfano uanzishwaji wa mashamba makubwa ya miwa Morogoro na Pwani (Bagamoyo) ambao utaongeza malighafi kwenye viwanda vya sukari.

Katika Awamu ya Tano ndipo kulipoanzishwa kiwanda cha kuunganishia Matrekta ya Urusus kule Kibaha Pwani kulikowapa wakulima fursa ya kumiliki matrekta kwa mikopo na kupunguza matumizi ya jembe la mkono ambayo ni teknolojia ya kizamani.

"Asiyefanya kazi na asile" ulikuwa moja ya misemo ya Hayati John Pombe Magufuli aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, hii iliongeza juhudi kwa mkulima mmoja mmoja.

Ruhusa ya kuuza popote penye soko mazao ya kilimo imeongeza ari kwa wakulima. Mikidadi Mpina mgani mstaafu kutoka mkoani Geita ambaye kwa sasa anajishughulisha na kilimo anasema, " Kila awamu kulikuwa na upigaji hatua kwenye kilimo ingawa kuanzia Awamu ya Nne mpaka sasa kumekuwa na ongezeko la wakulima wanaotafuta huduma za ugani kwenye kilimo" anasema licha ya idadi kuongezeka bado wakulima wengi wanalima kimazoea kunakowafanya walime eneo kubwa huku mavuno yakiwa kiduchu. Mfano kwa mkulima wa pamba wa mazoea kwenye hekari moja anavuna kilo 150 mpaka 250 huyu atalia kila mwaka bei haitoshi na kuna wakati atawekea hata uchafu kwenye pamba ili kuongeza uzito wakati yule anayezingatia kanuni bora za kilimo cha pamba na kupanda mbegu bora za Ukiriguru Mali 2018) ama UKM08 zinavyojulikana ana uhakika wa kuvuna kilo 750 mpaka 1200 kwa hekari hata kama atauza kwa bei ya soko atatengeneza faida kubwa.


Kilimo ni sayansi, uwekezaji wa kutosha kwenye vituo vya utafiti wa kilimo na matumizi ya kilimo cha umwagiliaji kutakifanya kilimo kifanye mapinduzi makubwa ya kijani nchini kwani ardhi bora tunayo, uongozi bora tunao bila shaka awamu hii ya sita kutakuwa na mapinduzi makubwa kwenye kilimo. Rais Samia katika hotuba zake amekuwa akisisitiza kufanyika kwa kilimo chenye tija na cha kisasa.

Akihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jijini Dodoma Aprili, 2021 alisema kuhusu kilimo, "Na nyinyi mambo ni mengi pia kayaangalieni huko, nafurahi kwamba sasa pembejeo na nini kelele zimepungua lakini kuna mambo hayo ya nzige, jinsi ya kucontrol na tumeambiwa yapoyapo kwa sana hapo jirani kwa hivyo na kwetu yatakuwa yapoyapo kwa sana. Mkulima akiweka nguvu yake ardhini anategema avune na ndio maisha yake."

Rais Samia aliongeza, "Kwa hiyo tuhakikiashe wakulima wetu hawapati shida hiyo pamoja na mazongezonge yenu mengine Vyama vya Ushirika na Waziri Mkuu nadhani ndio kajitwika hilo kapu kichwani kwake atakuwa nanyi katika suala la Vyama vya Ushirika. Tusinyonye nguvu za wakulima, mkulima apate haki yake kama anavyoingiza nguvu zake."

**Naukumbuka wito wa Mwalimu baada ya ukame mkali kulikumba taifa miaka ya 70 ilikuwa mvua ya kwanza ni yakupandia, hii ilitufanya wakulima wafanikiwe kwenye shughuli zao.**






# Kutoka Wanafunzi 14 wa Elimu ya Juu Mwaka 1961 Hadi 206,302 Mwaka 2021

Na **Oliva Kato- Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

Wakati nchi inaadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara (Tanganyika) tumeona mabadiliko mengi chanya katika maeneo mbalimbali yenye lengo la kuboresha maisha ya Mtanzania.

Sekta ya Elimu ni moja ya eneo ambalo tumeshuhudia mabadiliko makubwa ikiwa ni juhudi za kumkomboa Mtanzania kutoka katika ujinga wa kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu, kumuongezea ujuzi na maarifa, kuongeza fursa ya upatikanaji wa elimu.

Mabadiliko hayo pia yanaonekana katika mazingira ya kujifunzia na kufundishia ambapo serikali imekarabati, imejenga na kununua vifaa vya kutosha vinavyoendana na mabadiliko ya teknolojia na kuboresha maslahi ya kazi na taaluma ya ualimu, usimamizi wa elimu na mageuzi makubwa katika sayansi, teknolojia na ubunifu na usimamizi wa elimu ya Elimumsingi.

Jitihada hizi za kuendeleza Sekta ya Elimu nchini zimeleta sifa ambazo zimevuka mipaka ya nchi. Tanzania ni moja ya mataifa duniani ambayo yamenyakua tuzo ya Ushindi wa Kimataifa katika shughuli za elimu iliyotolewa mwaka 2010 na Umoja wa Mataifa (UN) kutokana na kuandikisha wanafunzi wengi wa kuingia darasa la kwanza.

Makala hii inaangazia mafanikio ya elimu katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika katika ngazi zote za elimu tangu mwaka 1961 hadi sasa ambayo Wizara inajivunia.

Pamoja na kwamba huduma za utoaji wa elimu katika shule za Awali, Msingi na Sekondari zimewekwa karibu zaidi na walengwa kwa kugatua usimamizi na uendeshaji wa shule hizo kwenda Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa mwaka 2009, historia yake inaanzia kwenye iliyokuwa Wizara ya Elimu na Utamaduni ambayo leo inajulikana kama wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Yapo mengi yaliyotekelezwa katika kipindi hicho kwa lengo la kuboresha elimu ikiwemo utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Elimu (ESDP) ambayo ilianza mwaka 1997 kwa lengo la kuhakikisha kuwa mipango ya elimu inatekelezwa kwa nchi nzima na kwa usawa. Ili kutekeleza programu hiyo, mipango mbalimbali ilianzishwa ikiwa ni pamoja na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) mwaka 2002; Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) mwaka 2004; na Mpango ya Maendeleo ya Elimu ya Juu (MMEJ) mwaka 2004.
Mradi mwingine ni Mradi wa Kuimarisha Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (LANES)

Mipango yote hii imeleta mabadiliko chanya katika eneo la elimumsingi ambayo sasa yanasimamiwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa huku Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ikibaki kutunga Sera, kusimamia utekelezaji wa Sera, kutoa Miongozo na Nyaraka mbalimbali za uendeshaji wa shughuli za elimumsingi.

Kabla ya Uhuru, Elimu kwa watu wenye Mahitaji Maalumu ilikuwa inatolewa na Taasisi za dini. Katika kipindi cha 1950 hadi 1960, kulikuwa na shule moja mkoani Dodoma iliyojulikana kama Wilson Carlile School for Blind Boys, kwa sasa inaitwa Buigiri Shule ya Wasiona.

Baada ya uhuru kumekuwa na ongezeko la shule za msingi zinazopokea wanafunzi wenye mahitaji maalumu kutoka shule 20 ilipofika mwaka 1978 na kwa sasa kuna shule 776 za msingi zinazopokea wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Ongezeko hilo la shule limechangia kuongezeka idadi ya wanafunzi kutoka wanafunzi 7 mwaka 1960 hadi kufikia wanafunzi 55,758 mwaka 2021.

Katika kuandaa walimu wenye taaluma ya elimu maalum, mwaka 1976, Serikali ilianza kuandaa walimu wa fani ya Wasioona na Viziwi katika Chuo Cha Ualimu Tabora kwa ngazi ya Astashahada. Aidha, Mwaka 1983 chuo hicho kilianza kuandaa walimu kwa ajili ya wanafunzi wenye Ulemavu wa Akili na mwaka 1996 Programu ya Ualimu wa Elimu Maalumu ilihamishiwa Chuo cha Ualimu wa Elimu Maalum Patandi ambacho kilianza kutoa kozi mbalimbali za Elimu Maalumu ngazi ya Astashahada na Stashahada. Hadi kufikia Mwaka 2004 kulikuwa na walimu 114 wenye Taaluma ya Elimu Maalumu ngazi ya Astashahada na walimu 47 ngazi ya Stashahada. Mwaka 2010 walimu walikuwa 1,104 ngazi ya Astashahada na 498 ngazi ya Stashahada. Mwaka 2021 idadi ya walimu wenye taaluma ya Elimu Maalumu ni 8,832 ngazi ya Cheti.

Mafunzo ya Elimu ya Ualimu kabla ya uhuru yalikuwa yakitolewa na mashirika ya dini katika kipindi cha miaka ya 1928 hadi 1960 ambapo kulikuwa na vyuo vitano. Baada ya Uhuru vyuo hivyo viliendelea kutoa mafunzo chini ya umiliki wa mashirikia hayo mpaka mwaka 1967 vilipochukuliwa na Serikali kufutia Azimio la Arusha na Sera ya Utaifishaji (Nationalization Policy).

Kati ya mwaka 1967 na 1980 Vyuo vya Ualimu viliendeshwa na Serikali vikijulikana kama Vyuo vya Elimu ya Taifa na mwaka 1995 vyuo hivi viliongezeka kwa idadi na kufikia 34, vyote vikiendeshwa na Serikali na vilijulikana kama vyuo vya Mafunzo ya Ualimu (TTCs).
kati ya mwaka 1995 na 2013 vyuo hivi viliongezeka hadi kufikia 126 baada ya Serikali kufungua fursa ya uwekezaji katika sekta binafsi ambapo kati ya vyuo hivyo vyuo 35 vinaendeshwa na serikali huku vikiendelea kuongoza kwa kudahili wanachuo wengi ambapo hadi mwaka 2021 vyuo hivyo vina wanachuo 19,193 wakati vyuo 91 vinaendeshwa na sekta binafsi kwa kutumia Mitaala na Miongozo ya Serikali.



Kwa upande wa miundombinu katika vyuo vya ualimu, kati ya mwaka 2015 na 2021 vyuo vya Serikali vya Kitangali, Kabanga, Ndala na Mpuguso vimejengwa upya baada ya miundombinu yake kuchakaa. Pia serikali imeviwezesha vyuo vya ualimu kupata vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia kadiri ya mahitaji ikiwemo vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na kuviunganisha kwenye mkongo wa Taifa wa mawasiliano.

Uthibiti Ubora wa Shule uliokuwa unafahamika kama ukaguzi wa shule ulianza zama za ukoloni wa Wajerumani kwa Waraka wa Elimu wa mwaka 1903 ambao ulisisitiza walimu kuwa na nidhamu safi, kufanya kazi kwa bidii na kufuata maadili ya serikali ya Wajerumani. Katika kipindi cha ukoloni wa Muingereza 1919 – 1961, mfumo wa ukaguzi wa shule ulibadilika kwa kukagua shule zote kwa kutumia Mtaala uliotungwa Kitaifa na kutoa ushauri na mapendekezo ya kutatua matatizo yaliyojitokeza shuleni.

Katika kuhakikisha vijana wa Kitanzania wanapata ujuzi na maarifa yatakayowawezesha kushindana katika soko la ajira kwa kujiari ama kuajiri, Serikali imejenga vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi vya mikoa na wilaya, kufanya upanuzi wa vilivyopo pamoja na kukarabati vilivyopo na kufanya idadi ya vyuo vya VETA kufikia vyuo 895 ikiwa vya serikali 852 na visivyo vya serikali 43 ikilinganishwa na kimoja kilichokuwepo mwaka 1961. Maboresho haya yamepelekea kuongezeka kwa udahili hadi kufikia 368,000 kwa mwaka ilinganishwa na wanafunzi 1,872 mwaka 1961.

Mfumo wa Elimu ya Juu Tanzania ulianza mwaka 1961 baada ya kuanzishwa kwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Dar es Salaam kama sehemu ya Chuo Kikuu cha London. Mwaka 1963 Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki kilianzishwa kikiwa na lengo la kuhudumia nchi tatu za Afrika Mashariki (Kenya, Tanzania na Uganda) ambapo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kikawa ni moja ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Chuo cha Afrika Mashariki. Mwaka 1970 Chuo Kikuu Kishiriki cha Dar es Salaam kilibadilishwa na kuwa Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam baada ya Shirikisho la Afrika Mashariki kupendekeza kila nchi kuwa na chuo kikuu chake.

Kutokana na mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kijamii, mwaka 1990 serikali iliruhusu sekta binafsi kutoa mchango katika utoaji wa Elimu ya Juu nchini. Mwaka 1996 vyuo vikuu vya binafsi vilianzishwa na kuongeza wigo mpana wa utoaji wa elimu na kufanya ongezeko la idadi ya vyuo vikuu kutoka chuo kikuu kimoja mwaka 1961 hadi kufikia Vyuo 47 mwaka 2021. Aidha vyuo vya umma ni 12, vya Binafsi 18, Vyuo Vikuu Vishiriki vya Umma7 na Vishiriki vya Binafsi 10.

Ongezeko la vyuo hivyo limekwenda sambamba na ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa kutoka wanafunzi 14 mwaka 1961 hadi kufikia wanafunzi 206,302 mwaka 2020/2021. Pia kumekuwa na ongezeko la wahadhiri kutoka sita mwaka 1961 hadi kufikia 7,187 mwaka 2020/2021. Kati yao wahadhiri 2,324 ni wa vyuo vikuu binafsi na wahadhiri 4,863 wa Vyuo Vikuu vya Umma.

Kutokana na ongezeko la vyuo vikuu nchini, Serikali iliona umuhumu wa kuanzisha chombo cha kusimamia ubora wa Elimu ya Juu nchini. Mwaka 1995, Serikali ilianzisha Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu (HEAC), ambapo kazi yake ilikuwa ni kuthibiti ubora wa vyuo vikuu nchini vilivyokuwa vinaanzishwa na kuendeshwa na taasisi binafsi. Mwaka 2005, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) ilianzishwa chini ya Sheria ya Vyuo Vikuu Sura 346 ya Sheria za Tanzania.

Baada ya kuona ongezeko la wanafunzi wa Elimu ya Juu, Serikali ilianzisha chombo kitakachosaidia kugharamia elimu ya juu kwa wanafunzi wasio na uwezo na kuanzisha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu(HESLB) mwaka 2005 ili iweze kutoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji. Kupitia Bodi ya Mikopo, Serikali imekuwa ikiongeza idadi ya wanufaika wa mkopo kila mwaka ili kuwanufaisha wanafunzi wengi zaidi, huku ikiendelea kuongeza tengeo la fedha za mikopo kutoka Sh bilioni 9.9 mwaka 2004/2005 hadi kufikia kiasi cha Sh bilioni 570 mwaka 2021/2022. Tangu kuanzishwa kwa Bodi ya Mikopo hadi mwaka 2020/2021, jumla ya watanzania 584,919 wamenufaika na mikopo hiyo ya takriban Sh trilioni 4.3.

Serikali imeendelea kuimarisha utoaji wa elimu ya juu kwa kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kujenga na kukarabati madarasa, kumbi za mihadhara, mabwalo ya chakula, maabara, maktaba, MABWENI, ununuzi wa vifaa vya utafiti na vifaa vya kujifunzia katika vyuo vikuu vya umma pamoja na kuongeza mitaala ya vyuo vikuu kutoka mtaala mmoja(1) mwaka 1961 hadi kufikia zaidi ya mitaala 260 mwaka 2021.



Sehemu ya Jiji la Dodoma, 2020

# Upimaji Ardhi kwa Kasi Wapunguza Makazi Holela

Na **Munir Shemweta, WIZARA YA ARDHI**

Ni ukweli usiopingika kuwa ardhi inabeba vitu vingi na hivyo kutolewa macho na wanadamu, wanyama na mimea. Kutokana na ukweli huo, ardhi inahitaji uangalizi wa pekee hususan katika kipindi hiki cha miaka 60 ya Uhuru ambacho ni sawa na umri wa kustaafu kwa watumishi wengi wa umma.

Wakati Tanzania Bara ikiadhimisha miaka 60 tangu ipate Uhuru wake mwaka 1961 Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi imendelea kupiga hatua kubwa katika juhudi za utekelezaji majukumu yake ikiwemo umilikishaji ardhi, kuboresha mazingira ya uwekezaji pamoja na ujenzi makazi bora kwa ajili ya shughuli za kijamii na kiuchumi.

Hatua kubwa na ya kujivunia iliyofanywa na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Kazi tangu Tanzania ipate uhuru wake kutoka kwa Wakoloni ni kuanzishwa ofisi za ardhi za mikoa, kuwezesha upatikanaji ardhi ya uwekezaji, kuimarisha usalama wa miliki, kushughulikia migogoro ya ardhi, upangaji na upimaji ardhi, kuboresha utunzaji taarifa za ardhi kutoka analogía kwenda digitali ikiwemo utoaji wa hati za kielektroniki pamoja na uboreshaji huduma kwa wateja.

Katika kusogeza huduma karibu na wananchi Wizara ilianzisha ofisi za ardhi za mikoa na kuzipatia vitendea kazi muhimu, rasilimali fedha, watumishi, mafunzo pamoja na kusimika mifumo unganishi ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi katika utoaji huduma. Awali ilimlazimu mwananchi kuifuata huduma Makao Makuu ya Wizara ama ofisi za ardhi za kanda zilizokuwa zikihudumia zaidi ya mikoa mitatu. Uamuzi huo wa kuanzishwa ofisi za ardhi za mikoa umeondoa kero na mzigo wa gharama kwa wananchi kwenye masuala ya ardhi.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Wizara ya Ardhi, katika kutimiza azma ya Serikali ya kuwa na ardhi ya uwekezaji, ardhi yenye ukubwa wa ekari 12,488 zilitengwa kwa ajili ya uwekezaji kati ya ekari 612,133.38 zilizopatikana kutokana na ubatilisho wa mashamba makubwa yaliyotelekezwa na wamiliki katika mikoa mbalimbali nchini. Pia ardhi yenye ukubwa wa ekari 224,439.4 zimetengwa kwa ajili ya uwekezaji kupitia Mipango Kabambe ya miji, mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya na Vijiji. Ardhi imemilikishwa kwa wawekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji (EPZA) na ardhi ya akiba (Land Bank).

Wizara imeendelea kushughulikia migogoro ya ardhi iliyohusisha migogoro ya mipaka ya kiutawala na ile inayotokana na mwingiliano wa matumizi ya ardhi. Aidha, kupitia tathmini iliyofanyika imebainika kwamba vyanzo vya migogoro ni pamoja na ongezeko la watu, uanzishwaji wa maeneo mapya ya kiutawala pasipo kuzingatia taratibu na muingiliano wa matumizi ya ardhi kutokana na mahitaji mbalimbali ya watumiaji.

Wizara ya Ardhi kupitia Mabaraza ya Ardhi imeendelea kutatua migogoro mbalimbali inayohusiana na masuala ya ardhi. Baada ya uhuru, utatuzi wa migogoro ya ardhi ulikuwa unafanyika kupitia mabaraza ya kimila na mfumo wa mahakama za kawaida. Hata hivyo, utatuzi wa migogoro ya ardhi kupitia mfumo wa mahakama ulibainika kuwa na changamoto za mrundikano wa mashauri na matumizi ya mbinu nyingi za kisheria katika utatuzi wa migogoro na kulazimika kuanzishwa mfumo mahsusi wa utatuzi wa migogoro ya ardhi.

Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Na. 2 ya mwaka 2002 (Sura ya 216) ilitungwa na kubainisha mfumo maalum wa utatuzi wa migogoro ya ardhi unaojumuisha Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji, Mabaraza ya Kata, Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa ambapo tangu kutungwa kwa sheria hiyo mwaka 2002, jumla ya mashauri 214,588 yalifunguliwa na mashauri 187,618 yameamuliwa. Aidha, Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yameanzishwa katika Wilaya zote 139 ambapo kati ya hayo, Mabaraza 60 yanatoa huduma. Dhamira ya Wizara ni kuhakikisha kuwa Mabaraza katika Wilaya zote nchini yanatoa huduma.

Wizara ya Ardhi imeendelea kupiga hatua katika mipango yake mbalimbali ili kurahisisha zoezi la upangaji na upimaji. Wizara imenunua vifaa vya kisasa vya upimaji na ramani kama vile ndege isiyokuwa na rubani (drone) kwa ajili ya upigaji picha za anga; vifaa vya upimaji ardhi vinavyotumia satelaiti (Global Positioning System-GPS) vyenye uwezo wa kupima takriban viwanja 50 kwa siku na vifaa hivyo vimesambazwa katika mikoa 26 nchini na darubini za kisasa za upimaji ardhi (Total Station).

**Taaluma ya Mipango Miji ilianza kutolewa nchini mwaka 1972 kupitia Chuo cha Ardhi. Katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru Serikali imewezesha kuanzishwa Chuo Kikuu Ardhi na vyuo vya kada ya kati vinavyotoa Stashahada ya Mipango Miji nchini.**

‘Halmashauri zote nchini zihakikishe zinatenga fedha kwa ajili ya upangaji, upimaji, umilikishaji wa ardhi pamoja na ununuzi wa vifaa, usimikaji wa mifumo ya TEHAMA na uwekaji wa miundombinu hususan barabara kwenye maeneo yao kwani Halmashauri ndio wenye ardhi na pia ni Mamlaka za Upangaji wa ardhi zao kwa mujibu wa sheria'', alisema Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe. William Lukuvi wakati akiwasilisha makadirio ya Bajeti ya Wizara yake kwa mwaka 2021/2022.

Wizara pia imeendelea na upimaji ardhi katika maeneo ya mipaka ya nchi ili kuimarisha ulinzi na usalama ikiwa ni pamoja na uimarishaji wa alama za mipaka ya Kimataifa ambapo Serikali kupitia Wizara ya Ardhi imekuwa na jukumu la kuhuisha alama za mipaka ya Tanzania na nchi jirani. Tanzania inapakana na nchi kumi kwa mpaka wenye urefu wa kilomita 1,841 nchi kavu na kilometa 2,086 ndani ya maji.

Kuhusu Sekta ya Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Ardhi imekuwa ikikua katika hatua mbalimbali tangu ilipoanzishwa mwaka 1959 kwa Sheria ya Mipango miji na nchi Sura ya 378 (Sheria ya Mipango Miji na Nchi ya Mwaka 1959).

Katika kipindi nchi inapata uhuru, taaluma ya Mipango Miji haikuwa ikipatikana nchini isipokuwa katika nchi ya Kenya na Ghana kwa Bara la Afrika na nchi za Magharibi na Ulaya. Taaluma ya Mipangomiji ilianza kutolewa nchini mwaka 1972 kupitia Chuo cha Ardhi. Katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru Serikali imewezesha kuanzishwa Chuo Kikuu Ardhi na Vyuo vya kada ya kati vinavyotoa Stashahada ya Mipango Miji nchini.

Katika kipindi cha miongo minne tangu uhuru, Wizara ilikua inatumia mfumo wa majalada pekee katika kutunza kumbukumbu za ardhi (analogia). Mfumo huo ulihifadhi kumbukumbu za upimaji, ramani, mipango miji, uthamini, hatimiliki katika nakala ngumu. Hali hii ilisababisha uhitaji wa eneo kubwa la kuhifadhi majalada, muda mwingi wa kutafuta majalada, ongezeko la kero zinazotokana na milki pandikizi na mahitaji makubwa ya rasilimali watu na fedha.

Ndani ya kipindi cha miaka 60 ya uhuru, Wizara imeboresha utunzaji wa taarifa za ardhi kwa kuunda mifumo mbalimbali ya TEHAMA kwa ajili ya kurahisisha utendaji kazi katika Sekta ya Ardhi. Mifumo hiyo ni pamoja na Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Ardhi pamoja na Usajili wa hati, Mfumo wa Usimamizi wa Kodi ya pango la Ardhi, Mfumo wa Uidhinishaji wa kazi za Upimaji na Ramani, Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Majalada na Mfumo wa Taarifa za mashamba. Mifumo hiyo ilirahisisha utoaji wa huduma za ardhi pamoja na utunzaji wa kumbukumbu kwa njia ya kielektroniki ambazo awali zilikuwa zikihifadhiwa katika majalada.

Aidha, katika kuboresha huduma kwa wateja, Wizara imeanzisha kituo cha mawasiliano kwa wateja (Call Centre +255 739 646 885) katika Ofisi ya Makao Makuu ya Wizara Jijini Dodoma. Lengo ni kuwezesha mawasiliano ya moja kwa moja na wateja popote walipo kwa njia za kielektroniki na kutatua changamoto zinazowakabili bila kulazimika kufika katika ofisi za ardhi Utaratibu huo unawapunguzia wananchi kero, gharama za usafiri na muda wa kupata huduma.

Wizara pia imeboresha ukadiriaji wa kodi ya pango la ardhi mtandaoni ambapo mwananchi anaweza kulipia kodi ya pango la ardhi kupitia simu ya mkononi (*152*00#). Vilevile, wizara imewezesha ukadiriaji wa kodi kupitia tovuti (www.lands.go.tz) ambapo mteja anaweza kulipa kwa awamu. Aidha, Wizara ina Mkataba wa Huduma kwa Mteja ambao ni mwongozo wa utoaji wa huduma. Mkataba huo unapatikana kupitia tovuti ya Wizara.

Katika kuondoa adha ya Makazi holela nchini, Wizara ya Ardhi imetekeleza mpango wa Urasimishaji makazi unaohusisha kutambua, kupanga, kupima na kumilikisha maeneo yaliyoendelezwa bila kupangwa. Lengo la urasimishaji ni kuhakikisha usalama wa milki na kuwezesha upatikanaji maeneo kwa ajili huduma za kijamii na miundombinu kwa njia shirikishi.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imedhamiria kuendelea kufanya mageuzi makubwa kwenye sekta ya ardhi kwa kutumia teknolojia za kisasa iliyowezesha utoaji wa hati za Kielektroniki. Mageuzi hayo yanalenga kuwawezesha wananchi kiuchumi na kijamii, kuimarisha usalama wa milki za ardhi na kuongeza thamani ya ardhi na hivyo kuongezeka kwa pato la Taifa.

Aidha, Serikali imetoa shilingi Bilioni 474.5 kuzipatia taasisi za kifedha 32 ili kuwezesha wananchi kukopa kwa ajili ya ujenzi wa makazi bora.

Vile vile Wizara imeshiriki katika utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati ya Kitaifa kwa kupanga, kupima na kufanya uthamini wa ardhi na mali kwenye maeneo ya miradi hiyo. Miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere, Bomba la Mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani Tanga nchini Tanzania na ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR).




Kituo cha Treni cha Dar es Salaam, 1973

**Serikali imetoa shilingi Bilioni 474.5 kuzipatia taasisi za kifedha 32 ili kuwezesha wananchi kukopa kwa ajili ya ujenzi wa makazi bora.**



# Tulikua Askari wa Kalamu, Mwalimu Nyerere Alitufunda

Na **Immaculate Makilika - MAELEZO**

**Tulifanya kazi kwa moyo wa furaha, Mwalimu Nyerere alifanya kazi kwa karibu na waandishi wa habari alikuwa Mhariri Mkuu, alikutana na waandishi wa habari kila baada ya miezi mitatu, alifanya hivyo kutufunda, yeye alisema mimi nasema huyu ni panya nyinyi mnasema huyu ni tembo nikisema huyu ni tembo itakuwaje? Kwa hiyo alitufundisha siasa pia"**
Scholastica Sylvan Kimario, Mwandishi Nguli

Mwaka 1969 ikiwa ni miaka 8 ya Uhuru, mwandishi nguli, Scholastica Kimario anasimulia jinsi yeye na wenzake walivyofundwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Awamu ya Kwanza ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhariri Mkuu wa Magazeti ya Serikali, Tanganyika Standard Newspapers.

Mwandishi huyu bila kumung'unya maneno anasema, "Tulifanyakazi kwa moyo wa furaha, Mwalimu Nyerere alifanya kazi kwa karibu na waandishi wa habari alikuwa Mhariri Mkuu, alikutana na waandishi wa habari kila baada ya miezi mitatu, alifanya hivyo kutufunda, yeye alisema mimi nasema huyu ni panya nyinyi mnasema huyu ni tembo nikisema huyu ni tembo itakuwaje? Kwa hiyo alitufundisha siasa pia".

"Alitufundisha kuhusu nchi zisizofungamana na upande wowote (NAM), vilevile alitueleza kuhusu umuhimu wa uhusiano wetu na China, Ujamaa", anaongeza Kimario.
Hakusita kueleza kuhusu hali ya maslahi ilivyokuwa, akisimulia kwa tabasamu murua kuwa mishahara ilikuwa midogo, hawakuwa na usafiri bali walitembea kwa miguu na baadhi ya waandishi wa habari wa wakati huo akiwemo Rais wa sasa wa Uganda, Yoweri Kaguta Museveni.

Akiwa mwanahabari mmojawapo kati ya wanahabari wanawake watatu ambao waliandikia magazeti ya chama wakati huo ambao ni Anna Kasambala na Theresia Mshuza, anasema kuwa alijiunga na uandishi wa habari akiwa mwanafunzi wa Chuo, kwa vile wakati huo kulikua na utaratibu wa 'cub reporter' huku akiandikia magazeti ya Nationalist na Mzalendo na baada ya kumaliza Chuo mwaka 1971 aliandikia gazeti la Tanganyika Standard Newspapers na baadae Daily News na Sunday News.

Kwa bashasha anasimulia,"Wakati huo tulikuwa askari wa kalamu na wana mapinduzi tuliokuwa tukipigania Uhuru wa kusini mwa Afrika, Palestina na mahali popote duniani, Tanzania ilijiweka mahali pa mbele sana, tulikuwa tunafanya kazi kwa karibu na wapigania uhuru kila tunachokiandika tuliangalia tunawezaje kusaidia katika harakati za kudai Uhuru".

Mwandishi huyu nguli anaeleza kuwa, alivyokuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Waandishi wa Habari Tanzania (TAJA), mara baada ya Nelson Mandela na Robert Mugabe waliokuwa vinara wa harakati za Uhuru katika nchi zao kumaliza shughuli zao hapa nchini waliwaaga kwa kuwafanyia sherehe katika Hoteli ya New Africa ambapo waliwapa zawadi za kalamu na kuwaambia kuwa sasa mnatoka mbugani kalamu ndio itakuwa silaha yenu.

'Every new day is a new challenge!' Hapa akieleza kuwa hakuwahi kuona changamoto kubwa wakati wote alipokuwa akifanya kazi yake ya uandishi wa habari, kila siku mpya alijipanga kujifunza mapya na mbinu mpya kazini.

Hata hivyo anawakumbusha waandishi wa habari wa miaka ya sasa kuwa na ajenda za masuala mbalimbali, "leo nikingalia sioni waandishi wa habari wakitilia mkazo ajenda za nchi, wakati huo Azimio la Arusha liliutuongoza sana, tuliunga mkono mabadiliko ambayo nchi ilichukua kuhusu masuala mbalimbali".

Anasisitiza kuwa, Mwalimu Nyerere alikuwa na ajenda ya wazi ya kujenga nchi, mfano elimu kwa wanawake au wafanyakazi kupitia vyama yeye aliamini kwanza kujenge taifa, alitaka tuelewane, kulikuwa na 'huge national agenda' ya kujenga ujamaa na maendeleo ya watu.

Kwa sasa Bi. Scholastica Sylvan Kimario ni Mwanzilishi na Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Maadili Leadership Solutions.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Misri, Mhe. Abdel Fattah Al Sisi wakikagua gwaride maalum la Jeshi la Misri baada ya Rais Samia kuwasili Ikulu Cairo nchini Misri tarehe 10 Novemba, 2021 kwa ajili ya kuanza ziara ya Kiserikali ya siku tatu kufuatia mwaliko wa Rais wa Abdel Fattah Al Sisi.

# Miaka 60 ya Uhuru: Tanzania Yaongozwa na Rais wa Kwanza Mwanamke

Na **Grace Semfuko-MAELEZO**

Tangu Tanganyika ipate Uhuru Tarehe 9 Desemba 1961, kumekuwa na mabadiliko makubwa ya usawa wa kijinsia, ambapo wanawake wanapata nafasi mbalimbali za uwakilishi kwenye nyanja za kijamii, kisiasa, kiutamaduni pamoja na kiuchumi.

Wakati Mataifa mbalimbali Duniani yakipigania kuhakikisha kunakuwa na usawa wa kijinsia kwenye maeneo mbalimbali, Tanzania imepiga hatua kubwa ya angalau kufikia usawa huo ingawa wasomi na wataalamu wa kijinsia wanasema bado hivyo tuendelee kukaza buti kuufikia usawa wa 50 kwa 50.

Wakati wa kupigania uhuru, wanawake walifanya kazi ya kuhakikisha wanashirikiana na wanaume katika kupambana na mkoloni ili wawe huru ambapo katika harakati hizi, Bibi Titi Mohammed pamoja na wanawake wengine walikuwa mstari wa mbele.

Jinsia ni dhana inayotumika katika kuelezea tofauti za kimaumbile kati ya mwanamke na mwanaume, kwa kawaida, binadamu huzaliwa na jinsi ya kike au kiume, jinsi hizi ni tofauti ya kibaolojia.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan ni Mwanamke anaeiongoza nchi na imekuwa na ustawi mkubwa wa kimaendeleo, hii inaonesha kuwa wanawake wanaweza kuleta mabadiliko ya kiuongozi, kiuchumi na kisiasa.

Tunaposema kumekuwa na mabadiliko makubwa ya usawa wa kijinsia tuna maana kubwa kwani ukiangalia wakati Tanganyika ilipopata Uhuru Mwaka 1961 ikiongozwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Baba wa Taifa aliunda Baraza la Mawaziri ambalo halikuwa na mwanamke ambaye alikuwa Waziri kamili.

Taarifa za kihistoria zinasema kuwa Mwanaharakati mashuhuri katika kupigania uhuru kwa wakati huo, Bibi Titi Mohammed alimwendea Mwalimu na kumuuliza kulikoni hakuna mwanamke ambaye ni Waziri, Nyerere alimjibu kuwa amejitahidi lakini imekuwa ni vigumu kumpata Mwanamke mwenye sifa stahiki kuwa Waziri kamili , bali Naibu Waziri, ndipo Bibi Titi akamuuliza "Hao wanaume wenye sifa leo walikuwa wapi wakati tunapigania uhuru?"

Bibi Titi Mohammed ni mfano mmoja wapo wa Wanawake shupavu katika kupigania usawa wa kijinsia ambaye alikuwa mstari wa mbele katika kupigania uhuru wa Tanganyika, tunapotafuta historia ya usawa wa kijinsia hatuwezi kuacha kumtaja mwanamke huyu.

Wanawake wengine walioonesha kuwa makini na kuweza kuzisimamia nafasi zao ni pamoja na Mama Getrude Mongella ambaye ni sehemu ya utajiri ambao Tanzania imebarikiwa kuwa nao kwani ni Mwanamke mwenye vipaji na uwezo wa kuongoza na kuiwakilisha jamii katika nyanja mbalimbali za kijamii na kisiasa akishika nafasi mbalimbali za uongozi ambazo zilidhaniwa kuwa ni za wanaume pekee.

"Kama unataka kuwa kiongozi ni lazima uwe una picha kamili ya unachotaka, lazima usimamie kanuni na maadili, hivyo vitu havitawezi kukuangusha kamwe" alisema Getrude Mongella wakati wa Mkutano wa 'African Women's Forum' nchini Ghana mwaka 1997.

Mongella ni mwanamke wa kitanzania aliyekuwa Rais wa kwanza wa Bunge la Umoja wa Afrika mwaka 1993 hadi 1995, alikuwa Katibu Mkuu wa Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Masuala ya Wanawake na kuhudhuria Mkutano wa nne uliofanyika Beijing nchini China mwaka 1995.

Tanzania imebarikiwa kuwa na wanawake shupavu wanaotambulika ndani na nje ya nchi katika umahiri wao kwenye utendaji kazi, mfano mzuri ni Dkt. Asha-Rose Migiro ambaye aliwahi kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na alifanya vizuri na kuaminika kitaifa na kimataifa akiwa ni mfano bora wa wanawake wa Kitanzania wenye uwezo mkubwa katika uongozi wa kisiasa.

Wapo wanawake viongozi mbalimbali nchini wakiwepo Mawaziri, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Taasisi mbalimbali ambao wanafanya vizuri. Baadhi ya viongozi hao ni pamoja na aliyekuwa Spika wa Bunge wa kwanza mwanamke, Mama Anne Makinda, Dkt. Tulia Ackson, Naibu Spika wa Bunge hadi sasa, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Mhe. Sofia Mjema, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Mhe. Dkt. Batilda Buriani na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dkt. Stergomena Tax bila kumsahau Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dkt. Doroth Gwajima, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Mhe. Jenista Mhagama na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji.

Mwaka 2015 wakati wa uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani, kwa mara ya kwanza Tanzania ilibahatika kupata mgombea pekee wa nafasi ya Urais Mwanamke kupitia chama cha ACT-Wazalendo, Marehemu Mama Anna Mghwira, na chama chake kilimmwagia sifa nyingi kwamba ni kiongozi bora.

Azimio la kuwepo kwa Protokali ya Jinsia na Maendeleo kwa Nchi za SADC imekuwa ni chachu ya maendeleo na jinsia kwa nchi nyingi za ukanda wa kusini. Ikiwa na vigezo vipatavyo 30 vya kufikia malengo yaliyoainishwa ili kuweza kuwa na usawa wa kijinsia hadi mwaka 2015, hatua hii ya mafanikio ni ya kwanza katika dunia na imeiweka jumuiya ya SADC katika mhimili wa juu katika utambuzi wa mikakati kushawishi utandawazi katika bara zima la Afrika na dunia kwa kuonyesha jitihada kwa upande wa kusini mwa Afrika.

Nchi ya Tanzania imeshaonyesha nia ya kupambana na baadhi ya sheria kandamizi ili kuwawezesha wanawake waweze kurithi mali zao na siyo kuwa wategemezi kwa baba, waume, watoto wao wa kiume pamoja na ndugu yeyote wakiume.

Jinsia ni dhana ambayo hutumika katika kuelezea mahusiano ya kijamii yaliyojengeka kati ya mwanaume na mwanamke, dhana hii hutumika kuelezea tafsiri ya jamii kuhusu maana ya kuwa mwanamke au mwanaume, ikiwa inatoa utofauti katika thamani ya utu wao, stahili na haki zao pamoja na nafasi zao kama vile wajibu au kazi, madaraka, maamuzi na umilki wa rasilimali.

Katiba ya Tanzania imeridhia kuwepo kwa usawa wa jinsia, ingawa mpaka sasa bado zipo baadhi ya sheria zinazofuata mila za baadhi ya makabila ya Tanzania zinakinzana na katiba, mpaka kufikia mwaka 2015 yapo marekebisho makubwa yalikayokuwa yamefikiwa na Serikali ya Tanzania kwa kushirikisha Asasi za kiraia.



# Miaka 60 ya Uhuru: Mipaka ya Tanzania Ipo Salama

Na **Luteni Kanali Josephat Musira**

**Taasisi zilizoanzishwa chini ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania-JWTZ (1964), Jeshi la Kujenga Taifa-JKT (1963), Shirika la Uzalishajimali la Jeshi la Kujenga Taifa-SUMAJKT (1982), Shirika la Nyumbu (1985) na Shirika la Mizinga (1971).**

Tanzania ina eneo lenye jumla ya kilomita za mraba 947,303 na mipaka yenye urefu wa kilomita 5,461.20 inayohusisha eneo la nchi kavu na eneo la maji. Hali ya mipaka ya nchi hii imeendelea kuwa shwari ndani ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara.

Usalama wa nchi yetu ni matunda ya maono ya Baba wa Taifa Hayati Julius Kambarage Nyerere aliyeamua kuanzisha wizara inayosimamia ulinzi wa taifa ikijulikana kwa jina la Wizara ya Mambo ya Nje na Ulinzi chini ya Waziri, Mhe. Oscar Kambona.

Mnamo 1964 Wizara ilibadilishwa jina na kuitwa Wizara ya Ulinzi, JKT na Vijana na kuhamishiwa Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Rashid Mfaume Kawawa.

Mwaka 1972, Wizara hii iliitwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Waziri wake akawa Mhe. Edward Moringe Sokine akifuatiwa na Mhe. Rashid Kawawa, Meja Jenerali Abdallah Twalipo, Brigedia Muhidini Kimario, Dkt. Salim Ahmed Salim, Mhe. Amran Mayagila, na Mhe. Jackson Makweta.

Wengine ni Mhe. Abdulrahman Kinana, Mhe. Maokola Majogo, Prof. Philemon Sarungi, Prof. Juma Kapuya, Dkt. Hussein Mwinyi, Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mhe. Elias John Kwandikwa na Dkt. Stergomena Tax.

Katika miongo sita ya uhuru wa Tanzania Bara, Wizara hii imepata mafanikio mengi yaliyochochewa na maono ya viongozi wa Awamu zote akiwemo Rais wa Awamu ya Sita na Amiri Jeshi Mkuu, Mhe. Samia Suluhu Hassan.

Miongoni mwa mafanikio hayo ni kuanzisha taasisi mbalimbali chini ya Wizara hii, ujenzi wa vyuo vya kijeshi, kuimarisha maslahi ya wanajeshi, ushindi katika Vita vya Kagera, ukombozi wa Bara la Afrika na ushiriki wa Tanzania katika opereshezi za ulinzi wa amani.

Taasisi zilizoanzishwa chini ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania-JWTZ (1964), Jeshi la Kujenga Taifa-JKT (1963), Shirika la Uzalishajimali la Jeshi la Kujenga Taifa-SUMAJKT (1982), Shirika la Nyumbu (1985) na Shirika la Mizinga (1971).

JWTZ na JKT zimekuwa zikishiriki katika shughuli za kuwaokoa Watanzania na watu wengine wanaoishi nchini pindi majanga yanapotokea ikiwemo ajali ya MV Spice Islander. JKT imekuwa ikijenga vijana wazalendo wenye maadili mema, ikichangia nguvukazi kwenye ujenzi wa vituo vya huduma za jamii, pamoja na kuendesha miradi ya kilimo inayochangia kwenye usalama wa chakula nchini.

Pia, Wizara imejenga vyuo vya kijeshi ambavyo vimepunguza gharama ya kuwapeleka askari wa Tanzania nje ya nchi kwa ajili ya kupata mafunzo ya kitaalamu. Vyuo vilivyoanzishwa ni Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi Monduli-TMA (1970), Chuo cha Ukamanda na Unadhimu-CSC (1979) na Chuo cha Ulinzi cha Taifa-NDC (2012). Wanajeshi kutoka mataifa mbalimbali wanakuja kwenye vyuo hivi kujifunza masuala ya kijeshi.

## TANZANIA BARA

**Tanzania ina eneo lenye jumla ya kilomita za mraba 947,303 na mipaka yenye urefu wa kilomita 5,461.20 inayohusisha eneo la nchi kavu na eneo la maji.**

Vilevile, Wizara kupitia JWTZ kwa kushirikiana na Chuo cha Uhasibu – Arusha imeanzisha program mbalimbali ikiwemo Kozi ya Shahada ya kwanza ya Sayansi ya Kijeshi (Bachelor of Military Science). Miongoni mwa jitihada zilizofanywa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika kuimarisha maslahi ya askari na familia zao ni ujenzi wa miundombinu na makazi. Serikali kupitia Wizara imejenga nyumba zaidi ya 6,064 kwa ajili ya wanajeshi katika mikoa tisa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Kagera, Kigoma, Morogoro, Pemba, Pwani na Tanga.

Ujenzi wa nyumba hizo unaenda sambamba na ukarabati wa nyumba zinazotumiwa na wanajeshi pamoja na majengo ya huduma kama vile Hospitali, mabwalo, Shule, Vyuo na miundombinu mingine.

# "Kazi Mliyotutuma, Tumeimaliza"

JWTZ, 1980

## VITA VYA KAGERA

Pamoja na mafanikio hayo, Tanzania ilikabiliwa na changamoto ya kiusalama kwenye mpaka wake wa wa kaskazini wenye kilomita 1,281.2 ambapo Tanzania inapakana na nchi za Kenya na Uganda. Tarehe 30 Oktoba, 1978 Nduli Idd Amin aliyaamuru majeshi yake kuivamia Tanzania kwa madai kwamba eneo la Kagera ni sehemu ya Uganda.

Majeshi hayo yalifanya uharibifu mkubwa wa mali, pamoja na kuua watu wengi katika eneo hilo. Tarehe 02 Novemba, 1978 Amiri Jeshi Mkuu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alitangaza uamuzi wa kuyaondoa Majeshi ya Uvamizi.

Hadi kufikia tarehe tarehe 25 Novemba, 1978 Majeshi ya Nduli Amin yalikuwa yamepigwa na kufukuzwa kutoka eneo lote la Kagera. Majeshi ya Tanzania kwa kushirikiana na Jeshi la Ukombozi la Uganda yaliingia nchini Uganda na kuuteka Mji Mkuu wa Kampala tarehe 25 Aprili, 1979 hali iliyopelekea Nduli Amin kuikimbia nchi yake.

Majeshi yetu yalirejea kishujaa mwaka 1980 na kauli nzito kwa watanzania kuwa "Kazi Mliyotutuma, Tumeimaliza".


## MCHANGO WA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA ULIMWENGUNI

Wizara kupitia JWTZ ina mchango katika maeneo yafuatayo; kushiriki harakati za ukombozi Barani Afrika na ushiriki wa JWTZ katika operesheni za ulinzi wa amani.

Historia na mchango wa JWTZ katika kusimamia masuala ya ukombozi inatokana na Sera ya Taifa ya Mambo ya Nje ya mwaka 1964. Lengo kuu la Sera hii ilikuwa ni kuhakikisha kuwa nchi zote za Afrika zilizokuwa hazijapata Uhuru zinakuwa huru.

JWTZ ilitoa mchango mkubwa kwa kutoa mafunzo ya kijeshi kwa wapigania uhuru wa vyama vya ukombozi vya FRELIMO (Msumbiji), MPLA (Angola), ZANU PF (Zimbabwe), SWAPO (Namibia), PAC na ANC vya Afrika Kusini. Mbali na kushiriki katika kutoa mafunzo kwa wapigania uhuru; Jeshi pia, lilipigana bega kwa bega na wapigania uhuru katika nchi husika.

Sambamba na hilo, katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru JWTZ imeendelea kushiriki katika Ulinzi wa Amani sehemu mbalimbali Duniani. Mataifa ambayo JWTZ imeshiriki kikamilifu katika ulinzi wa amani ni; Liberia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, nchini Lebanon, Darfur Sudan, Sudan ya Kusini, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Ivory Coast, Sierra Leone, Mpaka wa Ethiopia na Eriteria, Visiwa vya Shelisheli, Msumbiji na Visiwa vya Anjuan – Comoro.
Katika miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa limeifanya Tanzania kuwa sio tu miongoni mwa nchi zenye amani na utulivu duniani, bali inayochangia kwenye kuimarisha amani ulimwenguni. Miaka 60 ya Uhuru: Tanzania Imara; Kazi Iendelee.



**Katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru JWTZ imeendelea kushiriki katika Ulinzi wa Amani sehemu mbalimbali Duniani. Mataifa ambayo JWTZ imeshiriki kikamilifu katika ulinzi wa amani ni; Liberia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, nchini Lebanon, Darfur Sudan, Sudan ya Kusini, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Ivory Coast, Sierra Leone, Mpaka wa Ethiopia na Eriteria, Visiwa vya Shelisheli, Msumbiji na Visiwa vya Anjuan – Comoro.**



# Tanzania Yaendelea Kuwa Kinara wa Diplomasia Duniani

Miaka 60 ya Uhuru, Tanzania Imara, Kazi Iendelee ni kaulimbiu ya madhimisho ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania, kauli ambayo inasadifu kinagaubaga uwezo wa nchi, mafanikio na hatma yake. Katika nyanja ya diplomasia nchi hii imeupiga mwingi kama vijana wa sasa wanavyosema, kwa muktadha huu, Tanzania imeonesha umahiri mkubwa katika kuonesha misimamo yake hata kwa mataifa yanayotajwa kuwa na nguvu kiuchumi.

Na **Immaculate Makilika - MAELEZO**

Hiyo imedhihirika pale ambapo Balozi wa kudumu wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa, Balozi Salim Ahmed Salim alipotetea taifa la China ili lipate nafasi katika Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa.

Imekuwa fahari na heshima kwangu kusikia simulizi hizi za kweli na za kusisimua kutoka kwa waheshimiwa Mabalozi waliowahi kuhudumu katika nafasi mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Kwa bashasha na utulivu Balozi Elly Mtango anaanza kwa kueleza kuwa kabla ya kupata uhuru Tanzania Bara imekuwa chini ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wakati huo akiwa Waziri Mkuu wa Tanganyika ambapo ilidai haki za watu wote ulimwenguni hasa wanaonyanyaswa pamoja na kuhamasisha umoja wa nchi bila kujali dini wala kabila, viongozi walitia mkazo kuzungumza lugha ya Kiswahili kitu ambacho kinaongoza nchi na kimeletea heshima ulimwenguni kote.

Aidha, anaendelea kusema kuwa diplomasia ni kiunganishi na kitu muhimu kinachosaidia kujenga mahusiano mema duniani. Diplomasia kabla ya miaka 60 ya Uhuru, Tanzania ilikuwa nchi jasiri katika kuchukua misimamo ya kuzungumza katika nyanja mbalimbali za kimataifa, mambo iliyoyatilia maanani ni haki ambapo ilikua mstari wa mbele kutetea haki popote pale duniani ambapo haki haikutendeka hasa katika Ukanda wa Afrika.

Tanzania imekua hodari kutetea nchi za kusini au mahusiano kati ya nchi zote ulimwenguni zisizofikia kiwango kikubwa cha maendeleo, Baba wa Taifa Mwaimu Julius Nyerere alifundisha taifa hili diplomasia anasema Balozi Mtango.

"Mwalimu Nyerere alikua kiongozi mahiri, ambapo alishirikiana pia na viongozi wengine kama Indra Gandhi wa India, Mahatri Mohamed aliyekuwa Waziri Mkuu wa nchi ya Malaysia, Mwalimu Nyerere alitufundisha wanadiplomasia wa Tanzania argue don't shout, yaani usiwe unafoka utoe hoja, usemi huu umekua kama taa ambao umekuwa ukitumulikia njia katika mijadala ya kimataifa" anasema Balozi Mtango.

Akifafanua uwezo wa Tanzania katika anga za kimataifa, Balozi Mtango anasema ujumbe wa Tanzania ulisikilizwa na nchi ndogo na kubwa ulimwenguni, kwa sababu Mwalimu Nyerere alitufundisha msimamo wa kutetea haki na usawa.

Balozi Mtango anatoa mtizamo wake kwa Tanzania ifikapo mwaka 2081 kuwa ni muhimu Tanzania ikaendelea kuwa taifa lenye msimamo, taifa lenye kuendelea kusimamia haki, pia liwe Taifa lenye kujenga uchumi imara ndani na nje ya mipaka yake mfano katika Jumuiya ya Nchi za Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), vilevile nchi za kiafrika ziwe na umoja wa watu weusi kote ulimwenguni kwa vile watu weusi wanakabiliwa na ubaguzi wa rangi.

Aidha, Balozi Peter Kalaghe ambaye alikuwa Balozi wa Tanzania nchini Uingereza anasema kuwa Tanzania huru imekua mtetezi madhubuti wa maslahi ya Afrika duniani kwa kushirikiana na mataifa mengine katika kulinda haki za wanyonge, akitolea mfano hivi karibuni ambapo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan alikuwa Glasgow Scotland kuhutubia masuala ya tabia nchi ikiwa ni katika kutoa sauti ya watu wanaoathirika na tabia nchi ulimwenguni.

> **"Mwalimu Nyerere alikua kiongozi mahiri, ambapo alishirikiana pia na viongozi wengine kama Indra Gandhi wa India, Mahatri Mohamed aliyekuwa Waziri Mkuu wa nchi ya Malaysia, Mwalimu Nyerere alitufundisha wanadiplomasia wa Tanzania argue don't shout, yaani usiwe unafoka utoe hoja, usemi huu umekua kama taa ambao umekuwa ukitumulikia njia katika mijadala ya kimataifa**
> Balozi Elly Mtango

Balozi Kalaghe anasema "Tanzania ina sauti ya kuheshimika sana kama ilivyo katika Umoja wa Afrika au Nchi za Kusini mwa Afrika kwa sababu ya kutetea wanyonge pia tunaheshimika kwa nguvu ya kidiplomasia ambayo hailingani na uwezo wetu kiuchumi. Katika diplomasia watu wanaangalia una uchumi kiasi gani sasa sisi sauti yetu ni kubwa kuliko uchumi wa nchi yetu na hii imejengwa na Serikali za Awamu zote na kufanya tuwe na ushawishi mkubwa".

Vilevile nilipenda kuzungumza na mwanamama ambaye licha ya kuwa Balozi wa Umoja wa Afrika huko nchini Marekani mwaka 2007, alibadilisha taswira ya siasa nchini kwa kutangaza kuwania ngazi ya Urais ndani ya chama chake cha CCM katika Uchaguzi mkuu wa 2015.

Balozi Amina Salum Ally anasema kuwa maisha ya diplomasia yanabadilika kulingana na wakati, miaka ya nyuma masuala mengi yalikua siasa na ukoloni, kwa kipindi hiki maendeleo ya dunia yanategemea uchumi, akitolea mfano wa kuwepo kwa diplomasia ya michezo ambapo Tanzania ilishiriki vizuri wakati huo.

"Sera ya diplomasi ya uchumi inakua vizuri kwa kuwa mikataba mbalimbali inaandaliwa vizuri, tunaushawishi, tunashirikiana vizuri na mashirika ya kimataifa likiwemo Shirika la Biashara Duniani (WTO) na Shirika la Fedha Duniani (IMF), na kwa sasa balozi zetu zimeelekezwa kuimarisha diplomasi ya uchumi na kuvutia uwekezeja Tanzania", Amesema Balozi Amina.


Kuhusu suala ya nchi ya Tanzania kuwa na Rais wa Awamu ya Sita, Mhe. Samia Suluhu Hassan, Balozi Amina anasema, "Hakuna sababu kwamba Tanzania isingekuwa na kiongozi mwanamke, idadi ya watu wengi nchini ni wanawake kwa takwimu zilizopo, pia nguvu kazi hii inatakiwa ihamasishwe na ipewe kipaumbele kwa vile jicho la mwananmke linavyotizama mambo si sawa na la mwanaume".

Balozi Amina anafafanua,"Wanawake wanaelewa mambo mengi kwa karibu mfano afya, elimu, ukimponya mwanamke ushaiponya jamii hata vitabu vya dini vinasema hivyo, kwa sasa tunaona mwanamke anagusa mambo ambayo hapo mwanzo hayakuwa yanasemwa lakini sasa yanasemwa".

Katika kumalizia makala hii inayoangazia mchango wa sekta hii ya diplomasia katika miaka 60 ya Uhuru, Prof. Balozi Costa Mahalu, anasema Tanzania imekuwa na misimamo isiyotetereka katika kutetea uchumi wa jumuiya za kikanda, pia imekuwa ikiheshimu misimamo ya nchi jirani.


"Mtizamo wa Tanzania haujawahi kuwa dhaifu, tulishirikiana vizuri na wenzetu na tuliwaheshimu wala hatujawahi kuingilia uhuru wa nchi yoyote. Tumekua tukishirikiana kiuchumi na kisisasa na nchi za SADC. Tanzania ina mchango mkubwa katika SADC na jumuiya zote za kikanda".

Aidha, mtazamo wa Balozi Mahalu kuhusu Tanzania kuwa na Rais mwanamke ni kwamba kimataifa inaonesha hatuna ubaguzi wa kijinsia na nchi yetu ilivyo tumeonesha katika vyeo vyenye hadhi ya kitaifa tumeendelea kuwa na viongozi wanawake mfano katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, imewahi kuongozwa na Balozi Asha Rose Migiro, tumewahi kuwa na Makamu wa Rais mwanamke ambaye sasa ndiye Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano waTanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan na ameonesha wazi kuwa anaheshimika duniani kote na Katiba yetu inasema kinaga ubaga na sisi tumeifuata, huenda ingekuwa nchi nyingine wasingeruhusu mwanamke awe Rais, lakini kwetu ni tofauti na hayo ni mafanikio makubwa sana kwa nchi yetu inapotimiza miaka 60 ya Uhuru".











Jiji la Dar es salaam, Tanzania

# Tanzania Yaendelea Kuwa Kisiwa cha Amani Ndani ya Miaka 60 ya Uhuru

Ulinzi, Amani na Usalama ni mambo muhimu na ya msingi kwa ustawi wa binadamu hususan katika kupiga hatua kimaendeleo. Hii imejidhihirisha vipi katika miaka 60 ya Uhuru, fuatana na makala hii uweze kufahamu mengi kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Na **Christina Mwangosi, MNN**

Ulinzi, Amani na Usalama ni mambo muhimu na ya msingi kwa ustawi wa binadamu hususan katika kupiga hatua kimaendeleo. Hii imejidhihirisha katika miaka 60 ya Uhuru, fuatana na makala hii uweze kufahamu mengi kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Baada ya Tanzania Bara kupata Uhuru mwaka 1961, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imepitia katika hatua kadhaa za mafanikio, ikiwemo kusimamia jukumu kubwa la kuhakikisha Nchi yetu na watu wake wanakuwa katika hali ya amani, utulivu na usalama, hivyo kuwafanya watanzania na wageni kuendelea kuishi katika hali ya amani, utulivu na usalama, huku wakiendelea na shughuli za kiuchumi na maendeleo.

## MABADILIKO YA KIMUUNDO

Mafanikio mengine ni mabadiliko ya Kimuundo kwa baadhi ya Idara zake kuwa Jeshi kamili, ambapo Kikosi cha Zimamoto kilibadilishwa na kuwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Idara ya Uhamiaji kuwa Jeshi la Uhamiaji.

## UJENZI NA UBORESHAJI WA OFISI NA MAKAZI YA MAAFISA NA ASKARI

Umefanyika uboreshaji wa Ofisi na Makazi ya Askari wa vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama vilivyoko chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ambapo kwa sasa Wizara imebadilisha mfumo wa ujenzi wa nyumba za askari kutoka nyumba za mabati na kuwa za kisasa. Kati ya mwaka 2016 hadi sasa Jeshi la Magereza limejenga nyumba 310 za kisasa zenye uwezo wa kuhudumia familia 564 kwa ajili ya makazi ya maafisa na askari. Jeshi la Polisi limejenga nyumba 10,048 za makazi ya Maafisa na Askari wake katika mikoa mbalimbali nchini.

Idara ya Uhamiaji imepatiwa nyumba 103 za makazi ya Watumishi wake katika eneo la Iyumbu jijini Dodoma na kujenga nyumba 7 katika mikoa ya Mwanza, Dar es Salaam na Ruvuma. Jeshi la Zimamoto limefanikiwa kujenga nyumba 109 kwa ajili ya makazi ya maafisa na askari katika mikoa mbalimbali nchini.

Wizara kupitia Vyombo vya Ulinzi na Usalama vilivyo chini yake, imeendelea kuboresha Ofisi zake, ambapo karibu Vyombo vyote vina ofisi katika mikoa na wilaya, ukilinganisha na hali ilivyokuwa baada ya Uhuru. Aidha, Ofisi ya Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Makao Makuu ya Jeshi la Magereza zimejengwa Dodoma. Ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya Idara ya Uhamiaji unaendelea jijini Dodoma.
Aidha, Serikali imelipatia Jeshi la Polisi Ofisi za Makao Makuu ya Jeshi hilo Dodoma. Vituo 371 vya Polisi na Vituo vya Zimamoto 78 vimejengwa nchini ukilinganisha na vituo vinne vya Kikosi cha Zimamoto vilivyokuwepo kabla ya Uhuru.

## UANZISHWAJI NA UBORESHAJI WA VYUO VYA TAALUMA NA MAFUNZO YA KIJESHI

Umefanyika upanuzi wa Shule ya Polisi Tanzania (TPS) Moshi mkoani Kilimanjaro kilichoanzishwa wakati wa ukoloni, ambapo mabweni ya kuishi wanafunzi 662 na madarasa ya wanafunzi 320 yamejengwa, ujenzi wa bweni la ghorofa nne la kuishi wanafunzi 180 na ghorofa moja lenye madarasa ya kuweza kutumiwa na wanafunzi 140, ofisi na ukumbi wa mikutano vimejengwa katika Chuo cha Taaluma ya Polisi Dar es Salaam (DPA-Chuo kilichokuwepo wakati wa ukoloni). Vyuo vilivyoanzishwa baada ya Uhuru ni Chuo cha Polisi Zanzibar, Chuo cha Polisi Kidatu na Chuo cha Polisi Wanamaji Mwanza.

> **Mwaka 2009 Dawati la Jinsia na Watoto lilizinduliwa rasmi katika Kituo cha Polisi Oysterbay Dar es Salaam, kwa niaba ya Vituo vyote vya Polisi Tanzania. Kwa sasa Madawati ya Jinsia na Watoto 420 yameanzishwa nchi nzima**

## MFUMO WA UHAMIAJI MTANDAO

Huduma za uhamiaji baada ya Uhuru zilikuwa zikitolewa kwa njia ya kuandikwa kwa mkono “manual” hali iliyosababisha ucheleweshaji wa huduma kwa wateja na kuongezeka kwa matukio ya kughushi nyaraka mbalimbali za Uhamiaji. Kuanza kutumika kwa Mfumo wa Uhamiaji Mtandao, unaounganisha mifumo yote ya utoaji huduma za kiuhamiaji kama vile Pasipoti, Visa, Vibali vya Ukaazi pamoja na Udhibiti na Usimamizi wa Mipaka kwa njia ya kielektroniki, ni mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru ambapo, hati za kusafiria 442,173 zimetolewa kwa watanzania waliopo nchini na kupitia Ofisi za Balozi zetu nje ya Nchi. Mfumo wa Uhamiaji Mtandao, umesaidia kuimarisha ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi, kudhibiti ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali na kuimarisha utoaji wa Huduma za Kiuhamiaji kwa raia wa Tanzania na wageni wanaoingia na kuishi nchini, kwa madhumuni mbalimbali.

## UJENZI WA VIWANDA

Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza, (SHIMA) limekamilisha ujenzi wa viwanda vinne (4) vya Kampuni ya Kutengeneza Bidhaa za Ngozi. Viwanda hivyo vimejengwa katika eneo la Gereza Karanga Mjini Moshi kwa gharama ya Shilingi bilioni 9.63. Aidha, kimejengwa Kiwanda cha Ushonaji cha Jeshi la Polisi Tanzania katika eneo la Kurasini Jijini Dar es Salaam.

## UANZISHWAJI WA MADAWATI YA KIJINSIA

Mwaka 2009 Dawati la Jinsia na Watoto lilizinduliwa rasmi katika Kituo cha Polisi Oysterbay Dar es Salaam, kwa niaba ya Vituo vyote vya Polisi Tanzania. Kwa sasa Madawati ya Jinsia na Watoto 420 yameanzishwa nchi nzima lengo likiwa ni kuzuia na kupambana na matukio ya ukatili wa kijinsia na unyanyasaji dhidi ya watoto.

## UANZISHWAJI WA MASHIRIKA YA UZALISHAJI MALI.

Yameanzishwa Mashirika mawili ya Uzalishaji Mali likiwemo Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza linaloendesha miradi 23, kati ya hiyo 15 ya kilimo na 8 ya viwanda. Lingine ni Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi.

## USAJILI NA UTAMBUZI WA WANANCHI.

Mwaka 2008 Serikali iliidhinisha kuanzishwa kwa chombo cha Kusimamia Vitambulisho vya Taifa kinachojulikana kama Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, kwa lengo la kutoa Vitambulisho vya Taifa kwa Watanzania waliofikia umri wa miaka 18 na wageni wanaoishi nchini. Tangu kuanzishwa kwa Mamlaka hiyo, wananchi milioni 21,823,026 wamesajiliwa kati ya lengo la kusajili watu 25,237,954. Namba za Utambulisho wa Taifa 17,871,770 zimetolewa na Vitambulisho vya Taifa 6,103,225 vimechapisha na kutolewa kwa wananchi.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, iliundwa tarehe 15 Desemba mwaka 1961, baada ya Tanganyika kupata Uhuru. Kuanzishwa kwa Wizara hii kulilenga kuunda chombo ambacho kingesimamia masuala ya Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, katika mazingira ya Nchi huru. Chombo hiki kimeiwezesha Nchi yetu kuondokana na Sera za kikoloni ambazo zilianzishwa ili kulinda maslahi ya wakoloni. Majukumu ya Wizara yalitekelezwa kwa kupitia Jeshi la Polisi na Magereza. Idara nyingine zilizokuwepo baada ya Uhuru ni Idara ya Uhamiaji na Pasipoti na Kikosi cha Zimamoto.

Baada ya Serikali ya Awamu ya Nne kuingia madarakani, Jeshi la Polisi liliondolewa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kuundiwa Wizara mpya ya Usalama wa Raia, ambayo ilipewa jukumu pekee la kutekeleza shughuli za Usalama wa Raia na Mali zao. Hata hivyo, tarehe 12 Februari 2008, Serikali ilifanya tena mabadiliko ambapo Wizara ya Usalama wa Raia iliunganishwa tena na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kuitwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Hivi sasa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ina Vyombo vya Ulinzi na Usalama vitano ikiwemo Jeshi la Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji na Uhamiaji, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na Idara na Vitengo vinginevyo.

**“ Namba za Utambulisho wa Taifa 17,871,770 zimetolewa, vitambulisho vya Taifa 6,103,225 vimechapishwa na kutolewa kwa wananchi.**





Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akihutubia Mkutano wa 41 wa (SADC) ulioanza tarehe 17 Agosti Jijini Lilongwe nchini Malawi.

# Diplomasia ya Uchumi Kichocheo cha Maendeleo Tanzania

Na **Ally Kondo – Wizara ya Mambo ya Nje**

"Tutaendelea kuwa Tanzania ile ile mliyokuwa mkiifahamu na kuiamini. Tanzania yenye amani, inayoheshimu wengine na kushirikiana na nchi zote duniani, ziwe kubwa au ndogo, zenye nguvu au dhaifu, tajiri au maskini ili kufanya ulimwengu huu ambao ni wetu sote kuwa sehemu nzuri ya kuishi".

Ni maneno yanayoonesha utamaduni na desturi ya Tanzania tokea Taifa hili liwe huru mwaka 1961 na hadi sasa linafikisha miaka 60 ya uhuru. Katika awamu sita za uongozi wa Tanzania na utekelezaji wa sera mbili za mambo ya nje, moja ikilenga kuyakomboa mataifa ya Afrika huku nyingine ikijikita kwenye diplomasia ya uchumi, hulka njema hii imeing'arisha Tanzania ulimwenguni.

Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alijenga heshima ya Tanzania ulimwenguni kutokana na kupigania uhuru wa mataifa ya Afrika, kupinga ukandamizaji unaofanywa na mataifa makubwa, na kutetea wanyonge ulimwenguni.

Sera hii ilidumu hadi muhula wa kwanza wa Rais Ali Hassan Mwinyi baada ya Afrika Kusini kukwamuliwa kutoka kwenye makucha ya ubaguzi wa rangi uliokuwa ukifanywa na makaburu wachache, kumalizika kwa vita baridi, kuibuka kwa utandawazi na mageuzi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ikiwa ni pamoja na mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2020, Tanzania ina jumla ya walinda amani 2,303 kwenye misheni sita za kulinda amani za Umoja wa Mataifa. Misheni hizo ni MINUSCA –Afrika ya Kati (455), MONUSCO – Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (969), UNAMID – Darfur, Sudan (686), UNIFIL – Lebanon (159), UNISFA – Abyei, Sudani Kusini (12) na UNIMISS – Sudani Kusini (22).

Halikadhalika, katika awamu zote za uongozi, Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika kutafuta suluhu ya migogoro mbalimbali duniani ikiwemo mgogoro wa Burundi ambapo Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius K. Nyerere alikuwa Msuluhishi wa mgogoro wa Burundi hadi wakati anafariki mwaka 1999.

Aidha, ni kwa kutambua mchango wake katika uhuru wa Burundi na baadaye katika kuleta amani nchini humo, Serikali ya Burundi ilimtunuku Tuzo ya Juu ya Taifa la Burundi (Order of the National Republic of Burundi) kwenye kilele cha maadhimisho ya miaka 50 ya Uhuru wa Burundi zilizofanyika mwaka 2012.

Aidha, itakumbukwa kuwa Hayati Benjamin William Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu aliteuliwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa mwezeshaji wa usuluhishi wa mgogoro wa Burundi nafasi aliyoitumikia hadi mwaka 2016. Aidha, Rais wa awamu ya nne, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete aliteuliwa kuwa Mjumbe wa Umoja wa Afrika katika mgogoro wa Libya ikiwa ni jitihada za kuutafutia ufumbuzi mgogoro wa nchi hiyo.

Sambasamba na hayo, Tanzania katika kuamini mtangamano, ilishiriki katika kuanzisha jumuiya za ushirikiano za kikanda kama vile Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Nchi za Afrika (SADC), PTA/COMESA na Jumuiya ya Nchi zinazopakana na Bahari ya Hindi.
Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyoundwa baada ya ile ya awali kuvunjika, imeendelea kuimarika kwa kasi na nchi wanachama wake sasa wamefikia sita kutoka watatu wa awali. Wanachama wa Jumuiya hiyo ni nchi za Tanzania, Uganda, Kenya, Rwanda, Burundi na Sudan Kusini. Kutokana na fursa zinazopatikana katika EAC, kama vile ukubwa wa soko na fursa za uwekezaji, baadhi ya nchi za jirani zimeonesha dhamira ya kutaka kujiunga na Jumuiya hiyo yenye lengo la kuunda shirikisho hapo baadaye.

## KISWAHILI DUNIANI

**UNESCO imeidhinisha Siku ya Kiswahili kuanza kuadhimishwa rasmi baada ya Bodi ya Maamuzi (Executive Board) ya Shirika hilo kuipitisha Julai 7 kila mwaka kuwa ni Siku ya Kiswahili duniani.**

SADC iliyoanza kama Klabu ya Mulungushi na baadaye Nchi za Mstari wa Mbele wa Ukombozi wa nchi za kusini mwa Afrika nayo imepiga hatua kubwa katika kuimarisha ushirikiano wa nchi wanachama katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Kwa hakika Jumuiya hii imesaidia kuimarisha biashara baina ya nchi wanachama hasa kwa kuzingatia kuwa wakati Makala hii inatayarishwa, Jumuiya hiyo ina wanachama 16 ambao ni Tanzania, Angola, Botswana, DRC, Lesotho, Madagascar, Malawi, Mauritius, Msumbiji, Namibia, Shelisheli, Afrika Kusini, Swaziland, Zambia, Comoro na Zimbabwe.

Licha ya Tanzania kushiriki katika kuasisi jumuiya hizo, lakini pia imekuwa mwenyekiti katika awamu mbalimbali wa jumuiya hizo na zile za kimataifa kwa kutoa viongozi katika nafasi za juu.

Mifano ya Viongozi wa Tanzania walioshika nafasi za juu katika Jumuiya za Kikanda na Kimataifa ni pamoja na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius K. Nyerere, ambaye alishika nafasi hiyo mwaka 1984 – 1985 na Mhe. Jakaya M. Kikwete, Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliongoza umoja huo kama Mwenyekiti mwaka 2008. Pia, Mhe. Salim A. Salim, Waziri Mkuu Mstaafu, aliongoza umoja huo kama Katibu Mkuu kwa vipindi viwili mfululizo (1989-2001) na kuuletea maboresho makubwa umoja huo ikiwemo mchakato wa kugeuza OAU kuwa Umoja wa Afrika (AU). Vile vile, Mhe. Balozi Mstaafu Getrude Mongela alichaguliwa kuwa Spika wa kwanza wa Bunge la Umoja wa Afrika mwezi Machi, 2004.

**"Tutaendelea kuwa Tanzania ile ile mliyokuwa mkiifahamu na kuiamini. Tanzania yenye amani, inayoheshimu wengine na kushirikiana na nchi zote duniani, ziwe kubwa au ndogo, zenye nguvu au dhaifu, tajiri au maskini ili kufanya ulimwengu huu ambao ni wetu sote kuwa sehemu nzuri ya kuishi"**
Rais Samia Suluhu Hassan alikieleza Kikao cha 76 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa jijini New York, Marekani Septemba 2021.

Kadhalika, katika miaka ya hivi karibuni, Watanzania wameendelea kuaminiwa na kuteuliwa katika nyadhifa za juu kikanda na kimataifa. Miongoni mwao ni Dkt. Asha-Rose Migiro, ambaye mwaka 2007 aliteuliwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja huo; Balozi Liberata Mulamula, ambaye mwaka 2006 hadi 2011 alikuwa Katibu Mtendaji wa Kwanza wa Sekretarieti ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu (ICGLR) na Dkt. Stergomena Tax ambaye ameiongoza kwa mafanikio Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kama Katibu Mtendaji wa kwanza mwanamke kuanzia mwaka 2013-2021.

Pia, Tanzania imekuwa mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kwa nyakati tofauti tangu kuanzishwa kwake ikiwemo uenyekiti kwa vipindi viwili mfululizo (mwaka 2015 na 2016); Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) mwaka 2019 na Mwenyekiti wa Jumuiya ya nchi za Afrika, Caribbean na Pasifiki (Organization of ACPS) kwa kipindi cha miezi sita kuanzia tarehe 1 Agosti 2020.

Katika kuongeza ushirikiano wa karibu na nchi mbalimbali duniani kwa lengo la kuharakisha ustawi wa maendeleo ya nchi yetu, Tanzania imeshuhudia kukua kwa ushirikiano kati yake na nchi mbalimbali duniani. Hadi sasa Tanzania inazo Balozi 44 kutoka Balozi mbili (2) zilizokuwemo kipindi cha uhuru yaani London, Uingereza na New York, Marekani katika Umoja wa Mataifa. Vilevile, Tanzania ni mwenyeji wa Balozi 62 na Mashirika ya Kimataifa 30.

Katika kuunga mkono hoja ya kudumisha utamaduni wa Afrika, Tanzania imefanikiwa kutetea lugha ya Kiswahili na kukuza matumizi ya lugha hiyo adhimu katika Jumuiya ya Kimataifa na nchi mbalimbali duniani. Inatia moyo kuwa hivi sasa lugha ya Kiswahili inatambuliwa na Umoja wa Afrika. Hatua kadhaa zinachukuliwa ili lugha hiyo ianze kutumika rasmi katika shughuli za kila siku za Taasisi hiyo. Aidha, Kiswahili ni lugha ya nne inayotumika rasmi katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).
Lengo la hatua hii ni pamoja na kutoa fursa kwa vijana wa Tanzania kuwa walimu wa lugha ya Kiswahili katika nchi mbalimbali. Kufuatia juhudi zilizofanyika katika kukuza lugha ya Kiswahili, Serikali ya Afrika Kusini imeazimia kutumia Kiswahili kama moja ya lugha itakayofundishwa kwenye shule za msingi. Vilevile, Serikali ya Jamhuri ya Botswana imetangaza azma yake ya kufundisha Lugha ya Kiswahili katika shule za msingi. Hatua hii siyo tu inaongeza sifa kwa nchi yetu bali pia inatoa fursa ya ajira kwa walimu wa Kiswahili pamoja na waandishi wa vitabu.

Aidha, tayari Hati ya Makubaliano (MoU) kuhusu namna walimu wa kufundisha Kiswahili kutoka Tanzania watakavyopelekwa nchini Burundi ilisainiwa wakati wa ziara ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyofanyika nchini Burundi mwezi Julai 2021.

Katika hatua nyingine, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa kushirikiana na Watanzania waishio nchini Misri, imefanikisha kutoa mafunzo ya lugha ya Kiswahili katika Vyuo Vikuu vya Al Azhar, Ain Shams na Cairo kwa ngazi ya Shahada na Stashahada ambapo hadi sasa kuna wahitimu wa mafunzo hayo 130 na wanafunzi 318 bado wanaendelea na mafunzo hayo.

Mbali na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika medani za kikanda na kimataifa tangu uhuru hadi sasa, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imeendelea kuchangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya Taifa hususan katika upatikanaji wa wawekezaji, watalii, fursa za biashara na masoko nje ya nchi pamoja na mikopo ya masharti nafuu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo hapa nchini ikiwemo ya afya, elimu, miundombinu, kilimo, nishati na utunzaji wa mazingira.

**Tanzania imekuwa mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kwa nyakati tofauti tangu kuanzishwa kwake ikiwemo uenyekiti kwa vipindi viwili mfululizo (mwaka 2015 na 2016); Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) mwaka 2019 na Mwenyekiti wa Jumuiya ya nchi za Afrika, Caribbean na Pasifiki (Organization of ACPS) kwa kipindi cha miezi sita kuanzia tarehe 1 Agosti 2020.**


Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan katika Mkutano wa 26 wa Umoja wa Mataifa uliyojadili athari za mabadiliko ya tabianchi (COP26) Glasgow, Scotland tarehe 01 Novemba, 2021.




# Miaka 60: Uwekezaji wa Mitaji Kutoka Nje Wafikia Bilioni 1.01

## • Vibali vya Uwekezaji Sasa Vinatolewa Ndani ya Siku Moja Hadi Tatu
## • Wawekezaji Zaidi Wajitokeza Kuweka Nchini

Na **Ibrahim Hamidu, Ofisi ya Waziri Mkuu- Uwekezaji**

> **"Kampuni binafsi 74 kutoka nje ya nchi na kampuni nne za wabia zilifika kuulizia fursa za uwekezaji na kutokana na uhamasishaji huo, TIC tayari imepokea wawekezaji wakubwa ikiwemo Kampuni ya Elsewedy yenye Mradi wa thamani ya Dola za Marekani billioni tatu, miradi mingine ni mradi wa Uzalishaji Sukari wa Kampuni ya SJ Sugar na mradi wa Kiwanda cha Mbolea ya asili wa Kampuni ya ITRA-COM FERTILIZERS LIMITED ambao unatarajiwa kuzalisha ajira 3000**
>
> Mhe. Godfrey Mwambe
> Waziri wa Viwanda

Katika kusherehekea miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara, moja ya mambo ya kujivunia ni namna Serikali ilivyofanikiwa katika kuvutia uwekezaji wa ndani na nje katika sekta mbalimbali hapa nchini.

Desemba 9 mwaka 1961, Tanzania Bara ilipata uhuru wake kutoka kwa Wakoloni wa Kiingereza kwa njia ya amani chini ya uongozi wa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere na katika kipindi chote hicho cha miaka 60 ya uhuru, Serikali za Awamu zote kuanzia Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais Mstaafu Ali Hassan Mwinyi, Rais Benjamin Mkapa (Hayati), Rais Mstaafu Jakaya Kikwete, Rais Dkt. John Pombe Magufuli (Hayati) na sasa Rais wa Awamu ya Sita, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, zimefanya jitihada kubwa za kuvutia uwekezaji, kukuza uwekezaji, maendeleo ya sekta binafsi na ushiriki wa wananchi kwenye shughuli za kiuchumi na miradi ya kimkakati.

Uwekezaji ni injini muhimu katika kukuza uchumi na kuongeza ajira na ndio maana Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan imeendelea kuhakikisha inakuwa na Wizara maalum katika Ofisi ya Waziri Mkuu inayosimamia Uwekezaji nchini.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Mhe. Geoffrey Mwambe, anasema baada ya Tanzania Bara kupata uhuru mwaka 1961, Sera za Uwekezaji zilihamasisha uwekezaji wa sekta binafsi hadi ilipofika mwaka 1967 ambapo Azimio la Arusha lilitangazwa.

Anaeleza kuwa wakati wa Azimio la Arusha, Serikali ilikuwa ikisimamia na kuendesha shughuli kuu za uzalishaji na kusababisha mvuto mdogo wa uwekezaji binafsi ikiwemo wa kutoka nje ya nchi.

Mwambe anafafanua kuwa katika kipindi hicho, shughuli za uzalishaji zilizobinafsishwa ziliendeshwa na Watanzania wenyewe na katika miaka ya mwanzoni kulikuwa na mafanikio lakini baadaye mashirika mengi yalishindwa kujiendesha kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo mapungufu ya usimamizi.

"Kutokana na matatizo ya kiuchumi yaliyotokea kati ya miaka ya 1970 hadi miaka ya 1980, Serikali iliamua kurejesha Sera zinazohamasisha uwekezaji binafsi kuanzia mwaka 1986. Maamuzi haya yalichangia ukuaji mzuri wa uchumi ambao ulifikia 4% kwa mwaka katika kipindi cha mwaka 1986-1995 ikilinganishwa na ukuaji wa 2% kwa mwaka katika kipindi cha mwaka 1981-1985," anaeleza Mwambe.




## UWIANO WA UWEKEZAJI KWA PATO LA TAIFA

Waziri Mwambe anasema tangu Serikali ianze kutekeleza Sera ya Taifa ya Uwekezaji na Sheria ya Uwekezaji Tanzania, wastani wa uwekezaji unapimwa kwa kuangalia uwiano wa uwekezaji yaani ukuzaji rasilimali kwa Pato la Taifa umekuwa ukiongezeka.

Anasema takwimu zinaonesha kuwa uwiano wa ukuzaji rasilimali kwa Pato la Taifa umekua kutoka asilimia 14.7 mwaka 1997 hadi kufikia asilimia 39.7 mwaka 2019 na kuongeza kuwa viwango hivi ni vikubwa ikilinganishwa na wastani wa nchi za Afrika wa asilimia 21 hadi 22 na nchi zilizoendelea wa asilimia 23 hadi 25.

## UWEKEZAJI KUTOKA NJE

Kuhusu uwekezaji wa mitaji kutoka nje ya nchi, Mwambe anasema uwekezaji huo umeongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 0.73 mwaka 1996 hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 2.18 mwaka 2013 na Dola za Marekani bilioni 1.01 mwaka 2020.

## MAFANIKIO YA UWEKEZAJI AWAMU YA SITA

Wakati akizindua Kampeni ya Maendeleao kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya Covid-19 jijini Dodoma hivi karibuni, Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan, amesema baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya uwekezaji tangu aingie madarakani mwezi Machi 2021 ni pamoja na kuondolewa kwa urasimu wa utoaji vibali vya kazi na uanzishwaji wa dirisha moja la kieletroniki la uwekezaji.

Ameyataja mafanikio mengine kuwa ni kuanzishwa kwa kanzi data ya ardhi, kituo cha mawasiliano cha masuala ya uwekezaji, uboreshaji wa majadiliano na sekta binafsi pamoja na kuongezeka kwa usajili wa miradi ya uwekezaji. Kuhusu kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara, amesema Serikali yake imefanikiwa kuondoa urasimu wa utoaji wa vibali vya kazi kwa kuanzisha mfumo wa kieletroniki ambao umepunguza muda wa kutoa vibali kutoka zaidi ya siku 14 za awali hadi siku moja au tatu kwa sasa ikiwa mwombaji ametimiza taratibu zote.

Hatua zingine ambazo Serikali yake imezichukua ni kukamilisha dirisha moja la kieletroniki la uwekezaji, kituo cha mawasiliano cha masuala ya uwekezaji, kanzidata ya ardhi yenye ukubwa wa hekta milioni 1.6, uimarishaji wa majadiliano na Sekta Binafsi kwa kufanya mkutano wa Baraza la Taifa la Biashara.

"Kutokana na hatua hizi, miradi yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 3.5 imesajiliwa ambayo inatarajiwa kuzalisha ajira 43,782 na itasaidia kupunguza tatizo la ajira nchini. Miradi 164 yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 3,158 imesajiliwa na TIC na miradi 18 imeasajiliwa na Mamlaka ya Ukanda Maalumu wa Uwekezaji Tanzani (EPZA)," anasema Mhe. Rais Samia.

Aidha, Mheshimiwa Rais Samia aliongoza timu ya kurekodi Filamu ya Royal Tour na anaeleza kuwa filamu hiyo ikikamilika na kutangazwa, itawezesha kutangaza vivutio vya utalii na uwekezaji hapa nchini na kufanya uwekezaji kuendelea kukua.

## KUENDELEA KUVUTIA UWEKEZAJI

Kuhusu kuendelea kuvutia uwekezaji wa ndani na nje, Mwambe anasema TIC imeendelea kuhamasisha uwekezaji wa ndani na nje na kuifanya Tanzania kuendelea kupokea wawekezaji huku serikali ikiboresha mazingira ya uwekezaji na ujenzi wa miundombinu wezeshi kama barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege na umeme.

Anasema Serikali inaendelea kuhamasisha uwekezaji wa ndani ambapo kuanzia mwezi Machi hadi Agosti mwaka huu, wawekezaji wa ndani 92 wametembelea TIC kutafuta fursa na pia TIC imepokea jumbe za uwekezaji kutoka nchi za Uholanzi, Namibia, Nigeria, Misri, Poland, China, Uturuki, India, Oman, Marekani, Hong Kong, Afrika Kusini, Canada na Saudi.

Serikali inaendelea kuchukua hatua nyingine za kuandaa, kusimamia na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji ikiwemo Sheria, Kanuni na Maelekezo yote yanayohusu uwekezaji ili kuhakikisha kuwa vikwazo vyote katika uwekezaji vinatambulika na kuondolewa pamoja na kuwa na mazingira rafiki na sawa katika uwekezaji.

"**Kwa sasa changamoto za kuchaji simu hazipo tena tunaishukuru Serikali yetu kwa hatua hii kubwa ya kutufikishia umeme,sasa tutanunua majokofu na kupikia kwa kutumia umeme"**



# Matumizi ya Koroboi Yapungua kwa Zaidi ya 80%

Na **Daudi Manongi**

Ni miaka sitini tangu Tanzania Bara ipate uhuru, katika kipindi hiki, kama nchi tumepiga hatua kubwa kimaendeleo katika nyanja zote.
Mwaka 1961 wakati Tanzania inapata Uhuru tulikuwa na mikoa miwili tu ya Tanga na Dar es Salaam yenye umeme jambo ambalo lilifanya nchi yetu kuwa nyuma kimaendeleo.

Shughuli mbalimbali za kilimo, masuala ya afya pamoja na shughuli zote za kusaidia kuinua nchi kiuchumi zilidorora kwa sababu nishati ya umeme haikuwepo na hivyo kusababisha masuala haya kutokusonga mbele.

Katika kipindi hiki cha kupata uhuru nchi yetu ilikuwa na megawati 54 za umeme peke yake. Ili kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na umeme wa kutosha baada ya Uhuru, lilianzishwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mwaka 1964 ambalo lilitokana na kuunganishwa kwa mashirika binafsi mawili ya Tanganyika Electric Supply Company Limited (TANESCO) na Dar es Salaam and District Electric Supply Company Limited (DARESCO) chini...

...ya Sheria ya umeme ya mwaka 1931 iliyorekebishwa mwaka 1957 (Electricity Ordnance Cap 131 of 1931, na maboresho ya mwaka 1957).
Baada ya kuanzishwa kwa Shirika la TANESCO ikawekwa mikakati na ikaanzishwa miradi mipya ambayo imepelekea Tanzania kuwa na ongezeko la miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme ambapo ndani ya miaka 60 ya Uhuru imefikisha kilometa 6,110.57 za usafirishaji umeme.

Na katika kuhalalisha hilo, Spika Mstaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Pius Msekwa anabainisha kuwa,
"Kabla ya Uhuru sisi Ukerewe hatukuwa na umeme kabisa, tulikuwa tunategemea koroboi, koroboi ndo ulikuwa mwanga wetu wa nyumbani wakati wa usiku na tumekaa kwa muda mrefu mpaka utawala wa Rais wa Awamu ya Tatu, Hayati Benjamini William Mkapa mwaka 2005, sasahivi teknolojia imekua umeme unapitishwa chini ya maji, yote hayo ni maendeleo ya kujivunia na kuwashukuru viongozi wetu kwa maono", anasema Msekwa.

> "
> **Tunashukuru kwa kweli kwa kutuletea umeme maana watoto wetu sasa watasoma kwa raha sasa nafikiria kuweka mashine ya kusaga,tutapata taarifa za habari kwa ukaribu**

Katika upande mwingine Mfanyabiashara wa mahindi kutoka kijiji cha Nasuro mkoani Kilimanjaro amesema kuwa kwa sasa hali ni nzuri ukitofautisha na hapo nyuma wakati hawana umeme.

"Kwa kweli kwa sasa changamoto za kuchaji simu hazipo tena tunaishukuru Serikali yetu kwa hatua hii kubwa ya kutufikishia umeme, sasa tutanunua majokofu na kupika kwa kutumia umeme" ameongeza.


Naye mkazi wa Kijiji cha Nasuro, Bi Elizabeth Mndeme amesema kuwa miaka ya nyuma wamekuwa wakipata...

...tabu sana kwa kutokuwa na umeme lakini kwa sasa maendeleo yanakuja kwa kasi.

"Tunashukuru kwa kweli kwa kutuletea umeme maana watoto wetu sasa watasoma kwa raha sasa nafikiria kuweka mashine ya kusaga,-tutapata taarifa za habari kwa ukaribu", amesema.

Manufaa mengine yaliyopatikana ndani ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara ni kutokana na ugunduzi wa Gesi Asilia na TPDC kuunganisha wateja wa Gesi asilia kwenye mtandao wa miundombinu ya usambazaji yenye jumla ya kilomita 130 iliyotandazwa mikoa ya Dar es Salaam Pwani na Mtwara.
Bi. Pendo Kisaka Mkazi wa Ubungo anasema toka amefungiwa gesi asilia nyumbani kwake imemrahisishia mambo mengi.

Kwa upande Bw. Ernest Kashua amesema kwa miaka mingi wamekuwa wanatumia mkaa, kuni na umeme lakini tangu aunganishiwe gesi nyumbani kwake amepunguza safari za kununua gesi mbali na mtumizi ya mkaa na umeme.



Barabara za Juu za Ubungo (Ubungo Interchange), Dar es salaam

# Historia Yaandikwa Maendeleo ya Watanzania

Na **Ahmed Sagaff – MAELEZO**

Kamusi ya Baraza la Kiswahili la Tanzania inalitafsiri neno "Jamii" kama jumla ya watu waliokusanyika pamoja. Umoja wa Mataifa unakitafsiri kifungu cha maneno "Maendeleo ya Jamii" kama Mchakato wa wanajamii kukusanyika pamoja kwa ajili ya kupata suluhisho la matatizo yanayowakabili.

Hiyo inamaanisha kwamba Idara ya Maendeleo ya Jamii iliyopo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kwa maneno yasiyo rasmi tunaweza kuiita Idara ya Maendeleo ya Watu.

Kwa mujibu wa taarifa ya mafanikio ya miaka 60 ya uhuru iliyotolewa na Idara ya Maendeleo ya Jamii, mara baada ya uhuru wa Desemba 1961, kampeni mbalimbali za kitaifa zimeanzishwa kwa lengo la kuwahamasisha wanajamii kujiletea maendeleo.

Baadhi ya kampeni hizo ni "uhuru na kazi", "kisomo chenye manufaa", "mtu ni afya", "chanjo ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano", ujenzi wa nyumba bora" na "nyumba ni choo". Pia Serikali zikaanzisha vyuo vinavyotoa kozi ya maendeleo ya jamii ili kupata watumishi watakaoiendeleza jamii ya Watanzania.

Miongoni mwa kazi zilizofanywa ndani ya miongo sita ya uhuru ni kujenga mazingira ili jamii ya Watanzania iwe na watu wanaoishi maisha marefu kwa kudhibiti maradhi, kuwawezesha kuwa na makazi ya heshima, kuwaonesha njia ya kuinua vipato vyao na kulinda haki za makundi maalum wakiwamo watoto, wazee na wanawake.

Mafanikio yameonekana katika kampeni mbalimbali. Mathalan, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, wataalamu wa maendeleo ya jamii wamewezesha kaya 617,100 kuboresha vyoo, kaya 305,724 kuboresha maeneo ya kunawa mikono, kujengwa madarasa ya shule za msingi 6,521 na 2,499 ya sekondari, hospitali 67 za Halmashauri na miradi mingine vijijini na mijini.

"Hadi sasa vimeanzishwa vituo tisa vya ubunifu wa kidigitali na programu za ushirikiswaji jamii kutatua changamoto zinazowakabili kwa kutumia rasilimali zinazowazunguka zimeanzishwa," inahabarisha sehemu ya taarifa hiyo.

Juhudi za kuimarisha ustawi wa watoto nchini ulianza kwa kuweka haki za mtoto kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, pamoja na kuridhia na kusaini mikataba ya kikanda na kimataifa ukiwamo Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (1989) na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (1990) sambamba na kutungwa kwa sheria na sera zinazomlinda mtoto.

Pamoja na hilo, baadhi ya juhudi nyingine zilizochukuliwa kwa ajili ya kustawisha hali za watoto nchini ni kuanzisha majukwaa ya watoto yanayowapa stadi za maisha na ujuzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kuanzishwa program jumuishi ya kitaifa ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto na huduma za malezi na matunzo kwa watoto walio katika mazingira hatarishi.

Kwa upande wa wazee, serikali imeanzisha na kuimarisha vituo vya kutunza wazee ambapo zaidi ya wazee 600 wanatunzwa, imeimarisha ushiriki wa wazee kwenye masuala ya maendeleo ya kijamii, imeunda mabaraza 20,748 ya wazee na kuboresha mifumo ya utoaji huduma za afya kwa wazee.

Aidha, serikali imeendelea kuwawezesha wanawake kisiasa ambapo sasa kuna jumla ya wabunge wanawake 145, kuwainua kiuchumi kwa kuwapa mikopo ya halmashauri na katika vikundi vya VICOBA na Benki ya Wanawake, kupambana na kuzuia vitendo vya ukatili wa wanawake.

Sambamba na hayo, Serikali imesajili mashirika yasiyo ya kiserikali yapatayo 11,731 ambayo yanachangia kuleta maendeleo kwa kutoa huduma za kijamii ikiwemo huduma za jamii ikiwemo afya, elimu, kilimo, maji, mazingira, haki zabinadamu, jinsia na utawala bora.

Serikali ya Awamu ya Sita imeimarisha uhusiano na mashirika yasiyo ya kiserikali ambapo Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan akihutubia Mkutano wa Mashirika hayo hivi karibuni jijini Dodoma, aliahidi ushirikiano wa hali ya juu ili KAZI IENDELEE.

# Tanzania ya Miaka 60, Ndoto ya Mwalimu Nyerere



Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.



Rais wa Awamu ya Pili
Mhe. Ali Hassan Mwinyi

Na **Judith Mhina- MAELEZO**

Tanzania inatimiza miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara (Tanganyika) ambao ulipatikana tarehe 09 Desemba mwaka 1961.

Hakika kuna kila sababu ya kujivunia miaka 60 ya Uhuru, ni safari ndefu ambayo unapoitaja tu unaona alama za ushindi kwa Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Tanganyika na baadaye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Mungu amlaze mahala pema peponi.

Tanzania imekuwa na safari ndefu sana ya mapambano hadi kufikia mafanikio mbalimbali yaliyopo katika Jamii ya Watanzania kwenye nyanja ya elimu, afya, maji, umeme, barabara, usafiri wa barabara, anga na majini, ambao umeleta ustawi wa jamii ya Mtanzania. Yote hayo yamesimamiwa na kuelekezwa kwa weledi na Mwalimu Nyerere aliyeipokea nchi ya Tanganyika ikiwa iko nyuma sana kimaendeleo kutokana na kutokuwa na huduma za msingi za jamii zinazotosheleza kwa makusudi, wakoloni hao waliendeleza sera yao ya "Uwagawe Uwatawale" (Divide and Rule).

Siku ile ya Uhuru katika uwanja wa Uhuru jijini Dar es salaam, Mwalimu Nyerere alisema 'Uhuru Wananchi!' watu waliitikia 'Kazi ya TANU!' (Tanganyika African National Union) Nitawaita Waingereza miaka kumi ijayo wafike waone maendeleo ambayo Watanganyika watakuwa wameyafikia ikilinganishwa na wao wametawala miaka 40 bila kuacha maendeleo na ustawi wa jamii ya kila mwananchi wa Tanganyika".

**Pamoja na kupata Uhuru Mwalimu Nyerere alihakikisha ustawi wa Jamii ya Watanzania unafikiwa**

Pamoja na kupata Uhuru Mwalimu Nyerere alihakikisha ustawi wa Jamii ya Watanzania unafikiwa na leo hii mwaka 2021 dhamira na kiu ya Baba wa Taifa imetimia kwa kuonyesha ni jinsi gani Watanzania wamepambana kuhakikisha ustawi wao wa jamii unatimia kama alivyokusudia. Ipo sababu aliyoiahidi Baba wa Taifa kwamba waliotutawala waje waangalie maendeleo yetu.

Suala la elimu wakati wa ukoloni, wageni wa kwanza Tanzania Bara walikuwa Wareno, wakifuatiwa Waarabu na Wajerumani na Waingereza. Kwa kuwa wageni hao walipokezana madaraka ya sehemu ya nchi au nchi nzima, kila kundi lilibadili mfumo wa elimu kulingana na matakwa yao bila kujali yale yaliyokuwa na manufaa kwa Watanzania Bara. Sera yao ilikuwa moja ya "wagawe uwatawale" watoto walipewa elimu kwa kugawanywa katika makundi mbalimbali makabila yao, dini zao, na rangi zao. Shule za mataifa mbalimbali zilitofautiana katika malengo, mitaala, sifa na taaluma za walimu, lugha ya kufundishia, na ubora wa majengo ya shule na nyumba za walimu pia zilikuwa tofauti.

**Siku ile ya Uhuru katika Uwanja wa Uhuru, Mwalimu Nyerere alisema "Uhuru Wananchi!" watu wakaitika "Kazi ya TANU!"**

Historia inatuambia, Waarabu walipoingia walianzisha mafunzo ya Quran. Elimu hii ilitia mkazo uenezi wa dini ya Kiislamu na Utamaduni wa Kiarabu. Utawala wa Kijerumani na Kiingereza ulitanguliwa na ujio wa Wamisionari. Walipofika, Wamisionari walitoa elimu kufuatana na imani yao na historia ya nchi walikotoka. Elimu ya Wamisionari ilisisitiza uenezi wa dini ya Kikristo. Utawala wa Kijerumani ulitoa elimu iliyotilia mkazo stadi, maarifa na mafunzo ya kazi na uraia mwema na utii kwa Serikali ya Ujerumani.

Aidha, mfumo wa elimu ya Waingereza Tanzania Bara ulikuwa na misingi ya ubaguzi wa rangi na ulitoa nafasi na nyenzo bora zaidi za elimu kwa watoto wa Kizungu na Kiasia kuliko Waafrika. Lengo kubwa la elimu lilikuwa ni kupata watumishi Waafrika ambao wangetumika katika kutetea matakwa ya wakoloni, na hivyo kuwafanya wasomi kuwa tegemezi. Wakoloni walipoondoka Tanganyika kulikuwa na shule za msingi zipatazo 3000 zenye wanafunzi 486,000 tu.





Rais wa Awamu ya Sita
Mhe. Samia Suluhu Hassan

**Pamoja na kupata Uhuru Mwalimu Nyerere alihakikisha ustawi wa Jamii ya Watanzania unafikiwa na leo hii mwaka 2021 dhamira na kiu ya Baba wa Taifa imetimia kwa kuonyesha ni jinsi gani Watanzania wamepambana kuhakikisha ustawi wao wa jamii unatimia kama alivyokusudia.**



**Rais wa Awamu ya Tatu**
**Hayati Benjamin William Mkapa**



**Rais wa Awamu ya Nnne**
**Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete**



**Rais wa Awamu ya Tano**
**Hayati Dkt. John Pombe Magufuli**

Mara baada ya uhuru wa Tanganyika Hayati Mwalimu Nyerere aliliona pengo la elimu la sera za kikoloni "uwagawe uwatawale" kutokana na ubaguzi wa utoaji elimu hiyo maana wasomi wa enzi hizo wakaanza kuiga mifumo ya ukoloni na kujiona wao ni tofauti na wananchi wa kawaida. Mwalimu Nyerere alikuja na suluhisho "Azimio la Arusha na elimu ya kujitegemea" ikizingatia kufuta "Ujinga, Maradhi na Umaskini" ambapo alijua msingi wake ni elimu, afya bora na huduma bora za jamii.

Mwalimu Nyerere alitaifisha shule zote zilizokuwa na mrengo wa ubaguzi wa rangi, ukabila, udini na kuzifanya za Serikali ambapo iliamriwa watoto wote kupata elimu ambayo ilitolewa bure tangu darasa la kwanza hadi Chuo Kikuu. Mwaka 1961 Tanganyika ilikuwa na shule za msingi na sekondari 3,000 zenye wanafunzi 486,000 na Chuo Kikuu kimoja cha Dar-es-salaam.

Kwa mujibu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa sasa Tanzania Bara Shule za Msingi zipo 18,152 ambapo za Serikali ni 16,406 za binafsi ni 1,746 zenye idadi ya wanafunzi 10,460,785 shule za sekondari zipo 5,143 zenye idadi ya wanafunzi 2,338,457. Shule za Serikali ni 3,863 zenye wanafunzi kidato cha kwanza hadi cha nne ni 1,914,735, na shule za binafsi zipo 1,280 zina wanafunzi 5,143 na kidato cha tano na cha sita wanafunzi 151,247 shule za Serikali 109,540 za binafsi 41,707, kwa sasa vyuo vikuu ni 47 kutoka chuo kikuu kimoja wakati wa uhuru.

Wakati wa Ukoloni kwa upande wa huduma za afya zilikuwa duni, na hazikutosheleza mahitaji na zilikua za kibaguzi zinazozingatia malipo na madaraja (grade A, B na C )...

...Wazungu, Wahindi, Waarabu, Waafrika, ambapo wananchi wa kawaida hawakuweza kuyamudu. Ukoloni haukutoa umuhimu stahiki kwa sekta ya afya kwa Waafrika. Watu wengi waliishi kwa kutegemea miti shamba na waganga wa asili.

Wakoloni walipoondoka kulikuwa na jumla ya hospitali 98 tu kwa idadi ya watu milioni tisa (9,000) mwaka 1961. Mpaka kufikia Aprili mwaka 2021, Vituo vya Afya 8,458 Serikali inamiliki vituo 6,225 sawa na asilimia 73.6; mashirika ya dini yanamiliki vituo 917 sawa na asilimia 10.8 na Mashirika mengine na watu binafsi wanamiliki vituo 1,316 sawa na asilimia 15.6. Kati ya vituo 8,458 vilivyopo nchini, hospitali ni 369, vituo vya afya ni 926 na zahanati 51 7,163.


Eneo la Bandari ya Dar es salaam

# Uhuru Ulivyoimarisha Miundombinu ya Usafiri

Na **Ahmed Sagaff - MAELEZO**

Uwekezaji katika miundombinu ya usafiri huchochea ustawi wa taifa lolote ulimwenguni. Umoja wa Mataifa (UN) unasema kuwa miundombinu ya usafiri kwenye eneo lenye uchumi wa chini husababisha mabadiliko makubwa sana katika upatikanaji elimu, kazi na huduma za kijamii.

Pia, UN imeeleza kuwa miundombinu hiyo huyawezesha maeneo yaliyo kwenye uchumi wa kati kufikia uchumi wa juu maana hurahisisha biashara ya ndani na nje ya nchi. Swadakta, jitihada zilizofanywa ndani ya miaka 60 ya uhuru wa Tanzania Bara, zimeinua uchumi wa ardhi hiyo iliyopo Afrika Mashariki.

Tanzania Bara ilipata uhuru mnamo 1961 ikiwa na miundombinu dhaifu ya usafiri licha ya wakoloni kulitawala eneo hilo kwa zaidi ya miongo saba. Watu waliokuwa wakisafiri kutoka Dar es Salaam kuelekea Bukoba walilazimika kupita kwenye nchi za Kenya na Uganda maana hakukuwa na barabara iliyowezesha safari hiyo iliyokuwa ikichukua zaidi ya siku mbili njiani.

> **Mtandao wa barabara za lami umefikia kilometa 11,186 mnamo Septemba 2021 ukilinganisha na kilometa 1,360 zilizokwepo mwaka 1961.**

Baada ya uhuru, Marais walioiongoza ardhi hiyo wamefanya jitihada za kizalendo za kuhakikisha watu na mizigo yao wakisafiri kwa urahisi.

Miundombinu ya usafiri iliyoimarishwa katika miongo sita huenda ni moja ya mambo yaliyoifanya himaya hiyo kutangazwa na Benki ya Dunia kuwa imeingia kwenye uchumi wa kati mnamo 2020.

Mnamo Novemba 12, 2021, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa akiwa jijini Dodoma, alizungumza na watanzania kupitia vyombo vya habari ambapo alielezea hali ilivyokuwa mwaka 1961 huku akionesha mafanikio yaliyofikiwa mnamo 2021 kati sekta anazozisimamia.

Waziri Mbarawa anafahamisha kwamba mtandao wa barabara za lami umefikia kilometa 11,186 mnamo Septemba 2021 ukilinganisha na kilometa 1,360 zilizokwepo mwaka 1961. Barabara hizo zinajumuisha madaraja ya aina mbalimbali na mizani 64 ya kupima uzito wa magari na mfumo wa kamera za kisasa za CCTV zilizofungwa kwenye mizani 13.

Si barabara tu, mnamo 1961, mtandao wa reli ulikuwa na urefu wa kilometa 2,068. Punde baada ya uhuru, Serikali ikajenga kilometa 639 za reli ya kati, kilomita 1,860 za reli ya Uhuru (TAZARA) na sasa inajenga kilomita 1,219 za reli ya kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza. Usafiri wa SGR utaanza Desemba mwaka huu kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro.

Vilevile, usafiri wa majini (maziwani na baharini) umeimarika ukilinganisha na miaka 60 iliyopita. Prof. Mbarawa anasema kuwa baada ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ya 1977, Tanzania ilikabidhiwa bandari mbili tu za Dar es Salaam na Tanga hivi sasa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) inasimamia bandari rasmi 89 huku kwa ujumla kukiwa na bandari 693. Shehena zinazopita kwenye bandari za TPA zimeongezeka kutoka 1,185,000 mwaka 1961 hadi 17,716,429 katika mwaka wa fedha 2020/2021.

Amesema maendeleo hayo yanatokana na mabadiliko ya kimuundo, kisheria na kiutendaji pamoja na kuongeza kina cha gati katika bandari mbalimbali sambamba na ujenzi wa gati za kisasa zenye uwezo wa kuchukua meli kubwa zenye kubeba mizigo mikubwa. Aidha, Serikali inamiliki vivuko 33 katika maeneo 22 na boti 10 zinazotoa huduma wakati wa dharura.

Aidha, usafiri wa anga umeimarika ukilinganisha na miongo sita iliyopita. Idadi ya ndege zinazomilikiwa na Serikali zimeongezeka kutoka tatu mwaka 1977 hadi ndege 12 za kisasa zinazotoa huduma ndani na nje ya nchi mnamo 2021 huku mipango iliyopo ikiwa ni kufikisha ndege 17 mwaka 2023.

"Hadi sasa Serikali ina jumla ya Viwanja vya Ndege 58 vilivyo chini ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) na kimoja kilicho chini ya KADCO huko Kilimanjaro," amefahamisha Mhe. Mbarawa.

Sanjari na hayo, Serikali inamiliki mitambo minne ya rada zenye teknolojia ya kisasa za kuongozea ndege za kiraia. Rada hizo zimefungwa kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mwanza na Mbeya. Kabla ya ununuzi wa rada hizi mwaka 2019, ndege zilizopita kwenye anga la Tanzania, ziliongozwa na rada za Kenya.

Fauka ya hayo, Tanzania Bara wakati inapata uhuru ilikuwa na vituo viwili vya rada za hali ya hewa Dar es Salaam na Uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA). Lakini rada hizo za kizamani hazitumiki tena. Mwaka 2021, Tanzania ina jumla ya rada tatu za kisasa zaidi zilizofungwa Dar es Salaam, Mwanza na Mtwara huku malipo ya ununuzi wa rada nne yakiwa yameshafanyika.

Jambo lingine ambalo Tanzania inajivunia ni kuongezeka kwa idadi ya wahandisi wazawa kutoka wawili waliokwepo mwaka 1961 hadi wahandisi 32,145 mwaka 2021 waliosajiliwa sambamba na uwepo wa makandarasi wazawa 11,916 ukilinganisha na makandarasi wa nje 466 waliosajiliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) iliyoanzishwa mwaka 2002.

Ongezeko la wahandisi limechochewa na uwepo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu Ardhi vinavyotoa kozi za uhandisi. Aidha, uwepo wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) umeisaidia Tanzania Bara kuwa na wataalamu mbalimbali katika sekta ya usafirishaji.

Serikali, kupitia Mfuko wa Kusaidia Makandarasi wa ndani (CAF), imekuwa ikiwasiadia makandarasi wa ndani wadogo na wa kati kupata dhamana katika mabenki bila rehani ya kitu chochcote ambapo kuanzia mwaka 2015 hadi 2020 Makandarasi 1,168 wamenufaika na huduma za mfuko huo.

Uhuru wa Tanzania umeleta neema kwenye sekta ya usafiri, sio tu ndani ya eneo hilo bali hata katika baadhi ya mataifa ya Afrika ya Kati na yale ya Kusini mwa Afrika yasiyokuwa na bahari kwani hutegemea Bandari ya Dar es Salaam ili kusafirisha mizigo yao kwenda na kutoka ughaibuni.

**Serikali ina jumla ya Viwanja vya Ndege 58 vilivyo chini ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) na kimoja kilicho chini ya KADCO huko Kilimanjaro**

Ndege ya Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL)



**Viwanda na Biashara**

Moja ya mafanikio makubwa katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru ni kukua kwa mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa hadi kufikia asilimia 8.4 kwa mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 1961 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 4.9. Pamoja na athari za janga la UVIKO-19, Sekta ya Viwanda imeongeza ajira hadi 482,601 mwaka 2020 ukilinganisha na ajira asilimia tisa ya ajira zote katika kipindi hicho cha mwaka 1961.



# Miaka 60 ya Uhuru: Viwanda Vyaongeza Ajira 482,601 Mwaka 2020

Na **Wizara ya Viwanda na Biashara**

**Serikali imefanikiwa kupata thamani ya mitaji ya uwekezaji iliyosajiliwa chini ya EPZA ambayo ni Dola za Marekani Bilioni 2,539, ajira mpya za moja kwa moja 63,159 na thamani ya mauzo ya bidhaa za nje ya nchi ambazo ni Dola za Marekani Bilioni 2,443. Serikali imeandaa Mwongozo wa Uwekezaji katika Mitaa ya Viwanda (Industrial Parks) nchini**


Muonekano wa juu wa kiwanda cha saruji cha Twiga, ambapo Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alizindua kinu namba 2 cha saruji cha Kampuni hiyo, eneo la Wazo, Tegeta jijini Dar es salaam, Novemba 16, 2021 (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu)

Ni dhahiri kuwa sekta ya viwanda na biashara ina mchango mkubwa katika ujenzi wa uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Sekta ya viwanda inachochea uchumi shindani na shirikishi na kuimarisha ukuaji wa uzalishaji wa ndani na utoaji huduma, kukuza uwekezaji na biashara.

Hivyo, sekta hii ni kiungo muhimu katika kuchochea na kuhamasisha maendeleo ya sekta wezeshi na tegemezi katika ujenzi wa uchumi shindani na viwanda zikiwemo kilimo, uvuvi, mifugo, misitu na madini kwa uzalishaji wa malighafi za viwanda na miundombinu ya barabara, reli, usafiri wa anga, nishati, mawasiliano na maji. Aidha, uchumi shindani na viwanda unahitaji rasilimali watu ambayo ni muhimu katika mnyororo mzima kuanzia uzalishaji malighafi, uzalishaji wa bidhaa viwandani na usambazaji wa bidhaa hadi mikononi mwa walaji.

Katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru, Wizara na Taasisi zake 14 (EPZA, NDC, TIRDO, CAMARTEC, TEMDO, TANTRADE, FCC, FCT, BRELA, WMA, TBS, WRRB, CBE na SIDO imepata mafanikio makubwa katika ujenzi wa uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu kwa kuzingatia miongozo mbali mbali inayotolewa ikiwa ni pamoja na Dira ya Taifa ya 2025, Agenda ya Dunia ya Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; Agenda ya Maendeleo ya Bara la Afrika Tuitakayo, 2063, Ilani za Uchaguzi za CCM katika vipindi mbali mbali vya uchaguzi ndani ya mfumo wa chama kimoja na vyama vingi, MKUKUTA I & II (2000 – 2010) na Mipango ya Taifa ya Maendeleo ya Miaka Mitano katika vipindi vitatu (2011 – 2026).

Moja ya mafanikio makubwa katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru ni kukua kwa mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa hadi kufikia asilimia 8.4 kwa mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 1961 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 4.9. Pamoja na athari za janga la UVIKO-19, Sekta ya Viwanda imeongeza ajira hadi 482,601 mwaka 2020 ukilinganisha na ajira asilimia tisa ya ajira zote katika kipindi hicho cha mwaka 1961. Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo imechangia asilimia 35 katika Pato la Taifa na imeajiri zaidi ya Watanzania milioni nane, ikiwa ni ya pili katika sekta za kiuchumi katika kutoa ajira ikifuatia Sekta ya Kilimo kwa mwaka 2020. Vilevile, Sekta ya Biashara imechangia asilimia 8.7 katika Pato la Taifa kwa mwaka 2020.

Kwa upande wa sekta ya viwanda, Serikali imepata mafanikio katika nyanja mbalimbali. Moja ya mafanikio hayo ni ongezeko la uzalishaji wa bidhaa mbali mbali zikiwemo vifaa vya ujenzi (saruji, marumaru, nondo, mabati, vyuma, misumari, na vifaa vya umeme), bidhaa za plastiki na magodoro, nguo, chakula na vinywaji, chokaa, vioo, vifungashio, beteri za magari, na vitakasa mikono (ethanol) ambapo mwanzoni zilikuwa zinaagizwa kutoka nje ya nchi. Aidha, Serikali inaendelea kufanya jitihada mbalimbali katika kuhakikisha uzalishaji wa mbolea, dawa na vifaa tiba, mafuta ya kula na sukari unajitoshereza nchini na kupunguza uagizaji wa bidhaa hizo kutoka nje ya nchi.





Waziri Mkuu Kassim Majaliwa katika uzinduzi rasmi wa kinu namba 2 cha saruji cha Kampuni ya Twiga Cement, kilichopo eneo la Wazo, Tegeta jijini Dar es salaam, Novemba 16, 2021 (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu)

Kutokana na uanzishaji na uendelezaji wa viwanda katika maeneo ya EPZ/SEZ. Serikali imefanikiwa kupata Thamani ya Mitaji ya uwekezaji iliyosajiliwa chini ya EPZA ambayo ni Dola za Marekani bilioni 2,539, ajira mpya za moja kwa moja 63,159 na thamani ya mauzo ya bidhaa za nje ya nchi ni Dola za Marekani bilioni 2,443. Serikali imeandaa Mwongozo wa Uwekezaji katika Mitaa ya Viwanda (Industrial Parks) nchini ambao utatoa taswira na mwongozo kwa taasisi zinazohusika ili kurahisisha hatua za kuwekeza katika Mitaa ya Viwanda. Serikali imefanikiwa kutenga maeneo matano kwa ajili ya kuanza ujenzi wa mitaa ya viwanda katika mikoa ya Dar es salaam, Tanga, Arusha, Kilimanjaro na Mwanza. Aidha, Serikali ya Awamu ya Sita imetoa ridhaa ya kuendelea na majadiliano na wawekezaji ili kuendeleza eneo maalum la uwekezaji lililopo Bagamoyo ili kuvutia wawekezaji na kuendeleza eneo la Kurasini Logistics Centre lililopo Dar es Salaam ambapo kiasi cha shilingi bilioni 30 kimetolewa kwa ajili ya mradi huo.

Serikali imefanikiwa kuchochea uanzishwaji wa shughuli za kiuchumi kwa kutoa mafunzo na kutumia mikopo inayotolewa na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) chini ya Programu ya SANVN inayojumuisha taasisi za SIDO, VETA, AZANIA BANK, NSSF na NEEC na Mfuko wa Wafanyabiashara na Wananchi (NEDF) ambao hadi mwaka 2020 una shilingi bilioni 8.65 zinazotolewa kwa wajasiriamali. Vile vile, Serikali imekamilisha ujenzi wa majengo viwanda 11 (industrial sheds) na kukarabati jengo kiwanda moja (industrial shed) kwenye maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya mafunzo na uzalishaji wa bidhaa mbalimbali. Majengo hayo yamejengwa katika mikoa ya Kagera (1), Geita (4), Dodoma (3), Manyara (3) na Mtwara (1).



Kwa upande wa Sekta ya Biashara, Serikali iliandaa Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Mazingira ya Biashara nchini (Blue Print for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment for Tanzania). Mpango huo umewezesha maboresho ya tozo 233 ambapo kati ya tozo hizo, tozo 163 zimefutwa na tozo kero 10 zimepunguzwa kiwango. Kati ya tozo zilizofutwa, 114 ni za Sekta ya Kilimo na Mifugo, tano za OSHA, 44 za TBS, GCLA, Utalii, Maji, Uvuvi na iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa-TFDA. Mpango huo umewezesha kuhamisha jukumu la usimamizi wa masuala ya chakula kutoka iliyokuwa TFDA kwenda TBS, ili kuondoa muingiliano wa majukumu. Maboresho hayo yamesaidia kuondoa urasimu na kupunguza gharama za kufanya biashara. Aidha, Tozo 60 zilizokuwa zinatozwa na Wizara, Idara na Taasisi zinazojitegemea zimefutwa.

Serikali pia imefanikiwa kuboresha Vituo tisa vya Pamoja vya Mipakani (One Stop Border Posts - OSBP) kwa kuweka mifumo na kukamilisha ujenzi ili kurahisisha shughuli za Taasisi za usimamizi mipakani kutekeleza majukumu yao kwa pamoja kwa ufanisi, gharama nafuu na muda mfupi kwa kuwarahisishia wafanyabiashara, magari na bidhaa kukaguliwa mara moja wakati wa kuingia au kutoka katika mpaka wa nchi. Vituo hivyo ni pamoja na Holili/Taveta, Namanga/Namanga, Sirari/Isebania Horohoro/Lungalunga (Tanzania na Kenya), Kabanga/Kobero (Tanzania na Burundi), Rusumo/Rusumo (Tanzania na Rwanda), Mtukula/Mtukula (Tanzania na Uganda),Tunduma/Nakonde (Tanzania na Zambia) na Kasumulu/Songwe (Tanzania/Malawi).

Katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru, Serikali imefanikiwa kuboresha mazingira ya biashara kwa kurahisisha shughuli za usajili wa majina ya biashara, usajili wa makampuni, alama za biashara na huduma, na kutoa hataza, leseni za viwanda na leseni za biashara kwa njia ya mtandao (www.brela.go.tz). Aidha, kampuni inayoshughulikia mfumo wa utambuzi wa bidhaa (BarCodes), GS1 Tanzania imeanzishwa nchini.

Vilevile, kuanzishwa kwa mfumo wa stakabadhi za mazao ghalani mwaka 2007 kumetengeneza mazingira ya ushindani katika ununuzi wa mazao hali iliyosababisha wakulima kuwa na uhakika wa bei za mazao wanayozalisha. Halmashauri katika maeneo husika pia zimenufaika kupitia kodi kutokana na ongezeko la bei. Huku Wakala wa Vipimo (WMA) imeendelea kumlinda mlaji kwa kuhakikisha anapata bidhaa kupitia matumizi ya vipimo sahihi katika ununuzi na uuzaji. Wakala umesogeza huduma karibu na wananchi kwa kufungua ofisi katika mikoa yote ya Tanzania bara na kwa kila Wilaya kwa Mkoa wa Dar es Salaam.

Kwa upande wa masoko ya ndani na nje, Serikali imefanikiwa kuwaunganisha wazalishaji wa ndani na fursa za masoko ya ndani na nje ya nchi kupitia Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam ambayo yanayofanyika mwezi Julai kila mwaka, Maonyesho ya Viwanda yanayofanyika mwezi Desemba kila mwaka, Maonyesho mbalimbali ya Biashara ya Kimataifa ya nje ya nchi yanayolenga kukuza biashara, misafara ya kibiashara inayoingia nchini na inayotoka nje na Maonyesho makubwa ya EXPO yanayolenga kukuza Biashara na kuvutia wawekezaji kama vile Expo Aichi, Expo Shanghai, Expo Zaragoza na mwaka huu 2021 Tanzania inashiriki katika maonyesho ya Dubai EXPO 2020.

Serikali kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru imeendelea na uaandaaji wa viwango na usimamizi wa ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini na zile zinazoingia ndani ya nchi. Aidha kutokana na utaratibu wa kukagua magari baada ya kufika nchini (Destination Inspection) kuanzishwa mnamo Aprili 5, 2021. Hadi tarehe Novemba 4, 2021, jumla ya magari 23,048 yaliyotumika nje ya nchi yalikaguliwa na kuzalisha jumla ya shilingi bilioni 8.019 kama mapato ya Serikali ikilinganishwa na shilingi bilioni 2.375 ambazo zingepatikana endapo ukaguzi huu ungeendelea kufanyika nje ya nchi kwa kutumia mawakala.

Aidha, katika kipindi cha miaka 60 Serikali imefanikiwa kuhamasisha na kulinda ushindani, shughuli za kibiashara na kumlinda mlaji wa bidhaa na huduma dhidi ya mwenendo usio wa haki, na upotoshaji, ukiukaji wa mikataba, muonekano potofu wa bidhaa katika soko kupitia Tume ya Ushindani na Baraza la Ushindani.

Aidha, Serikali imefanikiwa kujenga masoko yanayokidhi viwango vya Kimataifa yanayowawezesha wakulima kuuza mazao yao yakiwa katika ubora. Mfano wa masoko hayo ni Kibaigwa-Dodoma, Kinole na Mgeta - Morogoro, Segera – Tanga na Makambako – Iringa pamoja una ujenzi wa masoko mapya katika kila Mkoa Tanzania bara.

Sekta ya Biashara imewezesha uuzaji wa bidhaa nje ya nchi zenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 6.06 kwa mwaka 2020. Ongezeko hilo limetokana na kuimarika kwa uzalishaji nchini na kutumika kwa fursa mbalimbali za masoko zinazotokana na uhusiano wa kibiashara baina ya Tanzania na nchi moja moja (bilateral), kikanda (regional) na kimataifa (multilateral) kwa madhumuni ya kutafuta fursa za masoko yenye masharti nafuu na kuboresha mazingira ya kufanya Biashara.

Mafanikio hayo yamepatikana kutokana na fursa mbalimbali za masoko ya upendeleo maalum (preferential market access) baina ya Tanzania na nchi za China, India, Japan, Kanada na Korea ya Kusini, Itifaki ya Umoja wa Forodha baina ya Tanzania na nchi zingine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Afrika ya Kati (CEMAC), Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS), Jumuiya ya Ulaya na Uswisi chini ya mpango wa Uza Kila Kitu Isipokuwa Silaha (Everything But Arms - EBA). Mkataba wa Eneo Huru la Biashara barani Afrika (AfCFTA), Karibiani na Pasifiki (ACP) na Kutetea maslahi ya kibiashara ya Tanzania na ya nchi za kundi la LDCs katika majadilianao ya Biashara ya Kimataifa (multilateral trade negotiations).

Mafanikio ya azma ya ujenzi wa uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu ni matokeo ya ushirikiano na jitihada za Wizara zote na Serikali kwa upande mmoja na Sekta Binafsi na Wadau wa Maendeleo kwa upande mwingine. Hivyo, Wizara pamoja na Taasisi zilizo chini yake itaendelea kubuni mikakati na mipango ya kutekeleza majukumu yake ili kuongeza mchango wa Sekta ya Viwanda na biashara katika pato la taifa.






Kiwanda cha dawa cha Prince Pharmaceuticals, Mwanza




Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama nchini na
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan,


MV. UKARA II
HAPA KAZI TU.


# Tumetoka Mbali..... Mzee Msekwa

Na **Jonas Kamaleki**



Tafakuri ya Spika Mstaafu, Mzee Pius Msekwa kuhusu Miaka 60 ya Uhuru inajikita wakati nchi ilivyokuwa kabla ya uhuru, wakati tumepata uhuru hadi sasa.

Mzee Msekwa anafahamu mengi kuhusu uhuru kwani wakati Tanganyika inapata uhuru ndio mwaka alipoajiriwa kwa mara ya kwanza baada ya kutoka Chuo Kikuu Makerere, Uganda.

"Tuliishi kwa shida wakati wa ukoloni, tulibaguliwa sisi watu weusi, tulipuuzwa na kunyanyaswa na utawala wa kikoloni, lakini baada ya kupata uhuru tulianza kuishi kwa neema", anaelezaMzee Msekwa katika mahojiano maalum na Jarida hili.

Kwa mujibu wa Spika Mstaafu, Pius Msekwa wakati Tanganyika inapata uhuru hali ya kiuchumi ilikuwa duni, umeme ilikuwa ni kitu cha kusikia kwa wakubwa kwani nyumbani kwao Ukerewe hapakuwa na umeme, walitumia vibatari kama chanzo cha nishati.

"Tulikuwa tunasomea vibatari ambavyo havikuwa vizuri kwa afya na macho yetu. Wazo la kupata umeme hatukuwa nalo kwani sisi ni watu wa kisiwani hivyo uwezekano wa kupata umeme haukuwepo kabisa, tulijua kuwa sisi ni watu wa kukosa tu", anasisitiza Mzee Msekwa.

Mzee Msekwa anasema kuwa nchi tuliyorithi ni tofauti na tuliyo nayo sasa, kwani ubaguzi ulikuwa mkubwa kuanzia kwenye usafiri, kwenye treni daraja la kwanza lilikuwa la Mzungu, daraja la pili, Mhindi na la tatu Mtu Mweusi.

Anaongeza kusema kuwa elimu nayo ilitolewa kiubaguzi. Kulikuwepo shule za watoto wa kizungu tu. Mfano St. Georges, Iringa, nyingine za wahindi na zile za kiwango cha chini zilikuwa za waafrika.

Mahakama za kikoloni nazo zilikuwa za kibaguzi. Haki haikutendeka kwa watu wote, ilitegemea nani anashitakiwa na nani ni hakimu wa shauri hilo. Kwa ujumla Mzee Msekwa anasema ndiyo maana Mwalimu Nyerere alisema lazima tupambane na hali hiyo tangu siku za mwanzo za uhuru.

Kilichotokea ni kutaifisha shule ili Watanganyika wote waweze kufaidi matunda ya uhuru.

Kuhusu miundombinu, Mzee Msekwa anasema hali ya barabara ilikuwa mbaya. Aliokuwa anasoma nao kutokea mikoa ya Kusini walipata shida sana katika usafiri na liwachukua siku kadhaa kutoka Songea kufika Dar es Salaam au Mwanza.

Miaka 60 ya Uhuru, Mzee huyu anasema yametokea maendeleo makubwa. Kwa sasa mtu anaweza kutoka Songea kwa gari na kufika Dar es Salaam au Kagera siku hiyo hiyo.

Usafiri wa anga umeboreshwa hasa kipindi cha Awamu ya Tano kilichoongozwa na Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. Ndege 11 zimenunuliwa na zinafanya kazi ndani na nje ya nchi. Viwanja vya ndege vimejengwa na kukarabatiwa, rada za kuongozea ndege zimenunuliwa na kusimikwa ili kuimarisha usafiri wa anga.

Usafiri wa majini umeimarishwa kwa kununua meli mpya na kukarabati za zamani kama vile, MV. Victoria, MV. Ukerewe, MV. Lihemba na MV. Serengeti. Usafiri ndani ya Ziwa Victoria umeimarika kwa kusafirisha abiria na mizigo kwa gharama nafuu.

Kwa ujumla Miaka 60 ya Uhuru kwa mujibu wa Mzee Pius Msekwa Tanzania imepiga hatua kubwa kiuchumi, kisiasa, kijamii na uzalendo umeongezeka.

Amewaasa Watanzania waendelee kuishi kwa utulivu na amani na wailinde amani hii kwa gharama zozote. Umoja na mshikamano iwe misingi ya utaifa wa Watanzania kwa kufanya hivyo uhuru wetu utalindwa na kudumishwa.

# Miaka 60 ya Uhuru: Uzoefu wa Mzee Kassim Mpenda Kwenye Tasnia ya Habari

Na **Jonas Kamaleki**

Tanzania inapoadhimisha Miaka 60 ya Uhuru tunapata Tafakuri ya Mwanahabari Mkongwe ambaye amefanya kazi katika vyombo vikubwa vitatu (3) tofauti vya Serikali akiwa katika ngazi ya uongozi.

Mzee Kassim Mpenda historia yake ya kazi za habari inaanzia kwenye Gazeti la Serikali la Kiingereza, The Standard mwaka 1970 hadi 1979 na baadaye kuwa Naibu Mhariri wa Gazeti jipya la Daily News. Anaeleza kuwa jukumu kubwa la gazeti hili lilikuwa ni kuhamasisha ukombozi au uhuru wa nchi za Kiafrika ambazo zilikuwa bado zinatawaliwa. Hii iliakisi Falsafa ya Mwalimu Nyerere ambayo ilisema kuwa uhuru wetu haujakamilika endapo majirani zetu bado wanatawaliwa.

Safari ya habari ya Mzee Mpenda iliendelea alipoteuliwa kuwa Mhariri wa Shirika la Habari Tanzania (SHIHATA). Akiwa SHIHATA anasema alikuwa na wakati mgumu na hali ya uchumi ilikuwa ngumu kipindi Tanzania imemaliza vita dhidi ya Nduli Idd Amin. Anasema kiongozi mmoja wa Serikali alijihusisha na biashara ya sabuni wakati huo ikijulikana kama biashara ya magendo yaani biashara haramu.

Mwandishi mmoja wa Shirika hilo la habari aliandika hiyo Habari na ikatolewa kwenye vyombo vya habari. Kiongozi huyo akashitaki kwa Mwalimu Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati ule.

Mzee Mpenda akiwa katika mtanziko kama Kiongozi wa SHIHATA na huku akisumbuliwa na kiongozi huyo, anasema alikosa amani. Kwa bahati nzuri Mwalimu hakufuatilia hilo shitaka nan do ikawa pona ya Mwanahabari huyo mkongwe.

Kutokana na uwezo wake kitaaluma alihamishiwa Redio Tanzania Dar es Salaan (RTD) kama Mhariri Mkuu. "Nikiwa RTD kulikuwepo na uvamizi uliofanywa na Wareno huko Mtwara, nilichaguliwa kupeleka damu Mtwara kuwasaidia waathirika. Jambo hili lilinifurahisha sana kwani nilikuwa nikiandika taarifa kuhusu uchangiaji wa damu, watu wengi walihamasika kuchangia damu ni maisha ya watu wengi yakaokolewa,"anasimulia furaha yake katika kazi.

Mnamo mwaka 1998, Mzee Mpenda alihamishiwa Idara ya Habari (MAELEZO) kwa nafasi ya Mkurugenzi wa Idara hiyo.

Aliendelea na kazi ya kuisemea Serikali akiwa hapo Idarani hadi alipostaafu.
Anasemaje kuhusu uhuru wa vyombo vya Habari, "Mimi ni muumini mkubwa wa uhuru wa vyombo vya Habari. Acha watu wajieleze bila kuwabughudhi na kuwafungia. Mimi nilikuwa najisikia vibaya kufungia chombo cha Habari. Niliamini mtu akikosea aonywe lakini sio kufungia chombo,"anasema mwanahabari mkongwe, Mzee Kassim Mpenda.

Kuhusu mitandao ya kijamii, Mzee Mpenda anasema habari zinazoandikwa kwenye mitandao ya kijamii zisitumike kumkomoa mtu. Zisiwe habari za upande mmoja bali ziwe na urari.

Miaka 60 ya Uhuru, Mzee Mpenda anasema Nchi inaendelea vizuri kwa utulivu na amani na anasema vyombo vya habari vinatimiza wajibu wake, hapa anamaanisha vya umma na vya binafsi.




Siku ya Uhuru wa Tanganyika 1961

# Mfahamu Mwanamke wa Kwanza Tanzania Kusoma Taarifa ya Habari ya Kiingereza

Ni mwanamke wa kwanza kuwa Mkurugenzi wa RTD.
Ni mwanamke wa kwanza kuwa Mkuu wa Mipango RTD.




> **Safari hii haikuwa rahisi kuanzia kwenye usahili, kuanza mafunzo kazini na hatimaye kusoma taarifa ya Habari nikiwa binti aliyezaliwa na kukulia kijijini,** 'you can imagine'
>
> **Edda Sanga.**

Na **Jonas Kamaleki**

Jarida la NCHI YETU limepata fursa ya kufanya mahojiano maalum na Mwanahabari Mwandamizi na Mkongwe ambaye amefanya kazi RTD miaka ya mwanzo baada ya Tanzania Bara kupata uhuru. Huyu si mwingine ni Bibi Edda Sanga.

Mama huyu, shupavu na jasiri anasimulia safari yake ya kitaaluma baada ya kurudi masomoni nchini Uholanzi na kuanza kazi Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD).

"Safari hii haikuwa rahisi kuanzia kwenye usahili, kuanza mafunzo kazini na hatimaye kusoma taarifa ya Habari nikiwa binti aliyezaliwa na kukulia kijijini, you can imagine", anasema Mama Edda Sanga.

Anaeleza alivyosahiliwa na kupewa kazi ya kutafsiri habari au taarifa za Kiswahili kwenda kwenye lugha ya Kiingereza na za Kiingereza kuzitafsiri kwa lugha Kiswahili ikiwemo misemo ya Kiswahili, "Mfano jitu lenye miraba minne, hiyo unaitafsirije" Anacheka kidogo Mama Edda Sanga.

"Kwa kweli nilipata shida kwani nilikuwa na kisauti cha kitoto licha ya kuweza hizo tafsiri lakini kwenda hewani sikuweza kuruhusiwa licha ya kufanya mafunzo kazini kwa miezi mitatu,"anasisitiza Mama Edda.

Anaeleza kilichomtokea kabla ya kuruhusiwa kwenda hewani, "Nilikawia kidogo, waliniona kama mshamba, Kiswahili changu kilionekana cha kishamba ukilinganisha na Kiswahili cha Pwani kama vile Tanga na Dar es Salaam. Wanawake tulikuwa tunapewa vitu laini kama vipindi vya watoto na kusoma kadi za salamu," anaeleza Edda Sanga.

Safari yake ya kukua kitaaluma inaanza na alipopata nafasi ya kutangaza kwa kiingereza katika Idhaa ya Nje. Hapa Edda Sanga anasema alifanya hiyo kazi kwa umahiri akitengeneza na kutangaza vipindi vya wapigania uhuru wa nchi za Kusini mwa Afrika ambazo zilikuwa zinatawaliwa na wakoloni kama vile Msumbiji, Angola, Zimbabwe, Afrika Kusini na Namibia.

## Nilikuwa mwanamke wa kwanza kusoma taarifa ya habari ya kiingereza hapa nchini miaka ya sabini

"Nilianza kupata mialiko ndani na nje ya nchi, nilihudhuria Mkutano wa Wanawake Duniani uliofanyika Nairobi, uliojulikana kama "Nairobi Looking Forward Strategies", na pia nilishiriki Mkutano Senegal ambao ulikuwa wa kuwaandaa wanawake wa Afrika kwa ajili ya Mkutano wa Beijing,"anasimulia Edda Sanga mwanzo wa Safari yake ya mafanikio kitaaluma.

Kwa sauti iliyojaa furaha, Edda Sanga anasema, "Nilikuwa Mwanamke wa kwanza kusoma Taarifa ya Habari ya Kiingereza hapa nchini miaka ya sabini". Nilifanya maandalizi makubwa ili nisiangushe wanawake wenzangu, maandalizi yalikuwa kabambe. Niliisoma vizuri, mabosi wangu walinisifia, kusema ukweli nilijisikia vizuri sana na nilimshukuru sana Mungu".


Mwanahabari huyu nguli alikuwa mwanamke wa kwanza Tanzania kuwa Mkuu wa Mipango, Naibu Mkurugenzi wa RTD na hatimaye Mkurugenzi wa kwanza mwanamke RTD. Kwa mujibu wa Edda Sanga hili jambo lilimfurahisha sana na kumfanya aendelee kufanya kazi yake kwa kujiamini na kuipenda.

Katika kufanya kazi zake alichukizwa sana na mfumo dume kiasi kwamba baadhi ya wanaume au vijana wa kiume waligoma kufuata maelekezo yake kisa yeye ni mwanamke. Anasema hakukata tama alipambana hadi wakamuelewa na kwenda nao sawa.

Kuhusu Mitandao ya Kijamii Mama huyu Shupavu asiyeficha hisia zake akiwa na jambo anasema inapaswa kudhibitiwa ili itoe taarifa sahihi kwa kuzingatia maadili ya Mtanzania. Wanaohusika na kutoa taarifa ya kwenye mitandao ya kijamii wapewe mafunzo ili waweze kujua nini cha kuripoti na kipi si cha kuripoti.


Edda Sanga anasema Miaka 60 ya Uhuru imeleta mafanikio makubwa katika Tasnia ya Habari kuanzia kwenye ongezeko la vyombo vya Habari, uhuru wa vyombo vya Habari na matumizi ya teknolojia ya kisasa katika kupashana habari.

Kwa maneno yake anasema safari haikuwa rahisi lakini kwa uwezo wa Mungu alifika alipopataka.



# Miaka 60 ya Uhuru Muungano Wetu ni Imara na Mfano wa Kuigwa

Na **Mwandishi Wetu - MAELEZO**



Muungano wa dola kadhaa unaounda taifa moja lenye nguvu ni dhihirisho la ustaarabu wa kisasa unaochochea ukuaji wa uchumi na ustawi wa maisha ya wananchi wanaoishi kwenye himaya iliyotokana na umoja.

Ni dhahiri kwamba ustawi wa watu wa Marekani (USA), Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na Uingereza (UK) umechagizwa na muungano, sera nzuri na uchapakazi wa viongozi na raia wa mataifa hayo.

Mara baada ya uhuru wa Tanganyika wa mwaka Desemba 9, 1961 na mapinduzi matukufu ya Zanzibar ya tarehe 12 Januari 1964, himaya mbili hizi ziliungana mnamo Aprili 24, 1964 na kuunda Taifa linalojulikana kama Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akichanganya udongo wa Tanganyika na Zanzibar ikiwa ni ishara ya kuunganisha nchi mbili wakati wa Sherehe ya Muungano Dar es Salaam tarehe 26 Aprili, 1964




Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (kushoto) na Sheikh Abeid Amani Karume (kulia) wakibadilishana Hati za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar tarehe 27 Aprili, 1964.

Muungano huo ukazalisha serikali mbili, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) inayoshughulikia mambo yote yasiyo ya Muungano, kwa upande wa Tanzania-Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) inayoshughulikia mambo yote ya Muungano kama yalivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na yasiyo ya Muungano kwa upande wa Tanganyika (Tanzania Bara).

Mambo yaliyosababisha Muungano huu ni historia na ukaribu wa dola mbili hizi, muingiliano wa kijamii, ushirikiano wa kibiashara, ushirikiano madhubuti na wa muda mrefu wa kisiasa baina ya TANU na ASP, ushirikiano na urafiki wa muda mrefu kati ya watu hususan katika harakati za utaifa uliopelekea uhuru wa ardhi hizi mbili.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Muungano na Mazingira) mnamo Novemba 15, 2021 jijini Dodoma, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar unahusisha mambo 22 yanayohusu Katiba, Bunge na Utawala Bora; Fedha na Biashara; Ulinzi na Usalama; Diplomasia na Ushirikiano wa Kimataifa; Usafiri na Usafirishaji; Utabiri wa Hali ya Hewa; na Elimu, Sayansi na Teknolojia.

"SMT na SMZ zimefanikiwa kusimamia utekelezaji wa mambo ya Muungano kwa ufanisi mkubwa na hivyo kuimarika kwa utaifa na umoja, amani na utulivu, na hali ya maisha ya watu kutokana na ukuaji wa uchumi wa pande mbili za Muungano.," inaeleza sehemu ya taarifa hiyo inayohabarisha mafanikio ya miaka 60 ya uhuru wa Tanzania Bara.



Hivi sasa, watu wengi kutoka Tanzania Zanzibar wanafanya shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii Tanzania Bara. Shughuli hizo ni kilimo, biashara, masomo ya elimu ya juu, na ajira katika utumishi wa umma na sekta binafsi. Hali kadhalika, wapo waliotoka Tanzania Bara kwenda Tanzania Zanzibar kujitafutia riziki halali.

"Nchi imeimarisha miundombinu ya barabara, usafiri wa anga, usafiri wa majini na huduma za kijamii katika pande zote za Muungano na kuendelea kutumia maliasili vizuri kwa manufaa ya wananchi kuliko ilivyokuwa kabla ya Muungano.

"Mafanikio haya, bila shaka, ndiyo yaliiwezesha Tanzania kutangazwa na Benki ya Dunia kuwa imeingia katika kundi la nchi za uchumi wa kati kutoka kundi la nchi masikini mwezi Julai 2020," inaarifu taarifa hiyo.

Sanjari na hayo, mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuwa salama kutokana na ulinzi madhubuti wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa kushirikiana na vikosi vingine na wananchi wa pande mbili za Muungano.

Watanzania wengi tunajivunia Muungano wetu ambao ni zao la uhuru wa Tanzania.

Nchi nyingi zilijaribu kuungana zikashindwa. Mathalan, Senegal na Gambia ziliungana na kuunda taifa la Senegambia, lakini muungano huo ulidumu kuanzia Desemba 1981 hadi Septemba 1989.

# Utamaduni, Sanaa, Michezo Vyakonga Nyoyo za Watanzania Miaka 60 ya Uhuru

Na **Eleuteri Mangi, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**

Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ni miongoni mwa ni Wizara zenye sekta kongwe na za mwanzo kuundwa na Serikali ya Awamu ya Kwanza tangu kupatikana kwa Uhuru wa Tanganyika mwaka 1961 chini ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Tangu mwaka 1961 Wizara imekuwa kinara wa kusimamia na kuhakikisha Taifa linaendelea kuenzi Utamaduni imara wa Mtanzania, kuwa na kazi bora za Sanaa na taifa lenye umahiri mkubwa katika michezo.

Falsafa hiyo imejengwa katika moja ya falsafa muhimu aliyoweka Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere kwa kuamini kuwa Utamaduni ni kiini ama roho ya taifa lolote, taifa lisilo na utamaduni ni sawa na mkusanyiko wa watu usio na roho.

Pia kwa umuhimu huo huo Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe, Samia Suluhu Hassan imekuja na falsafa ya kupenda vya kwetu ambapo imefanya mapinduzi makubwa katika kipindi kifupi. Mathalani mafanikio kwenye soka la wanawake, kufufua UMISSETA na UMITASHUMTA, kuanzisha tamasha kubwa la michezo kwa wanawake la Tanzanite, Ushindi wa kihistoria wa mashindano ya 'Miss and Mr Deaf Africa' na Tamasha la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni la Bagamoyo

Kwa mujibu wa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Innocent Bashungwa, Katika Sekta ya Utamaduni, katika kipindi hiki Serikali kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, imefanikiwa kuanzisha Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania; Mfuko wa Utamaduni na Sanaa umehuishwa ili, pamoja na mambo mengine uweze kugharamia mafunzo kwa Sekta za Sanaa na Utamaduni na kutoa mikopo ya masharti nafuu kwenye miradi bora ya Sanaa na Utamaduni.

Serikali imeanza mchakato wa kujenga jengo la Kisasa eneo la NCC Jijini Dodoma ambalo litakuwa One Stop Center kwa Taasisi za Wizara zinazohudumia Sekta ya Utamaduni na Sanaa.

Aidha, lugha aushi na adhimu ya Taifa Kiswahili chini ya Serikali imeendelea kuimarika na kutumika hatua inayoifanya kuwa lugha ya 10 kutumiwa na watu wengi duniani.

Kwenye Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC uliofanyika kwa siku mbili kuanzia Agosti 17-18, 2019) katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam chini ya aliyekuwa Mwenyekiti wa jumuiya hiyo, Rais wa Serikali ya Awamu ya Tano Hayati Dkt. John Pombe iliamuriwa kuwa lugha ya Kiswahili iwe lugha rasmi ya nne ya jumuiya hiyo.

Mafanikio haya yameifanya Wizara kununua vifaa vya ukalimani ambavyo vinamchango mkubwa wa kuisaidia lugha ya Kiswahili kuendelea kutumika kimataifa kwa kuwapata wakalimani ambao ni wabobezi kwa kutumia vifaa vya kisasa katika kazi mbalimbali duniani.

Tanzania imeendelea kuwa na mafanikio kedekede hatua iliyofanya kupewa heshima ya kuwa Makao Makuu ya Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika mwaka 2011 na Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika walioidhinisha utekelezaji wa Programu hiyo na kuomba Kamisheni ya Umoja wa Afrika na Nchi Wanachama kushirikiana na Tanzania kuhakikisha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika unatukunzwa na kuhifadhiwa.

Programu hiyo ilizinduliwa rasmi na Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Ukumbi wa Mlimani City- Dar es Salaam tarehe 8 Desemba, 2011 ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo, Dkt. Hassan Abbasi anasema, katika kipindi hiki kumeundwa Idara ya Maendeleo ya Sanaa baada ya muundo mpya wa Wizara ya mwaka 2016. Kabla ya hapo Idara ilikuwa ni sehemu ndani ya Idara ya Maendeleo ya Utamaduni.

> **Ni kutokana na usimamizi wa Baraza muziki wa Bongo Fleva na Singeli umezaliwa, Sanaa za uchongaji za kisasa (modern carvings) zimezalishwa (mfano Ujamaa, Mawingu, Kimbulumbulu) na pia Sanaa za michoro kama Tingatinga ambazo ni ngeli zinazoitangaza Tanzania kimataifa**
>
> Dkt. Emmanuel Ishengoma.





Pia kuanzishwa kwa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) ambapo Mwaka 1984 Serikali ilitunga Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa Na. 23 ambayo ilianzisha Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA). Pamoja na majukumu mengine husajili Wasanii, kutoa vibali vya shughuli za Sanaa, kuwatetea wasajiliwa wake, kuwatafutia masoko ya kazi zao na kusimamia uanzishwaji wa Mashirikisho ya Sanaa nchini. Kuwepo kwa Baraza kumeifanya Sekta ya Sanaa kushamiri hadi kufikia Sekta kuongoza katika ukuaji kwa mwaka 2018/2019 kwa asilimia 13.7.

"Ni kutokana na usimamizi wa Baraza muziki wa Bongo Fleva na Singeli umezaliwa, Sanaa za uchongaji za kisasa (modern carvings) zimezalishwa (mfano Ujamaa, Mawingu, Kimbulumbulu) na pia Sanaa za michoro kama Tingatinga ambazo ni ngeli zinazoitanagaza Tanzania kimataifa". Anafafanua Mkurugenzi wa Idara ya Sanaa. Dk Emmanuel Ishengoma.

Pia katika kipindi hiki kuamenzishwa kwa Bodi ya Filamu Tanzania (TFB) ambapo Mwaka 1976 Serikali ilianzisha Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Tanzania kwa Sheria Namba 4 ambayo husimamia masuala yote ya Filamu na Michezo ya kuigiza, kusajili wasanii na wadau katika Tasnia ya Filamu na Michezo ya Kuigiza na kutoa vibali vya kuendesha shughuli husika. Bodi ya Filamu imewezesha kuzaliwa ngeli ya Bongo Movies ambayo sasa ni maarufu Afrika na duniani kote.

Chini ya Bodi ya Filamu, Waziri mwenye dhamana na Sanaa nchini alianzisha Kamati ya Kutetea Haki za Wasanii ambapo familia za wasanii kama marehemu Stephen Kanumba na marehemu King Majuto wamenufaika.

Vilevile Kuanzishwa kwa Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) mwaka 1999 kwa Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Namba 7 ambapo pamoja na mambo mengine huwalinda na kuwatetea wabunifu dhidi ya matendo ya uharamia na kusaidia kukusanya mirabaha itokanayo na matumizi ya kazi zao.

Baada ya kuonekana kuna uhitaji mkubwa wa kuwa na mafunzo rasmi ya mambo ya Sanaa mwaka 1972 Serikali ilianzisha Chuo cha Sanaa Bagamoyo (BCA).

Mwishoni mwa mwaka 2005 uamuzi ulifanywa na iliyokuwa Wizara ya Elimu na Utamaduni kwamba, Chuo cha Sanaa Bagamoyo kibadilishwe kuwa wakala wa Serikali chini ya mpango wa mabadiliko ya sekta ya umma, kwa hiyo Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo kuanzishwa Novemba 2007 kwa tangazo Na. 220 lililochapishwa kwenye gazeti la Serikali kwa mujibu wa sheria ya Wakala wa Serikali namba 30 ya mwaka 1997.

Taasisi hii imefanikiwa kuelimisha wasanii muhimu hapa nchini ambao sio tu wanaendesha shughuli zao kwa ufanisi na hivyo kuwahamisha wengine kujiunga bali pia wanataaluma katika eneo la Sanaa wametokana na Chuo hiki. Mifano hai ni pamoja na Msanii Mrisho Mpoto na mwanazuoni Profesa Frowin Paul Nyoni.

Akilihutubia Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dodoma, 22 Aprili 2021 kutoa mwelekeo wa Serikali yake, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan alisema Sekta ya sanaa, michezo na utamaduni inakua kwa kasi kubwa hivi sasa na kuonesha kuwa vijana wetu wengi wamepata ajira kupitia sekta hiyo.

Kwa upande wa Sekta ya michezo Waziri mwenye dhamana ya Michezo. Mhe, Innocent Bashungwa amefafanua kwamba Tanzania imefanikiwa kupata jumla ya Medali 16 katika michezo mikubwa kabisa duniani ambayo ni ya Olympic (2), Jumuiya ya Madola (7) na Michezo ya Bara la Afrika (7) na kwamba timu zetu zimeshiriki katika michezo hii mikubwa bila kukosa tangu uhuru.

Kwa upande wa wachezaji wa kulipwa Tanzania imefanikiwa kuwa na wachezaji wakulipwa katika nchi mbalimbali tangu uhuru. Kwasasa inajumla ya wachezaji 54 wakulipwa katika nchi mbalimbali ambapo (28) ni wachezaji wa mpira wa miguu, (16) mpira wa kikapu, (4) mpira wa wavu, (2) Kabbadi, (2) Netiboli (1) kuogelea na (1) mchezo wa Roliball.

**Wanawake hawakuwa wanashiriki katika baadhi ya michezo kabla ya uhuru lakini sasa kumekuwa na ongezekzo kubwa kushiriki katika michezo mathalan mpira wa miguu ambapo sasa ligi ya mchezo huo imeanzishwa na Timu za Taaifa za mchezo huo zimeundwa** ”

Yusuf Singo, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Michezo

Vile vile Tanzania imeshinda vikombe mbalimbali katika mashindano ya kimataifa tangu kupata uhuru wake ambapo kwa upande wa mpira wa miguu kwa wanawake Tanzania imechukua vikombe vitano (5) katika mashindano mbalimbali ya kimataifa ikiwa ni pamoja na COSAFA, EAst Afriaca, CECAFA. Aidha kwa upande wa mpira wa miguu kwa wanaume timu zetu zimefuzu kushiriki kwenye mashindano mbalimbali ambapo Taifa stars imefuzu mara 2 kushikiri fainali za kombe la Afrika AFCON 1980 na 2019 vile fainali za mashindano ya wachezaji wa ndani CHAN mara mbili.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Michezo nchini Yusufu Singo, Timu ya Gofu Wanawake ilichukua ushindi wa Bara la Afrika na timu zetu za Kricketi chini ya umri wa miaka 19 na Timu ya Wanawake kushika nafasi za tatu katika Bara la Afrika mwaka 2021. Pia kuongezeka kwa ushiriki wa wanawake katika michezo mbalimbali.

“Wanawake hawakuwa wanashiriki katika baadhi ya michezo kabla ya uhuru lakini sasa kumekuwa na ongezekzo kubwa kushiriki katika michezo mathalan mpira wa miguu ambapo sasa ligi ya mchezo huo imeanzishwa na Timu za Taifa za mchezo huo zimeundwa”, ameongeza Singo.

Anasema, watalaam wa michezo wameongezeka kwa kuongeza udahili katika vyuo vinavyo fundisha fani ya michezo ikiwa ni pamoja na Chuo cha Maendeleo Malya na Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Malya kilidahili wanafunzi 40 mwaka 2013 hadi na kufikia wanafunzi 137 mwaka 2020. Aidha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilidahili wanafunzi 14 mwaka 1997 hadi kufikia wanafunzi 105 mwaka 2020.

Kwa upande wa mabondia pia kumekuwa na mafanikio makubwa ambapo mabondia wameshinda katika mapambano mbalimbali na kujinyakulia ubingwa wa Bara la Afrika, mabara mengine na dunia, baadhi ya mabondia hao ni pamoja na Hassan Mwakinyo ambaye ni bingwa wa uzito walterweight, Bruno Melchony aliyenyakua mkanda wa International Super Featherweight, Tony Rashid mkanda wa Super Bantaman, Abdalah Shaban Pazi mkanda wa Asia Pacific Superweight middleweight na Salin Jengo world Supe featherweight.

Mwaka 2019 Tanzania imeshiriki mashindano ya special Olympic yaliyofanyika Abu-Dhabi na Tanzania kupata jumla ya medali 16 katika mashindano ya Riadha (12 Dhahabu, 1 Fedha na 2 Shaba) mwaka 2020 Tanzania imeshiriki Special Olympic iliofanyika Misri na Tanzania kupata medali 11 (Dhahabu 6, Fedha 3, na Shaba 2). Timu ya mpira wa miguu kwa watu wenye ukemavu kwa mara ya kwanza walishiriki mashindano ya Bara la Afika kwa michezo hiyo na kushika nafasi ya 4.

Mafanikio haya ya Wizara ni mwanzo mpya unaotokana na maono yenye tija na uongozi thabiti wa Wizara ambayo yamejengwa kwenye dhima ya taifa ya kukuza Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa lengo la kuleta maendeleo ya jamii kiuchumi kwa kuongozwa na kaulimbiu ya Serikali ya Awamu ya Sita “Kazi Inendelee”.

**“Watalaam wa michezo wameongezeka kwa kuongeza udahili katika vyuo vinavyo fundisha fani ya michezo ikiwa ni pamoja na Chuo cha Maendeleo Malya na Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Malya kilidahili wanafunzi 40 mwaka 2013 hadi na kufikia wanafunzi 137 mwaka 2020.**

Yusuf Singo, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Michezo











# Maendeleo ya Teknolojia Yarahisisha Mawasiliano

Na **Prisca Ulomi- Wizara ya Habari, Mawasiliano na TEHAMA**

"Serikali inatarajia kuwa na jamii iliyohabarika kama Katiba ya nchi inavyofafanua kwa kuwa na jamii na vyombo vya habari vinavyozingatia maadili na weledi wa taaluma ya habari sambamba na jamii inayoendana na mabadiliko ya teknolojia ya habari yanayotokea duniani," Dkt. Ashatu Kijaji, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari aliwaeleza Watanzania katika mkutano wa waandishi wa habari uliofanyika Novemba 16, 2021 jijini Dodoma.

Katika mkutano huo, Waziri Kijaji amearifu mafanikio yaliyofikiwa katika sekta anazozisimamia ndani ya miaka 60 ya uhuru wa Tanzania Bara huku akifahamisha azma ya Serikali katika kuziendeleza sekta hizo kwa manufaa ya Watanzania.

Nukuu ya kiongozi huyo iliyopo hapo juu inadhihirisha kwamba Serikali inayotokana na Chama Cha Mapinduzi imedhamiria kutekeleza maono ya Chama hicho yanayotaka kumaliza kabisa umasikini wa taarifa, juhudi ambazo ziliasisiwa na Baba wa Taifa Hayati Julius Kambarage Nyerere.

Itakumbukwa kuwa, baada ya Tanzania Bara kupata uhuru Desemba 9, 1961 na baada ya nchi kutangaza mwelekeo wake kwenye Azimio la Arusha la 1967, vyombo vya habari vichache vilivyokwepo vilitekeleza maono ya Serikali yaliyokusudia kumaliza umasikini wa taarifa katika mapambano dhidi ya ujinga, maradhi na umasikini.

Mathalan, kitabu kilichoandikwa na Martin Stummer kinachoitwa "The Media History of Tanzania" kinaeleza kwamba mwaka 1975 Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD) ilianza kurusha kipindi kijulikanacho kama "Mtu ni Afya" ili kupambana na adui maradhi.

Utafiti uliofanywa mnamo 1981 ulibaini matokeo ya kipindi hiki huko Bahi – Dodoma ambapo nyumba zilizokuwa na bomba la maji ziliongezeka kutoka 37 hadi 54, nyumba zenye vyoo kutoka 37 hadi 54, nyumba zenye vyandarua kutoka 37 hadi 54, nyumba zenye madirisha kutoka 20 hadi 60, na nyumba zisizokuwa na panya kutoka 27 mpaka 154.

Ili vyombo vya habari viweze kumaliza umasikini wa taarifa muhimu zinazoinua maisha ya Watanzania, sheria mbalimbali zimetungwa tangu Tanzania Bara ilipopata uhuru. Baadhi ya sheria hizo ni Sheria ya Magazeti 1976, Sheria ya Utangazaji ya Mwaka 1993, Sheria ya Huduma za Habari 2016 na Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa 2016.

Sera, sheria na maono mema ya viongozi wa awamu zote ndizo zilizochangia ongezeko la vyombo vya habari. Aidha, matatu hayo yalichochea matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) pamoja na mawasiliano ya kutumia njia ya posta.

Kwa upande wa vyombo vya habari, katika miaka 60 ya uhuru, redio zimeongezeka kutoka moja hadi zaidi ya redio 200 na kutoka kutokuwa na hata chaneli moja ya televisheni mpaka sasa ambapo kuna vituo vya televisheni 48. Hali kadhallika, kwa sasa kuna jumla ya magazeti na machapisho yaliyosajiliwa 270, tovuti 122 na redio mtandao dhaidi ya 20.

Katika sekta ya TEHAMA, matumizi ya kompyuta yalianza mwaka 1965 huku watumiaji wa intaneti wakiwa wamefikia 29,152,713 mnamo Juni 2021 ambao kabla ya uhuru hawakuwepo. Aidha, mnamo 1961 hakukuwa na Mkongo wa Taifa lakini hadi kufika mwaka 2016 kulikuwa na kilomita 7,910 za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Pamoja na hayo, himaya hiyo imekuwa ikienda sambamba na aina za TEHAMA zilizogunduliwa baada ya uhuru. Hadi Juni 2021 kulikuwa na laini za simu za mkononi 53,111,246 huku watumiaji wa simu za mezaji wakiongezeka kutoka 16,238 mwaka 1961 hadi 71,405.

> **Katika sekta ya TEHAMA, matumizi ya kompyuta yalianza mwaka 1965 huku watumiaji wa intaneti wakiwa wamefikia 29,152,713 mnamo Juni 2021 ambao kabla ya uhuru hawakuwepo.**
> Dkt. Ashatu Kijaji, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

**Wakati wa uhuru, Serikali ilianzisha huduma ya ofisi ndogo za posta iliyojulikana kwa jina la Sub-Post Office kwa ajili ya kuhudumia wananchi kwa kutoa huduma za posta kwa siku maalumu za mikusanyiko kama vile siku za magulio ambapo kunakuwa na mkusanyiko wa watu wengi**

Dkt. Ashatu Kijaji,
Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.



Hadi sasa nchi yetu ina jumla ya minara ya mawasiliano 12,902 ambapo minara 2,630 inatoa huduma ya 2G pekee na minara 9,579 inatoa huduma ya mawasiliano ya 2G, 3G au/na 4G.

"UCSAF imejenga minara 1,068 kati ya minara tajwa hapo juu kwa kutumia ruzuku ya Serikali kwa kushirikiana na watoa huduma ambapo hadi sasa takribani shilingi bilioni 161 zimetumika kujenga minara hiyo.

"Hivyo, ujenzi wa minara ya mawasiliano umefanyika kwenye kata 2,579 za Tanzania Bara kati ya kata 3,956 ambazo ni sawa na asilimia 65 na kwa upande wa Zanzibar, minara hiyo imejengwa kwenye kata 101 kati ya kata 110 ambazo ni sawa na asilimia 92.

"Mnara mmoja una uwezo wa kutoa huduma za mawasiliano kutoka eneo mnara ulipo hadi eneo la umbali wa kilomita 11 kutegemea na jiografia ya eneo husika na aina ya masafa kwa kuwa huduma za mawasiliano kutoka katika mnara zinafika mbali zaidi kama eneo ni tambarare, halina misitu, miti mirefu, miinuko na milima," amearifu Dkt. Kijaji.

Akielezea maendeleo kwenye huduma za posta, Waziri Kijaji amesema: "Wakati wa uhuru, Serikali ilianzisha huduma ya ofisi ndogo za posta iliyojulikana kwa jina la Sub-Post Office kwa ajili ya kuhudumia wananchi kwa kutoa huduma za posta kwa siku maalumu za mikusanyiko kama vile siku za magulio ambapo kunakuwa na mkusanyiko wa watu wengi."

Ni wazi kwamba juhudi za Serikali katika kuziendeleza Sekta za Habari, Mawasiliano na TEHAMA zimesaidia kupunguza umasikini wa taarifa muhimu wanazohitaji Watanzania katika kuboresha hali za maisha yao ikiwamo kwa kujenga nyumba bora zenye vyoo vya kisasa. Taarifa hizo huzipata kwenye vyombo vya habari vya kawaida, mitandao ya kijamii au kwa kutumiana jumbe fupi kwenye simu zao.

**Mnara mmoja una uwezo wa kutoa huduma za mawasiliano kutoka eneo mnara ulipo hadi eneo la umbali wa kilomita 11 kutegemea na jiografia ya eneo husika na aina ya masafa kwa kuwa huduma za mawasiliano kutoka katika mnara zinafika mbali zaidi kama eneo ni tambarare, halina misitu, miti mirefu, miinuko na milima.**



Dkt. Ashatu Kijaji,
Waziri wa Habari, Mawasiliano
na Teknolojia ya Habari.



Dkt. Zainab Chaula
Katibu Mkuu,
Wizara ya Habari, Mawasiliano
na Teknolojia ya Habari.



Shule ya Sekondari ya wavulani Ihungo, Bukoba, Mkoani Kagera

# Miaka 60 ya Uhuru: Ustawi wa Jamii Katika Elimu, Afya na Miundombinu

- **Kutoka Shule za Msingi 3,270 mwaka 1961 hadi 16,656 mwaka 2021**
- **Kutoka wanafunzi 486,470 mwaka 1961 hadi 10,687,593 mwaka 2021**
- **Zahanati kutoka 158 mwaka 1961 hadi 5,152 mwaka 2021**

Na **Nteghenjwa Hosseah, OR-TAMISEMI**

MARA baada ya Uhuru mwaka 1961, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliyekuwa Waziri Mkuu wa kwanza aliunda Wizara ya Serikali za Mitaa na kumteua Mhe. Job Lusinde kuwa Waziri wa kwanza kuongoza Wizara hii. Ndani ya miaka 60, wizara hii imeongozwa na mawaziri 19 na kati ya hao wanawake ni watatu akiwemo Waziri wa sasa Mhe. Ummy Mwalimu.

Kipindi chote cha miaka 60 ya Uhuru, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imekuwa ni Wizara inayojitegemea na katika vipindi tofauti imekuwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Rais huku makao Mkuu yake yakiwa Dodoma mara baada ya Serikali kutangaza kuhamishwa makao Makuu kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma miaka ya 70 kwa lengo la kurahisisha utoaji huduma na kutoa fursa sawa kwa wadau wake wakuu hususan Mikoa na Mamlaka za Serikali za mitaa.

Baada ya Uhuru, kulikuwa na halmashauri 45 na majimbo 10 ya Utawala yaliritihiwa kutoka utawala wa kikoloni wa Mwingereza, Serikali ilifanya mageuzi kwa kuunda mikoa 15 na kuondoa utaratibu wa mgawanyo wa nchi katika majimbo. Hadi sasa kuna mikoa 26, Wilaya 139, Halmashauri 184, Tarafa 570, Kata 3,956, Vijiji 12,319, Vitongoji 64,384 na Mitaa 4,263.

Wakati wa Uhuru hakukuwa na Halmashauri za Majiji na sasa kuna Halmashauri za Majiji 6, kulikuwa na Halmashauri ya Manispaa moja ya Dar es Salaam na sasa kuna Halmashauri za Manispaa 20, Halmashauri za Miji zilikuwa 9 na sasa Halmashauri za Miji ni 21 na Halmashauri za Wilaya zilikuwa 10 na sasa zipo Halmashauri za Wilaya 137.

Kwa lengo la kuziimarisha Serikali za Mitaa na kuziwezesha kutoa huduma bora kwa wananchi, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ikiwemo ya Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa ulioanzishwa mwaka 1998 ambao ulilenga katika kupeleka madaraka kwa Wananchi (D by D) na kuwa njia muafaka wa kufikisha na kuharakisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi na kuinua utoaji wa huduma kwa wananchi.

Katika Sera hii Mamlaka za Mitaa zinapewa uhuru wa kufanya maamuzi mbalimbali yanayohusu utoaji wa huduma kwa wananchi walio katika Mamlaka zao na kuwashirikisha katika kujiletea maendeleo na ustawi wao kwa ujumla na kwa kuzingatia Katiba na Sheria za nchi.

Kuhakikisha kunakuwa na Usimamizi wa Rasilimali Fedha mzuri kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, Serikali imeendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa katika hatua ambayo imepunguza hati chafu kutoka 20 mwaka 2004/2005 hadi kufikia 8 mwaka 20019/2020.

Kuhusu kuwawezesha Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kati ya mwaka 2005 hadi 2010, Halmashauri 88 zimepatiwa Sh millioni 708.8 kila moja kwa ajili ya kukopesha vikundi hivyo. Aidha, katika kipindi cha 2006 hadi 2010, Vyama vya Kuweka na Kukopa (SACCOs) 232 katika Halmashauri 128 zilikopeshwa jumla ya Sh bilioni 1.2 kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Vijana kwa lengo la kuwawezesha vijana kimtaji..

Kiasi cha Sh bilioni 145.83 kimetolewa kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka 2020 na kunufaisha vikundi 47,309 vyenye watu 490,815 ambapo wanawake ni 318,616, vijana ni 155,781 na watu wenye ulemavu ni 16,418. Mikopo hii imechangia kukuza uwekezaji mdogo na mkubwa na kuongeza kipato cha wananchi. Aidha, kuanzia mwaka wa fedha 2019/20, mikopo kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu inatolewa bila riba.

Aidha, katika kudhibiti uadilifu, Serikali imeanzisha Kamati ya kudhibiti uadilifu na kuimarishwa kwa lengo la kuhakikisha Ofisi ya Rais TAMISEMI kudhibiti na kupambana na vitendo vyote vya rushwa na viashiria ikiwa ni kuendeleza jitihada za Serikali katika mapambano dhidi ya rushwa.

Kwa upande wa Sekta ya Elimu ndani ya miaka 60 ya Uhuru, Serikali imefanya maboresho mbalimbali katika Elimumsingi kwa lengo la kuongeza upatikanaji, ubora na usawa katika elimu.

Kabla ya mwaka 1961, elimu ilitolewa kwa watu wachache kwa lengo la kupata maafisa ambao wanaweza kusaidia katika shughuli za utawala na kuandaa watu kwa ajili ya kushika uongozi wa nchi huku kukiwa na Shule za Msingi 3,270 zilizokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 450,626.

Shule hizo zilitoa elimu kwa matabaka ya rangi ambapo kati ya Waafrika 9,869,000 wanafunzi 431,056 walipata nafasi ya kusoma katika shule 3,115 na kati ya wananchi wasio Wafrika 150,000 wanafunzi 19,570 walipata nafasi ya kusoma katika shule 155.

Mabadiliko yalifanyika katika mfumo wa uendeshaji wa elimu nchini yalitokana na pamoja na mambo mengine; Azimio la Arusha lilipelekea kuanzisha mikondo mingi ya shule za msingi hasa katika Vijiji vya Ujamaa na kuongeza idadi ya wanafunzi kutoka 753,114 mwaka 1967 hadi 848,215 mwaka 1971.

Ubinafishaji wa Shule za Msingi na Sekondari kutoka kwa Mashirika ya Dini na taasisi binafsi. Lengo la ubinafsishaji huu ni kuongeza fursa za utoaji wa Elimu kwa watu wote bila ya ubaguzi kama ilivyokuwa wakati wa mkoloni wa Kiingereza.

Tanzania iliridhia utekelezaji wa tamko la 'Education for all' kwa kuanzisha Programu ya Universal Primary Education – UPE. UPE iliongeza fursa za utoaji wa Elimu kwa wanafunzi ambao walifikia umri wa kwenda Shule. Elimu ya Msingi ilitajwa kama ya lazima;

Juhudi za serikali zilichangia kuongezekea kwa idadi ya shule za Msingi za Serikali kutoka 3,270 mwaka 1961 hadi 16,656 mwaka 2021, huku idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka wanafunzi 486,470 mwaka 1961 hadi 10,687,593 mwaka 2021 huku walimu wameongezeka kutoka 9,885 mwaka 1961 hadi 171,993 mwaka 2021.

Kwa upande wa shule za Elimu Maalum zimeongezeka kutoka nne za wamisionari (Tabora, Buigiri, Irente na Uhuru Mchanganyiko mwaka 1961 hadi kufikia 746 mwaka 2021 huku idadi ya wanafunzi wenye mahitaji maalum imeongezeka kutoka 1,000 mwaka 1960 hadi 70,265 mwaka 2021;

Shule za Sekondari zimeongezeka kutoka 39 mwaka 1961 hadi 4,002 za Serikali mwaka 2021, idadi ya wanafunzi ikiongezeka kutoka wanafunzi kutoka 11,832 mwaka 1961 hadi 2,379,945 mwaka 2021 wakati walimu wameongezeka kutoka 764 mwaka 1961 hadi 87,992 mwaka 2021.

Miundombinu ya kutolea huduma za Afya ya Msingi na mkakati ni kuhakikisha ujenzi wa Hospitali kwenye Halmashauri ambazo hazikuwa na Hospitali, vituo vya Afya vinakuwa na uwezo wa kutoa huduma za upasuaji na kukamilisha maboma ya Zahanati.



Muonekano wa sasa wa Vyumba vya madarasa katika Chuo cha FDC Ilula baada ya Ukarabati

Katika Kipindi cha miaka 60 ya Uhuru, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imefanikiwa kuongeza idadi ya Zahanati kutoka 158 hadi 5,152, Vituo vya Afya kutoka 49 hadi 630 na Hospitali za wilaya kutoka 14 hadi 154.

Matarajio ni kuendelea kuboresha miundombinu chakavu katika vituo vya zamani pamoja na kujenga vituo vipya vya kutolea huduma za Afya kwenye maeneo za Kimkakati ambayo hayajafikiwa na huduma sambamba na ujenzi wa nyumba za watumishi.

Kwa Sekta ya Barabara, katika miaka 60 ya Uhuru, Tanzania Bara imepata mafanikio makubwa katika sekta ya barabara ambayo yenye mchango muhimu katika kuinua uchumi wa Taifa.

Juhudi za Serikali zimewezesha mtandao wa barabara zinazosimamiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuongezeka kutoka kilometa 17,600 zilizokuwepo mwaka 1961 hadi kufikia kilometa 144,429.77 mwaka 2021, hivyo barabara nzuri na za wastani kutoka kilometa 61,798.45 hadi kilometa 77,078.69 ikiwa ni ongezeko la kilometa 15,280.24 ambayo ni ongezeko la asilimia 24.72.

Julai Mosi mwaka 2017, Serikali iliunda Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini -TARURA na kwa sasa mtandano wa barabara za lami umeongezeka kutoka kilometa 1,325.49 hadi kilometa 2,404.90 ongezeko kilometa 1,079.41 sawa na asilimia 81.47, barabara za changarawe kutoka kilometa 22,088.79 hadi kilometa 29,166.57 sawa na ongezeko la kilometa 7,077.78 ambazo ni sawa na ongezeko la asilimia 32.04

Ongezeko la bajeti ya ujenzi na matengenezo ya barabara kutoka Shilingi Bilioni 94.020 katika mwaka wa fedha 2011/12 hadi Shilingi Bilioni 966.90 katika mwaka wa fedha wa 2021/22 sawa na ongezeko la asilimia 927

Ndani ya miaka 60 ya Uhuru, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na vituo vya kutoa huduma za afya na elimu imepiga hatua katika uwekaji na matumizi ya miundombinu, vifaa na mifumo ya TEHAMA.

Kuanzia mwaka 1961 mpaka 1999, hakukuwa na matumizi ya mifumo ndani ya Ofisi hii na mageuzi yalianza mwaka 1999 ambapo mifumo ya kwanza kuanzishwa ya usimamizi wa fedha za umma (Epicor/Platnum), ukusanyaji wa taarifa (LGMD) na mifumo ya upangaji wa mipango na bajeti (PlanRep), tovuti, barua pepe na intaneti.

Kutokana na maboresho ya mwaka hadi mwaka yamefanikisha matumizi ya mifumo katika Mikoa yote 26, Halmashauri zote 184 na baadhi ya Taasisi, Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Shule za Sekondari.



# Sekta ya Madini Yachangia Tsh Bilioni 584.8 Kwenye Pato la Taifa 2021

Na **Nuru Mwasampeta na Asteria Muhozya**

**Baada ya Uhuru, shughuli chache za uchimbaji zilifanyika ambapo Mgodi wa kwanza kuanzishwa mwaka 1984 uliiitwa Nyarugusu Gold Mine. Inaelezwa kuwa, katika kipindi hicho, mgodi huo ulizalisha kilo 82.2 za dhahabu.**



Doto Biteko
Waziri wa Madini

Shughuli za uchimbaji na biashara ya madini nchini Tanzania zimekuwepo kabla na baada ya Uhuru wa Tanzania Bara Mwaka 1961. Kabla ya Uhuru, shughuli za madini na biashara ya madini hazikuwa kubwa, wakati huo uchimbaji wa madini ulisimamiwa na Sheria ya Madini ya Mwaka 1920 (The Mining Ordinance 1920), ambapo biashara zilizofanyika zilikuwa za kufua vito chini ya Sheria ya Goldsmiths na Silversmiths Ordinace 1937 ambayo ilihusu usimamizi wa udhibiti wa biashara ya dhahabu.

Baada ya Uhuru, shughuli chache za uchimbaji zilifanyika ambapo mgodi wa kwanza kuanzishwa mwaka 1984 na uliiitwa Nyarugusu Gold Mine. Inaelezwa kuwa, katika kipindi hicho, mgodi huo ulizalisha kilo 82.2 za dhahabu. Awali, miaka ya 1965 mpaka 1975 Bunge lilipitisha Sheria ya 'The National Investment Promotion and Protection Act' ambayo ilisimamiwa na Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) kwa kuendeleza shughuli chache za uchimbaji na biashara ya madini. Uchache wa shughuli za uchimbaji madini ulitokana na Serikali kuhifadhi rasilimali za madini hadi muda ambao Taifa litapata utaalamu na wataalamu katika Sekta ya Madini yaani wanajiosayansi wa kusimamia na kuendesha shughuli za uchimbaji kwa ufanisi.

Msukumo mpya katika Sekta ya Madini ulitokana na mataifa ya kigeni kugeukia Bara la Afrika baada ya kufanya shughuli hizo katika Bara la Amerika ya Kusini kupitia Mikataba ya Uchimbaji (Mineral Development Agreements) na kujipatia uzoefu ulioyafanya mataifa ya Ulaya na Amerika kuhamishia mitaji katika Bara la Afrika. Wawekezaji walifika katika nchi za Magharibi ya Afrika kama vile Ghana, Nigeria, Liberia na Siera Leone wakitumia taratibu na Sheria zilizotumika katika Bara la Amerika ya Kusini ambapo walikuwa wakiendesha shughuli hizo. Hii ilikuwa ni pamoja na umiliki wa maeneo na madini yote yaliyopatikana na kuzuia Mamlaka ya nchi kuingilia shughuli zilizofanyika katika migodi.

Mara baada ya vita baina ya Tanzania na Uganda, mwaka 1978/79, Tanzania haikuwa na fedha za kutosha kujiendesha na katika kuhakikisha Serikali inajiendesha na huduma zinatolewa kwa Wananchi, Bunge lilitunga Sheria ya Madini mwaka 1979 ambapo Wawekezaji katika sekta ya rasilimali ya madini walianza kuingia nchini mwanzoni mwa miaka ya 1990 ambapo makampuni yaliyowekeza katika uchimbaji madini yaliitaka Serikali kuwapatia masharti nafuu ya uwekezaji katika madini ikiwemo kupewa uhakika wa kuweka fedha zitokanazo na uchimbaji au mauzo ya madini katika benki za nje, kusamehewa kodi ya makampuni, kuleta kutoka nje ya nchi wataalam wa kuendesha mitambo na watumishi wengine kama watakavyoona inafaa.

Tanzania ilitunga upya Sera ya Madini 1997 na Sheria ya Madini 1998. Ilifanya mabadiliko makubwa katika Sheria za kodi kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali ya mwaka 1997. Kimsingi, Sheria ya Madini ya mwaka 1998 haikufanya mabadiliko mengi ukilinganisha na Sheria ya Madini ya mwaka 1979. Sheria ya mwaka 1979 na 1998 zilishindwa kutekeleza mambo kama kufungamanisha Sekta ya Madini na Sekta nyingine za maendeleo na zilitoa manufaa zaidi kwa wawekezaji katika rasilimali ya madini hali iliyosababisha malalamiko kutoka kwa wananchi na kamati mbalimbali ziliundwa na kutoa ripoti ya namna Taifa linavyoweza kufaidika zaidi na madini.

Tangu wakati huo, Sheria ya Madini imekuwa ikifanyiwa marekebisho mara kwa mara kadri inavyoonekana kufanya hivyo kwa mfano, mwaka 2009 Serikali ilitunga upya Sera ya Taifa ya Madini na kufuatiwa na Sheria ya Madini ya Mwaka 2010. Hata hivyo, Sera ya Madini ya Mwaka 2009 na Sheria ya Madini 2010, zilishindwa kutekeleza mambo kama kufungamanisha Sekta ya Madini na Sekta nyingine za maendeleo, zilishindwa kuongeza mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa ukilinganisha na ukuaji wake, kudumaa kwa sekta ya uchimbaji mdogo na serikali kutokuwa na uwezo wa kutosha kusimamia sekta ya madini na uharibifu wa mazingira.

Mwaka 2017 yalifanyika marekebisho makubwa katika Sheria ya Madini ya Mwaka 2010. Malengo Makuu ya marekebisho hayo yalifanyika kupitia Sheria ya marekebisho ya Sheria mbalimbali Na.7 ya mwaka 2017 ambayo yalilenga kuweka masharti yatakayowezesha wananchi na Taifa kunufaika zaidi na maliasili ya madini yaani dhana ya 'Permanent Sovereinty over Natural Resources'.





Ili kuwezesha kupatikana kwa manufaa hayo, masharti yafuatayo yaliingizwa kwenye Sheria ya Madini ya Mwaka 2010; kwanza ni Kutambua na kuweka umiliki wa rasilimali madini, petrol na gesi asilia kwa wananchi chini ya usimamizi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa niaba ya Wananchi, pili ni kuweka umiliki wa rasilimali madini kwa Serikali bila kuathiri masharti ya Mikataba iliyoingiwa na makampuni ya uwekezaji. Hii ina maana kwamba mikataba ya madini kabla ya marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 yaliyofanyika Mwaka 2017 ilikuwa inahamishia umiliki wa madini kwa wawekezaji na kusababisha mikataba kuwa na nguvu zaidi ya sheria ya madini.

Aidha, marekebisho ya Sheria ya Madini 2010 yaliyofanyika Mwaka 2017 yalilenga kutambua haki ya ushiriki wa Serikali (Government participation) katika shughuli zote za uchimbaji, uchakataji na uchenjuaji wa madini na ununuzi wa hisa katika makampuni ya kuchimba madini umiliki wa hisa kwa asilimia 16 (16 non dilutable free carried interest) na Serikali kuwa na Uwezo wa kuongeza ushiriki (Umiliki) mpaka asilimia 50 kwa kuzingatia thamani ya vivutio vya uwekezaji na kikodi alivyopewa muwekezaji. Haya yamewezekana na yanatekelezwa ndani ya miaka 60 ya uhuru.

Pamoja na hayo, Serikali imeweza kuondoa utaratibu wa sasa wa Mikataba ya Uendelezaji wa Madini na kuweka msingi utakaowezesha Serikali kufanya majadiliano na wawekezaji katika Sekta ya Madini kwa lengo la kupitia upya baadhi ya masharti hasi kwenye mikataba iliyokwishafanyika. Baada ya marekebisho yaliyokuwa yakifanywa kwa vipindi tofauti ikiwemo yale ya Mwaka 2017 hivi sasa Taifa linashuhudia mapinduzi makubwa ya kiuchumi, viwanda na maendeleo kwenye sekta ya Madini kupitia Taasisi za Wizara zinazosimamia masuala mbalimbali kwenye Sekta ya hiyo.

Vilevile, Marekebisho makubwa ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 yaliwezesha kuundwa na kuanzishwa kwa Tume ya Madini ili kuboresha usimamizi na kuongeza udhibiti katika Sekta ya Madini. Tume ya Madini imekuwa ni Taasisi inayotekeleza majukumu yake kwa mafanikio makubwa.

Kupitia Tume ya Madini, Serikali imeanzisha jumla ya Masoko ya Madini 49 na Vituo 52 vya Ununuzi wa Madini nchi nzima na hivyo kurahisisha biashara ya Madini nchini kwani masoko hayo licha ya kuwezesha serikali kukusanya mapato ya serikali, yamewezesha kuondoa biashara bandia hususan kwenye Madini ya dhahabu, yameweka uwazi kwenye biashara ya Madini na yamevutia nchi nyingi kuja kujifunza namna serikali inavyosimamia masoko hayo na yamekuwa kivutio kwa nchi nyingine kufanya biashara kupitia masoko hayo.

Wizara ya Madini ina taasisi zinazotekeleza majukumu ya kisekta, miongoni mwake ni Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kuanzisha Kiwanda cha kisasa cha kwanza nchini cha kusafisha Dhahabu kwa kiwango cha kimataifa cha 999.9 purity chini ya Kampuni ya Mwanza Precious Metals Refinery (MMPR). Kiwanda hiki ni cha wabia na Kampuni ya ACME Engineering PTY kutoka Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu na Singapore. Kwa sasa, kiwanda hicho kina uwezo wa kusafisha kilo 480 kwa siku na kinaweza kuongezewa uwezo na kufikia hadi kilo 960 kwa siku kulingana na upatikanaji wa dhahabu. Katika ubia huu, STAMICO inamiliki asimilia 25 na wabia wenza wanamiliki asilimia 75 za hisa. Kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa, Hisa za STAMICO zitakuwa zinaongezeka kwa asilimia 5 kila baada ya miaka miwili hadi zitakapofikia asilimia 51 na wabia asilimia 49. Ongezeko hilo la hisa halitakuwa na gharama yoyote kwa STAMICO. Aidha, mbali na kiwanda hicho, viwanda vingine viwili vya kusafisha dhahabu vimeanzishwa katika mikoa ya Geita na Dodoma.

Aidha, Shirika na mbia mwenza linaendeleza mradi wa Dhahabu wa Buhemba uliopo Butiama, Mkoani Mara. Katika Ubia huo, STAMICO itakuwa na asilimia 35 na Kampuni ya GOODFIELD International DMCC ya Dubai asilimia 65 kupitia leseni ya uchimbaji madini. Uchimbaji wa dhahabu katika mradi huo unatarajia kufanyika kwenye miamba migumu katika maeneo ya Ilasaniro, Kilamongo, Mwizi, Buhemba Kuu na Buhemba. Kutokana na utafiti wa awali, mradi wa dhahabu wa Buhemba unakadiriwa kuwa na kiasi cha takriban wakia 600,000 za dhahabu na zinatarajia kuongezeka baada ya kukamilika kwa uchorongaji utafiti wa ziada wa miamba.

## BAADA YA UHURU

Pia, katika kipindi hiki cha baada ya uhuru serikali ilihamisha umiliki wa Mgodi wa Biharamulo (Tulawaka) uliokuwa ukimilikiwa na Pangea Minerals Limited (PGM) kuwa chini ya Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kwa asilimia 100 na kuanzisha Kampuni tanzu ya STAMIGOLD kusimamia mgodi huo ambao unasimamiwa na wataalam wazawa Watanzania.

Vilevile, katika kipindi cha miaka 60 baada ya Uhuru, Serikali ilikamilisha taratibu za kisheria za kuurejesha Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira Serikalini mnamo Desemba 2013 kutoka Kampuni ya TanPower Resources Limited. Mgodi huo kwa sasa unamilikiwa na Serikali kupitia STAMICO kwa asilimia 100. Haya ni mafanikio makubwa kwani sasa Serikali kupitia shirika hili inamiliki migodi yake yenyewe.

Kwa haraka mabadiliko yaliyofanywa na Serikali katika sheria za madini zilizopita hadi sasa imetoa nafasi kwa Serikali kuwa na umiliki katika kampuni na kushiriki katika shughuli za madini kupitia STAMICO. Ukiangalia historia tulipotoka na sasa ni dhahiri kuwa mambo makubwa yamefanyika tangu uhuru katika Sekta ya Madini nchini. Aidha, shirika lenyewe limepitia vipindi mbalimbali tangu kuanzishwa kwake mwaka 1972 hadi sasa na mafanikio yake hivi sasa yanaonekana wazi...

**inaendelea**

**"Tangu kufufuliwa kwake hadi mwaka 2015, STAMICO imepata mafanikio makubwa ikiwemo, Kusainiwa kwa Hati ya Marekebisho ya Uanzishwaji wa Shirika (Establishment Order) na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania. Hati hiyo italiwezesha Shirika kufanya shughuli zake kibiashara ikiwa ni pamoja na kuruhusiwa kumiliki na kuendeleza migodi.**

Tukiangazia Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST), hii ni taasisi kongwe na yenye uzoefu mkubwa katika masuala ya utafiti wa madini (mineral explorations) na uratibu wa majanga asili ya jiolojia katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Taasisi hii ilitokana na Idara kongwe ya Serikali ya Mwingereza iliyojulikana kama Idara ya Jiolojia na ilianzishwa rasmi tokea Mwaka 1925. Kuanzishwa kwa GST kulichangiwa kwa kiasi kikubwa na mabadiliko yaliyokuwa yanatekelezwa na Serikali ikiwa ni juhudi za kuvutia wawekezaji katika sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Madini.

Kwa kipindi cha miaka 60 ya uhuru (GST) mpaka sasa imefanikiwa kutambua jiolojia ya nchi nzima kwa asilimia 96. Ikiwa sehemu ya juhudi za kuimarisha upatikanaji, utunzaji na usambazaji wa taarifa, GST imefanikiwa kuboresha mfumo wa usambazaji wa taarifa/takwimu za jiosayansi. Uanzishwaji wa mifumo hii umerahisisha kwa kiasi kikubwa upatikanaji na usambazaji wa taarifa hizi kwa wadau.

Pamoja na mafanikio hayo, GST kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo imefanikiwa kufanya tafiti mbalimbali katika Sekta ya Madini na jiosayansi, ambazo ni ukamilishaji uandaaji wa Ramani za jiokemia za nchi nzima (Country Wide Mult-Element Geochemical Maps) zinazoainisha wingi wa madini ya aina mbalimbali za metali (k.m. dhahabu, shaba, chuma, nikeli, bati n.k.) katika sehemu mbalimbali nchini zimetengenezwa. Kazi hii imefanywa kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ambao ni Geological Survey ya Finland na Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA).

Aidha, GST imefanikiwa kufanya tafiti kwenye madini mkakati kama ya Gesi ya Helium ambapo utafiti huo umeibua maeneo mapya kwenye ukanda wa kaskazini tofauti na ilivyozoeleka kuwa helium hupatika maeneo ya kusini. Kwa mujibu wa taarifa za kitafiti za gesi hiyo, Tanzania ina kiasi cha ujazo wa bilioni 54 cha gesi hiyo ambacho kinaizidi nchi ya Marekani yenye hazina ya futi za ujazo bilioni 24.2.

## Miaka 60 ya Uchumi imara kupitia Sekta ya Madini na Maendeleo Endelevu yanaonekana.

Aidha, kutokana na kuboreshwa kwa vifaa na miundombinu ya Maabara ya GST sasa inaendeshwa kwa kufuata viwango vya kimataifa vya ISO 17025:2017 na ilipata ITHIBATI (ACCREDITATION) katika viwango hivyo kutoka Shirika la Viwango la Kimataifa la SADCAS. Hivyo, matokeo ya uchunguzi kutoka maabara ya GST yanakidhi viwango vya kimataifa.

Vilevile, katika juhudi za kuinua Sekta ya Madini nchini ndani ya Serikali ya Awamu ya Tano, GST imefanikiwa kuandaa Ramani inayoonesha viwango vya ubora wa PH (pH values) kwenye udongo nchi nzima imechorwa/imetengenezwa. Ramani hiyo inaonesha maeneo yenye PH ndogo na kubwa ambayo ni mikoa ya Mbeya, Njombe, Dodoma-Singida, Manyara, Arusha, Shinyanga na Kigoma.

Sambamba na mafanikio haya GST inaamini kuwa upatikanaji wa taarifa sahihi za jiosayansi kupitia tafiti mbalimbali kutawezesha azma ya Serikali kwa Sekta ya Madini kufikia asilimia 10 katika kuchangia Pato la Taifa ifikapo mwaka 2025 kama Dira ya Maendeleo ya Taifa, na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/2017– 2020/2021 unavyoelekeza.

Serikali kupitia Wizara ya madini imekuwa na mafanikio katika kipindi chote cha kuboresha sheria na mikataba ikiwemo kuongeza uwazi na ushiriki wa Watanzania katika sekta ya madini. Mathalan, kufuatia juhudi hizo, Serikali imefanikiwa kusaini Mikataba ya Ubia na Kampuni ya LZ Nickel ya nchini Uingereza na kuanzisha Kampuni ya Tembo Nickel Corporation Limited yenye Kampuni tanzu mbili ambazo ni Kampuni ya uchimbaji wa madini ya Tembo Nickel Mining Company Ltd na Kampuni ya Usafishaji wa Madini ya Tembo

Nickel Refinery Company Ltd.

Aidha, Serikali imetoa Leseni za uanzishwaji wa Mgodi Mpya Mkubwa wa Uchimbaji Dhahabu wa Nyanzanga utakaojengwa kijiji cha Sotta Wilayani Sengerema Mkoani Mwanza na Mgodi Mkubwa wa uchimbaji madini ya Rare Earth elements utakaojengwa kijiji cha Ngwale Mkoani Songwe.

Aidha, katika kuweka wazi kwa umma ripoti za Ulinganishi wa malipo ya kampuni za madini, mafuta na gesi asilia na mapato ya Serikali kwa kipindi cha Julai 1, 2018 hadi Juni 30, 2019, Tanzania imechapisha na kutoa ripoti kumi na moja (11) zinazolinganisha kodi na malipo mengine yaliyofanywa na kampuni za mafuta, gesi asilia kwa Serikali Kuu na Halmashauri ambazo zinapokea tozo (Service levy). Ripoti hizo zinaonyesha kuwa Serikali imeshapokea kiasi cha jumla ya bilioni U$ 3.78 kutoka katika kampuni zilizofanyiwa ulinganishi wa fedha zilizolipwa na makampuni hayo na fedha zilizopokelewa na Serikali.

Ama kwa hakika madini ya Tanzania yametoka kumilikiwa na wachache ambapo awali madini yaliyochimbwa na eneo lote ilikuwa mali ya mwekezaji. Aidha, uchumi wa Tanzania kupitia Sekta ya madini tulipo sasa unaonekana ukilinganisha na mahali Sekta hii ilipotoka.

Miaka 60 ya Uchumi imara kupitia Sekta ya Madini na Maendeleo Endelevu yanaonekana.



# Miaka 60 ya Uhuru: Vijana Wapatiwa Ujuzi, Wajiepusha na Dawa za Kulevya, Wajikita kwenye Uzalishaji

Na **Mwandishi Wetu- Ofisi ya Waziri Mkuu**

Programu ya kuwajengea vijana uwezo katika kilimo cha kisasa kupitia teknolojia ya kitalu nyumba

**Utengaji wa** Ekari
**217,882.32**

**Vijana**
**3,232**

**Halmashauri**
**111**
zikiendelea kutoa asilimia nne ya mapato yake kwa ajili ya kuwapa vijana mikopo isiyokuwa na riba.

> **Maambukizi mapya kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto yameshuka kutoka 18% mwaka 2010 hadi 7% mwaka 2020"**
> Mhe. Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu



Vijana ni kundi muhimu sana katika ujenzi wa Taifa. Mbali na kazi nyingine, tangu mwaka 1961 Ofisi ya Waziri Mkuu imekuwa ikichukua jitihada za dhati za kujenga vijana wenye afya, maarifa na uzalendo kwa lengo la kuhakikisha nchi yetu inasonga mbele katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Katika hatua zake za kujenga Taifa imara, Ofisi hii adhimu imekuwa ikipambana dhidi ya UKIMWI na dawa za kulevya.

Sanjari na hatua hiyo muhimu, Ofisi ya Waziri Mkuu imekuwa ikishirikiana na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) kuhakikisha vijana wanapata ujuzi na uzoefu pamoja na kuhakikisha vijana hao wanapata sehemu za kufanya shughuli za staha za kujitafutia riziki halali.

Aidha, Ofisi hii imekuwa ikichukua jitihada za dhati kuhakikisha vijana hao wanaishi maisha ya staha baada ya kustaafu.

Mnamo Novemba 2021, akiwa jijini Dodoma kwenye mkutano wa waandishi wa habari, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu), Mhe. Jenista Mhagama aliwaeleza Watanzania mafanikio yaliyopatikana katika miaka 60 ya uhuru wa Tanzania Bara katika sekta anazosimamia.

Akizungumzia mapambano dhidi UKIMWI, Waziri huyo amesema vifo vitokanavyo na UKIMWI vimepungua kwa 50% kutoka vifo 64,000 mwaka 2010 hadi vifo 32,000 mwaka 2020 huku akihabarisha kuwa maambukizi mapya ya VVU kwa watu wazima (miaka 15 na zaidi) nchini Tanzania yameshuka kutoka 110,000 mwaka 2010 hadi 68,000 mwaka 2020.

"Maambukizi mapya kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto yameshuka kutoka 18% mwaka 2010 hadi 7% mwaka 2020," amearifu Mhe. Mhagama.

Kuhusu vita dhidi ya dawa za kulevya, Waziri Mhagama amesema uingizaji wa dawa za kulevya umepungua kwa asilimia 90 na kwamba mnamo 2011 Serikali ilianza kuwapa tiba vijana waliothirika na dawa za kulevya ambapo kuanzia vijana waathirika 3,500 walipatiwa matibabu kuanzia mwaka 2011 hadi 2016.

Pamoja na hayo, Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) ina vituo 11 vinavyotoa tiba kwa zaidi ya waathirika 10,565 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Songwe, Arusha, Tanga, Dodoma na Pwani.

Vilevile, Asasi za Kiraia zimeanzisha Nyumba 31 za Upataji Nafuu (Sober Houses) ambazo huwahudumia waraibu wa dawa za kulevya kwa kuwapitisha kwenye hatua 12 za upataji nafuu bila kutumia dawa ya aina yoyote.
Aidha, Mhe. Mhagama amesema Serikali imetoa mafunzo ya ukuzaji ujuzi kwa njia ya uanagenzi kwa vijana 43,381 tangu yalipoanzishwa mafunzo hayo mwaka 2018 ambapo kwa sasa vijana 14,440 wanaendelea kupokea mafunzo haya.

Pia, vijana 6,300 wamepatiwa mafunzo ya utarajali ambapo vijana wengine 2,591 wanaendelea kupokea mafunzo haya huku mfumo wa urasimishaji Ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa mafunzo ukiwanufaisha vijana 20,334 na kwamba vijana 4,316 wanaendelea kurasimisha ujuzi wao.

"Tangu mwaka 2020/2021, Serikali imekuwa ikitoa mafunzo ya kujenga uwezo kwa waliopo makazini kwa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ambapo mpaka sasa kwa sekta binafsi wafanyakazi 1,550 na sekta ya umma 2,400 wamejengewa uwezo," ameeleza Waziri Mhagama.

Hadi mwaka 2020 viwanda vilivyopo nchini vimeajiri zaidi ya watu laki nne na kwamba zaidi ya watu laki tano wanafanya kazi kwenye utumishi wa umma.

Sambamba na hayo, mwaka 2019 Serikali ilianza kutekeleza programu ya kuwajengea uwezo katika kilimo cha kisasa kupitia teknolojia ya kitalu nyumba ambapo vijana 12,580 wamenufaika katika mikoa 17 na halmashauri 117. Kati ya hao, vijana 2,340 walipatiwa mafunzo ya kujenga vitalu nyumba.

Hatua hiyo inaenda sambamba na utengaji wa maeneo yenye ukubwa wa ekari 217,882.32 yaliyotolewa kwa zaidi ya vijana 3,232 katika halmashauri 111 huku halmashauri zote zikiendelea kutoa asilimia nne ya mapato yake kwa ajili ya kuwapa vijana mikopo isiyokuwa na riba.

Aidha, Serikali kupitia mifuko ya hifadhi ya jamii imekuwa ikihakikisha vijana wanaofanya kazi serikalini na sekta binafsi wanachangia kwenye mifuko hiyo ili fedha hizo zinazotokana na matumizi sahihi ya ujana wao ziwafae wanapofikia umri wa uzee.

**"Tangu mwaka 2020/2021, Serikali imekuwa ikitoa mafunzo ya kujenga uwezo kwa waliopo makazini kwa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ambapo mpaka sasa kwa sekta binafsi wafanyakazi 1,550 na sekta ya umma 2,400 wamejengewa uwezo**

Mhe. Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu


NATIONAL DEFENCE COLLEGE


Check - In


MUHIMBILI ORTHOPAEDIC









# Natamani Kuanzisha Elimu ya Watu Wazima ya TEHAMA: Balozi Mongella

Na **Jonas Kamaleki**

Miaka 60 ya Uhuru mambo mengi mazuri na ya kupigia mfano yamefanyika nchini ikiwemo matumizi ya teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kama anavyotafakari mwanasiasa mkongwe na kiongozi shupavu, mtetezi wa wanawake duniani, Mhe. Balozi Getrude Mongella.

Katika mahojiano maalum na Jarida la NCHI YETU, Balozi Mongella anasema katika miaka 60 ya uhuru Tanzania imepiga hatua katika mawasiliano ya kidigitali lakini si kwa wote, anataka watu wazima wapate elimu ya TEHEMA ili wasitengwa na ulimwengu wa kidijitali.

"Ningekuwa na nguvu ningeanzisha Elimu ya TEHAMA ya Watu Wazima ili kuhakikisha watu hao hawaachwi nyuma na teknolojia hiyo", anasema Balozi Mongella.

Ameongeza, "Digital illiteracy itatutenga na ulimwengu wa sasa hivyo inabidi tujitahidi kuikumbatia TEHAMA kwa nguvu zote".
Tathmini ya miaka 60 ya uhuru inadhihirisha kuwa Tanzania imepiga hatua katika kuboresha miundombinu ya barabara, madaraja, umeme na maji.

Balozi Mongella anasema kuwa nishati ya umeme imeleta ukombozi mkubwa kwa Watanzania hasa waishio vijijini. "Nilipokwenda Ukerewe na wanangu walishangaa kuona vibatari au koroboi hadi wakawa wanashika hivyo vibatari… anacheka kidogo,.. halafu wanapuliza na kuvizima…kwa sasa Ukerewe tuna umeme hadi vijijini, kweli maisha yamebadilika," anasisitiza Mwanasiasa Mkongwe, Balozi Mongella.

Amani, utulivu, mshikamano na umoja ni tunu za Taifa ambazo zimeifanya Tanzania iwe nchi nzuri na ya kupendeza, kwa mujibu wa Balozi Mongella.

"Pengine tunaropoka, tunasema lolote wala hatubughudhiwi, hatuna mizozo, hatuulizani makabila…anatulia kidogo na kusema kwa tabasamu, Mimi ni Mkerewe lakini niliolewa na Msukuma, Watoto wetu wanaishi vizuri wala la kuwa na wazazi wa makabila tofauti haliwasumbui", Balozi Mongella anasema.

"Ningekuwa na nguvu ningeanzisha Elimu ya TEHAMA ya Watu Wazima ili kuhakikisha watu hao hawaachwi nyuma na teknolojia hiyo

"Kwa sasa Ukerewe tuna umeme hadi vijijini, **kweli maisha yamebadilika.**"

Anaisifu Serikali kwa kujenga hospitali za Rufaa kila mkoa, za wilaya, vituo vya afya karibu kila kijiji na kuboresha huduma za utoaji wa afya kwa kuweka vifaa vya kisasa na wataalaam wa kutmia vifaa tiba hivyo kama CT- Scan, MRI na X- Rays za kisasa.

Miaka 60 ya Uhuru Tanzania ina mambo mengi ya kujivunia ikiwepo kuboresha usafiri wa anga kwa kununua ndege mpya 11, majini na nchi kavu bila kusahau ujenzi wa Reli ya kisasa (SGR) na Bwawa la Kufulia Umeme la Julius Nyerere litakalozalisha Megawati 2115.















Awamu ya Kwanza



Awamu ya Pili



Awamu ya Tatu



Awamu ya Nne



Awamu ya Tano



Awamu ya Sita

# Mabaraza ya Mawaziri Tanzania kuanzia Awamu ya Kwanza hadi ya Sita 1962-2021

60

1961-2021

**MIAKA 60 YA UHURU;**
**Tanzania imara, Kazi iendelee.**




Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama nchini na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan,










Air Tanzania



# Tanzania Kuendeleza Jitahada za Kukuza Uchumi

Na **Mwandishi Wetu - MAELEZO**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan amesema kuwa Tanzania inaendelea kuwa kati ya nchi 10 za Afrika ambazo uchumi wake unakua kwa kasi ikiwa ni mafanikio ya miaka 60 ya Uhuru.

Akifungua mkutano wa taasisi za fedha hapa nchini uliolenga kuweka mikakati ya pamoja ya kupambana na athari za UVIKO-19 uliofanyika Novemba 25, 2021 jijini Dodoma, Mhe. Rais Samia amesema kuwa ugonjwa huo umeifanya Tanzania kuchukua hatua mbalimbali zilizopunguza athari za ugonjwa huo.

"Mafanikio tuliyopata katika kipindi hiki tunapoelekea kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru ni pamoja na kuongezeka kwa umri wa kuishi kutoka wastani wa miaka 50 hadi 66, na pia Julai 2020 Tanzania iliingia uchumi wa kati, kupungua kiwango cha umasikini kutoka asilimia 28.6 mwaka 2015 hadi 26.2 mwaka 2020," aliarifu Rais Samia.

Mhe. Rais ameeleza kuwa Tanzania imeweza kudhibiti mfumuko wa bei na thamani ya shilingi imeendelea kuimarika kutokana na hatua zilizochukuliwa na Serikali ikiwemo kuruhusu wananchi waendelee na shughuli za uzalishaji hata wakati wa janga la UVIKO-19.

Rais Samia amehabarisha kwamba pamoja na uchumi kushuka kutoka ukuaji wa wastani wa asilimia 6.8 hadi 4.8 mwaka 2020/2021, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kuyaomba Mashirika ya Kimataifa kuifutia madeni Tanzania na kuipa mikopo ya masharti nafuu ili iendeleze mapambano dhidi ya athari za UVIKO-19 ambapo tayari Shirika la Fedha Duniani limeipatia Tanzania mkopo wa shilingi trilioni 1.5 zinazosaidia kupunguza athari za kiuchumi zilizosababishwa na janga hilo.

Sanjari na hayo, Mhe. Rais amefahamisha kuwa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imetenga shilingi trilioni 1.5 kwa ajili ya kukopesha benki za biashara ili nazo ziwakopeshe wananchi kupitia sekta ya kilimo, viwanda na sekta nyingine kwa riba nafuu.

Aidha, Rais Samia amedokeza kwamba dhamira yake ni kuiwezesha sekta binafsi kwa kuendelea kuweka mazingira wezeshi ili iweze kukua kwa kasi na kuondokana na athari za UVIKO-19.
Zaidi ya hayo, Mhe. Samia amebainisha kuwa Serikali inakamilisha Sera na Mkakati wa Kukuza Uchumi Kidigitali kwa kutumia tafiti na ubunifu sambamba na kuendelea kuwekeza kwenye rasilimali watu ili kuchochea ukuaji wa uchumi.

Kwa upande wake, Gavana wa BoT, Prof. Florens Luoga amesema Tanzania imeendelea kuwa na utulivu wa bei za bidhaa na huduma hali iliyochangia kutokuwepo kwa mdororo wa kiuchumi licha ya kuwepo kwa ugonjwa wa UVIKO-19 ikilinganishwa na nchi nyingine.

Prof. Luoga amewajulisha Watanzania kuwa BoT imepunguza amana inayowekwa Benki Kuu na Benki za Biashara kwa lengo la kutoa unafuu kwa mabenki yatakayotoa mikopo katika sekta za kilimo na viwanda ili kuzifungua sekta hizo na kukuza uchumi.
Aidha, ameongeza kuwa Tanzania imeweza kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosheleza mahitaji kwa kipindi cha miezi zaidi ya sita kwa sasa.

"Matarajio yetu ni kukuza uchumi kwa wastani wa asilimia nane kwa kipindi cha miaka mitano ijayo kutokana na hatua zinazochukuliwa na Serikali kwa sasa," amedokeza Prof. Luoga.

# Miaka 60 na Mapinduzi ya Sekta ya Maji

Na **Mwandishi Wetu, Wizara ya Maji**

Na Mwandishi Wetu, Wizara ya Maji
"Maji ni Uhai" ni usemi ambao umekuwa ukisikika kwa masikio ya walio wengi. Miaka 60 ya uhuru, Tanzania imeshuhudia miradi mikubwa ya maji inayolenga kuwapatia wananchi maji safi na salama na yenye kutosheleza. Makala hii inajikita katika kuelezea juhudi ambazo Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imetekeleza na inaendela kutekeleza.

Katika kipindi cha mwaka 1961 hadi 2021, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo (Development Partners) kupitia Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Maji (WSDP) pamoja na Taasisi mbalimbali nchini imetekeleza miradi mikubwa mbalimbali ya majisafi na usafi wa mazingira nchini katika maeneo tofauti mijini. Utekelezaji wa miradi mikubwa ya maji umefanyika kati ya mwaka 1961 na 2021.

Serikali katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2009, ilikamilisha kazi za ujenzi wa mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria hadi miji ya Kahama na Shinyanga kwa gharama ya shilingi bilioni 252. Utekelezaji wa Mradi huu wa maji mkubwa kuliko yote nchini uliotekelezwa kwa fedha za Serikali tu. Kukamilika kwa mradi huu kumeboresha huduma ya maji katika miji ya Shinyanga, Kahama na Vijiji vipatavyo 76 kando ya bomba kuu.

Sanjari na utekelezaji huu, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya India imekamilisha ujenzi wa bomba kuu lenye urefu wa Kilomita 281 kutoka Kijiji cha Solwa (Shinyanga) kwenda katika miji ya Tabora, Nzega na Igunga. Mradi umelenga kusambaza maji mita za ujazo 54,145 kwa siku na kuongeza upatikanaji wa maji katika Miji ya Tabora, Nzega, Igunga kwa asilimia 100, na jumla ya vijiji 142 katika Wilaya za Shinyanga Vijijini, Nzega, Igunga na Uyui. Gharama ya Mradi ni Dola za Marekani milioni 268.35.

Mradi huu ulizinduliwa na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati John Magufuli mnamo tarehe 23/2/2020 na unahudumia zaidi ya wakazi milioni 1.2 katika miji hiyo.

Mradi wa maji Chalinze ulijengwa kwa ajili ya kusambaza maji katika vijiji vya Wilaya za Bagamoyo na Morogoro Vijijini. Awamu ya kwanza iliyogharimu Shilingi bilioni 23.4 ilihusisha vijiji 20 Wilayani Bagamoyo imekamilika. Ujenzi wa awamu ya pili inayohusisha vijiji 48 umekamilika. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya India inaendelea kutekeleza awamu ya tatu kwa gharama ya Shilingi bilioni 41.3. Mradi wa Chalinze awamu ya tatu umelenga kunufaisha vijiji 68 ambapo vijiji 19 viko kaskazini na 49 viko kusini mwa mto Wami.

Serikali kwa kushirikiana na BADEA, OFID, SAUDI Fund na Kuwait Fund inatekeleza mradi wa maji wa Same – Mwanga – Korogwe unaotekelezwa katika miji ya Same na Mwanga pamoja na vijiji 38 vilivyomo kandokando ya bomba kuu katika Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe. Mradi utakapokamilika utazalisha maji lita milioni 103.7 kwa siku na utawanufaisha wananchi wapatao 438,930 katika Wilaya za Same 246,790, Mwanga 177,090 na Korogwe 15,050. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2021 na utaondoa kero ya maji ya muda mrefu kwa wananchi wa maeneo husika.

Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) inatekeleza mradi wa ujenzi wa Miundombinu ya usambazaji majisafi na uboreshaji wa huduma ya uondoshaji wa majitaka katika Jiji la Arusha unaogharimu Shilingi bilioni 520 ambapo AfDB inatoa Shilingi bilioni 492.612 na Serikali Shilingi bilioni 53.59. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 40 hadi lita milioni 200 kwa siku, muda wa upatikanaji wa huduma ya majisafi kutoka saa 12 za sasa hadi saa 24 kwa siku pamoja na kuongeza huduma ya uondoshaji wa majitaka kutoka asilimia 7.6 za sasa hadi asilimia 30.



Mradi wa upanuzi wa mtambo wa maji wa Ruvu Juu na ulazaji wa mabomba makuu ya maji ya kutoka Mlandizi hadi Dar es Salaam




Mradi wa Maji Kagongwa-Isaka, Wilaya ya Kahama, Mkoani Shinyanga

Vilevile, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya majisafi katika miji mikuu ya mikoa nchini kwa dhumuni la uboreshaji wa upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi kupitia mradi ya kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Dodoma kwa kutekeleza miradi mbalimbali. Wizara imeanza utekelezaji wa mradi wa kutoa maji katika visima vya Ihumwa kwenda tanki la Njedengwa ambao unagharimu Shilingi bilioni 2.4. Hadi mwezi Machi 2021, visima nane (8) vimechimbwa na visima vitatu vya zamani vimekarabatiwa. Kazi ya ufungaji wa miundombinu inaendelea na itakapokamilika inatarajia kuongeza muda wa upatikanaji wa maji kwa wakazi wa Dodoma.

Aidha, Serikali imeendelea kuchua hatua ya uboreshaji wa miundombinu ya majitaka mijini kwa kujenga mipya na baadhi yake kupanuliwa katika miji ya Arusha, Dodoma, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Tabora, Moshi, Tanga, Songea na Iringa. Hii imeongeza huduma ya uondoaji majitaka kufikia asilimia 20 ya wakazi wanaoishi kwenye miji hiyo mwezi Desemba, 2020.

Kwa miji ambayo haina miundombinu ya majitaka, huduma ya uondoshaji wa majitaka hufanyika kwa kutumia magari maalum. Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo imekamilisa ujenzi wa mabwawa ya kutibu na kusafisha majitaka katika Miji ya Sumbawanga, Kahama, Misungwi, Lindi, Magu, Kigoma, Nansio na Lamadi. Vilevile, Serikali inaendelea kuboresha huduma kwa kujenga na kupanua mifumo pamoja na ununuzi wa magari ya uondoshaji majitaka kwa lengo la kufikisha wastani waasilimia 30 ifikapo mwaka 2025.

Aidha, Serikali imefanya uwekezaji mkubwa kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kuhakikisha wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam wenye wakazi wengi na viwanda vingi huduma ya maji inaimarika na kuwa toshelevu kwa kutekeleza miradi takriban 16 (12 imekamilika na miradi 4 inaendelea ikiwa katika hatua mbalimbali) yenye Jumla ya Shilingi 127,416,346,397.33.

Haya ni baadhi ya mafanikio makubwa ambayo Serikali imeyapata katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru katika Sekta ya Maji kwa upande wa maji mijini, wakati mikakati mikubwa ikiendelea kutekelezwa kuhakikisha lengo la Serikali la kufikisha huduma ya maji kwa wakazi wa mijini kwa asilimia 95 ifikapo mwaka 2025 inafikiwa na baadhi ya maeneo yakiwa tayari yamefikia asilimia 100 ya upatikanaji wa huduma.

**Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) inatekeleza mradi wa ujenzi wa Miundombinu ya usambazaji majisafi na uboreshaji wa huduma ya uondoshaji wa majitaka katika Jiji la Arusha unaogharimu Shilingi bilioni 520 ambapo AfDB inatoa Shilingi bilioni 492.612 na Serikali Shilingi bilioni 53.59.**




NEW VICTORIA
HAPA KAZI TU


EMIRATES
APL
msc
CAPITAL








ARUSHA TOURISM
&
DIPLOMATIC POLICE STATION


Posta


PARLIAMENT OF TANZANIA
UHURU NA UMOJA


MHE. SAMIA SULUHU HASSAN
RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MHE. DKT. PHILIP ISDOR MPANGO
MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MH. DKT. HUSSEIN ALI MWINYI
RAISI WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI
MHE. KASSIM M. MAJALIWA
WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA





Disemba, 2021. maelezo.go.tz

1961-2021
MIAKA 60 YA UHURU;
Tanzania imara, Kazi iendelee.


Tanzania imara, kazi iendelee.


Idara ya Habari MAELEZO
S.L.P. 25
Dodoma, Tanzania
Simu: **+255 22 292192**
Barua pepe: **maelezo@mawasiliano.go.tz**
**www.maelezo.go.tz**


Tufuatilie katika kurasa zetu
kwenye mitandao ya jamii

/ Msemaji Mkuu wa Serikali
/Maelezo News